

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Tatu – Tarehe 13 Juni, 2011

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE.PEREIRA AME SILIMA):-

Taarifa ya Mwaka ya Benki Kuu ya Tanzania kwa Mwaka 2009/2010 (*The Annual Report of Bank of Tanzania for the Year 2009/2010*).

NAIBU WAZIRI WA MAJI:-

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Nishati na Maji kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010. (*The Annual Report of Energy and Water Utilities Regulatory Authority EWURA for the year ended 30th June, 2010*).

MASWALI NA MAJIBU

Na. 26

Ujenzi wa Daraja la Igumbilo-Tegamenda

MHE. RITTA E. KABATI aliuliza:-

Daraja la Igumbilo- Tegamenda katika Mto Ruaha linaunganisha Manispaa ya Kilolo na Iringa lakini daraja hilo ambalo limejengwa kwa mbao sio imara na linahatarisha maisha ya watumiaji na uwezo wa Halmashauri wa kulijenga daraja hilo ni mdogo sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kusaidia ujenzi wa daraja mahali hapo ili liweze kuwa salama na kuitika wakati wote?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Ernest Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008/2009 Halmashauri ya Manispaa ya Iringa iliomba fedha kiasi cha Shilingi milioni 172 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Igumbilo-Tegamenda. Fedha zote zimeshatolewa na kazi zilizofanyika ni usanifu wa daraja hilo kwa gharama ya shilingi milioni 16. Baada ya upembuzi yakinifu kufanyika gharama za ujenzi wa daraja hilo ni shilingi bilioni 1.09. Halmashauri imewasilisha maombi maalum Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI ili kupata fedha kwa kazi hilo. Aidha, Halmashauri mbalimbali nchini zimewasilisha maombi maalum kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya barabara na madaraja yanayofikia shilingi bilioni 123 hadi kufikia 2011/2011

Mheshimiwa Spika, maombi yaliyowasilishwa yataendelea kufanyiwa kazi ili kuona uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo muhimu. Aidha, Halmashauri inashauriwa kuendelea kutenga fedha katika bajeti yake ili kutimiza azma ya kujenga daraja hilo.

MHE. RITTA E. KABATI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba Waziri atambue kwamba idadi ya watumaji wa daraja lile ni kama elfu nne na mia mbili na kuna shule ya Sekondari ya Tegamenda kama mia tisa hamsini na tano na kuna Chuo cha Igumbilo. Pia atambue kwamba kuna watoto wa shule wamekwisha poteza maisha.

(a) Je, yupo tayari kuwasiliana na Waziri wa Ulinzi ili tuweze kupatiwa daraja la dharura ili wananchi wale wasiweze kuteseka, kwa sababu pamoja na hayo kuna wanawake wanadhalilika wanapovuka katika lile daraja?

(b) Kwa kuwa kuna utaratibu wa kupandisha barabara za Halmashauri kwenda *TANROAD*. Je, upo utaratibu gani wa kupandisha madaraja kama haya ambayo Halmashauri zimeshindwa kuyajenga?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwa namna anavyopigania maendeleo ya Manispaa ya Iringa. Ni kweli kabisa kwamba si mara ya

kwanza nimemsikia akifuatilia maendeleo haya kwa hiyo mimi napenda kumpongeza sana.

Sasa amesema jambo moja hapa la kuzungumza na Waziri wa Ulinzi, yumo humu ndani najua kwamba ananisikiliza. Mimi sina tatizo kwenda kumwona Mheshimiwa Mwinyi kumwomba kwamba atusaidie hili daraja lina matatizo hapa. Mimi nitafanya kwa sababu ndiyo kazi ninayoifanya. Nina hakika kabisa Mheshimiwa Mkuchika atanisiaidia katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili anazungumzia suala la kupandisha madaraja, utaratibu wa kupandisha madaraja ni kama ule wa kupandisha hadhi kwa maana ya barabara. Waziri mwenye dhamana wa suala hili ni Mheshimiwa Dkt. Magufuli, yeye ndiye anayefanya kazi hii. Nina hakika kwamba ananisikia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, *significance* ya daraja hili linalozungumziwa hapa sisi wote tunalijua na wewe najua ni mdau unatoka huko Iringa kunakozungumzwa. Nikimaliza Bunge hapa nitakwenda Iringa kwa ajili ya kazi hii.

Lakini nichukue nafasi hii kama alivyotuomba Mheshimiwa Mbunge, tumwombe Waziri mwenye dhamana ya kupandisha madaraja haya lakini utaratibu ni lazima wapitishe *DCC, RCC* halafu baadaye maombi haya ndiyo yaende rasmi Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tupo tayari kufanya hivyo. (*Makofii*)

MHE. FREEMAN A. MBOWE-KIONGOZI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI: Mheshimiwa Spika nakushukuru, kwa kuwa suala la madaraja ni suala la msingi ambalo linaweza likahatarisha maisha ya watumiaji na kwa sababu tatizo la Iringa lililozungumzwa hapa na Mheshimiwa Mbunge linafanana sana na tatizo la daraja ambalo linaitwa daraja la Mnepo linalounganisha Jimbo la Hai Mkoaa wa Kilimanjaro na Jimbo la Moshi Vijijini katika Kata ya Machame Weruweru, katika Kijiji cha Mijongweni. Ni daraja ambalo limepata kutolewa ahadi mara kadhaa na viongozi wa Kitaifa akiwemo Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa.

Je, Waziri atatusaidiae katika kutatua hili la daraja la daraja la Mnepo linaloounganisha Kata na vilevile Majimbo mawili ambayo ni muhimu na linatumwa na wananchi walio wengi wakiwemo wanafunzi?

SPIKA: Haya, ingawa ni swali jipya kabisa lakini kwa sababu mnatoka jirani labda unalijua.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOAA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, daraja ninalifahamu, mimi ninamwomba Mheshimiwa Mbwe kwamba tutoke tuende tukaiangalie *status* ya jambo hili tujue vizuri anapozungumza hapa anazungumza nini, kwa sababu daraja moja hapa lile la kwanza lilouliziwa swali hapa ni shilingi bilioni 1.9 ni hela nyingi.

Sasa nikisema kwamba aingize katika Bajeti ya Halmashauri, hela zinazopelekwa katika Halmashauri sana sana hazizidi milioni mia nne na hamsini, kule kwangu Siha ni milioni mia tatu na hamsini, hela tunazokupelekea Hai ni milioni mia nne na ishirini ndizo zinazopelekwa kwa ajili ya barabara. Sasa haya yote ni lazima tuende tukaketi tuangalie kwa pamoja mimi na yeye.

Mheshimiwa Spika, huyu namwita *homeboy* wangu kwa hiyo tutakwenda kuzungumza tutaelewana katika jambo hili ili tujue kwamba itakuwaje.

SPIKA: Itabidi mlete msuluhishi hapo katikati. (*Kicheko*)

Tunaendelea, leo tuna maswali kumi na moja, siku ya Alhamisi hatukujibu maswali. Kwa hiyo, tuna maswali kumi na moja badala ya kumi. Kwa hiyo, nitakuwa napunguza maswali ya nyongeza. (*Makofi*)

Na. 27

Hati Safi na Chafu za Ukagazi wa Hesabu za Halmashauri

MHE. REGIA E. MTEMA aliuliza:-

Kila mwaka Mdhhibit na Mkagazi Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG hufanya Ukagazi kwenye Halmashauri mbalimbali na kutoa Hati safi au chafu au zeny shaka:-

(a) Je, Serikali huchukua hatua gani kwa Halmashauri zilizopata Hati zeny shaka au chafu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa Hali ya namna hiyo haitokei tena kwenye Halmashauri husika?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Serikali kufanya ukagazi ni kupima usimamizi wa Fedha wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kupata thamani ya fedha (*Value for Money*) na kutoa ushauri katika sehemu zeny mapungufu ili kuhakikisha kuwa Fedha za Umma zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, inapogundulika kuwa Halmashauri imepata Hati chafu au yenyenye mashaka, Serikali inatumia sheria na Kanuni zilizopo kuchukua hatua zinazostahili na kulingana na sababu zilizosababisha hali hiyo kutokeea. Hatua hizo ni pamoja na kutoa adhabu, kutoa ushauri, kuzijengea Halmashauri uwezo unaotakiwa, Fedha za Ruzuku ya Maendeleo hazitatolewa endapo Halmashauri imepata Hati chafu.

Kamati ya *LAAC* hupendekeza kwa Waziri mwenye dhamana ya mamlaka za Serikali za Mitaa watumishi waliosababisha ubadhirifu kukatwa sehemu ya Mishahara yao kufidia hasara iliyojitokeza, kusimamishwa kazi, kushushwa vyeo na ikithibitika hupelekwa Mahakamani.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kwamba Hati zenyenye shaka na chafu hazirudii tena katika Halmashauri husika, Serikali inafanya yafuatayo:-

Kuweka usimamizi madhubuti wa mfumo (*Epicor*) wa kudhibiti matumizi ya fedha na kuhakikisha kuwa watumishi wanaweza kutumia mfumo huo, kuhakikisha kuwa wapo watumishi wa kutosha na wenye ujuzi unaotakiwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na kuwajengea uwezo wa kutosha Wakaguzi wa Ndani. Aidha, hivi sasa Wakaguzi wa Ndani wameunganishwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani na sasa hawaripoti tena kwa Mkurugenzi wa Halmashauri. Aidha, mpango wa kuziimarisha sekretariati za Mikoa ili zisimamie Mamlaka za Serikali za Mitaa vizuri kama inavyotakiwa.

MHE. REGIA E. MTEMA: Mheshimiwa Spika nakushukuru, kwa kuwa *CAG* amekuwa akikagua maeneo mbalimbali ya Serikali na kila mwaka amekuwa akigundua kuna ubadhirifu wa fedha za Umma.

(a) Je, hatuoni sasa umefika wakati wa *CAG* kuongezewa meno yeye mwenyewe akigundua ubadhirifu moja kwa moja achukue hatua ili hali hii isiendelee tena?

(b) Ningependa kufahamue. Je, ofisi ya *CAG* na yenyewe inakaguliwa na nani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, swali la kwanza analosema na kuongezewa meno, kama nakumbuka vizuri Mheshimiwa Rais alipokuja hapa kulihutubia Bunge alitoa tamko hapa kwamba *Controller and Auditor General* akienda katika Halmashauri au kwenye Shirika la Umma akakuta kuna ubadhirifu umefanyika pale, aende na polisi.

Mheshimiwa Spika, kauli ya Rais ni Sheria, amesema jambo kubwa sana mimi nina-quote hapa *I want to be concrete*. Lakini sheria hizi anazozisema Mheshimiwa Mtema zimempa mamlaka na madaraka, ukienda ukafanya ukaguzi *CAG* akatoa ripoti anachofanya pale ni *post-mortem*, maana yake ni kwamba hela zimeshaibiwa. Anaweza akatoka pale akamwambia *OCD* na *DC* hebu nakuomba uniitie *OCD* na *DC* waje hapa kamata hawa kuna hela za Serikali zimeibiwa hapa, nguvu nyingine inayotafutwa hapa wala siifahamu.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mtema mimi nafikiri *CAG* ana Mamlaka makubwa sana na sisi kama Wizara tunasaidiana naye. Hivi ninapozungumza hapa tumeshafukuza Wakurugenzi karibu 73 tumewaondoa kabisa kazini. Sasa hivi tunazo kesi kama 78 lakini Wakurungezi 73 tumewaondoa kazini kabisa. Ni mmoja tu ndiyo ame-*clear* pale.

Kwa hiyo hapa muwe na uhakika kabisa kwamba ipo Serikali madhubuti inayojua kwamba inajua nini kuhusu matatizo yanayotokea hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili analoniuliza kwamba *CAG* anakaguliwa na nani, Wizara ya Fedha inakuwa na utaratibu wa *ku-create consultancy* kama nakumbuka vizuri, na wale ndiyo wanaotusaidia kwa ajili ya ukaguzi huu anaouzungumzia wa Ofisi ya *CAG*.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kuwa Naibu Waziri kwenye jibu lake la msingi amekiri kwamba watendaji wanapoonesha ubadhirifu, wakati mwingine Halmashauri hizo hunyimwa fedha za Maendeleo.

Je Serikali haioni kwamba kuwanyima wananchi Fedha za Maendeleo ni kutokuwatenda haki kwa ubadhirifu wa watendaji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hoja yake ninaiona lakini labda nilisaidie Bunge lako hapa. Anachosema ni kwamba kwanini unaiadhibu Halmashauri ya Wilaya ya Singida kwanini usimwadhibu Mkurugenzi Mtendaji au yule *Accountant* wao au wale watumishi waliopo pale wakuu wa Idara.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme hapa kwamba baada ya kuamua kwamba hela zinazopelekwa kwa ajili ya Maendeleo ambazo zinapelekwa pale *fifty percent* inatakiwa ibakie pale katika Halmashauri, hizi hela tumekuwa tunazizuia. Wakati tulipoanza utaratibu huu wa kuzuia hela za maendeleo Halmashauri ambazo zilikuwa na Hati chafu zilikuwa sabini na nane, tulipoanzisha utaratibu huu zikashuka mpaka ikabaki Halmashauri moja ilikuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa mwaka jana. Hivi hivi tunavyozungumza sasa hivi zimepanda tena zimekuwa nne, Halmashauri ya Wilaya ya Rombo, Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa, na Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga. Kwanini tunafanya hivi? ili kuzuia hizi hela zisiende kule. Zinaitwa *Local Government Capital Development Grant*, tunazizuia ili kupandisha hasira ya Madiwani, wakipata hasira pale maana yake ni kwamba watadhibiti pale. Kuna Halmashauri zingine zinanyimwa mpaka bilioni moja. Kwa mfano Halmashauri ya Manispaa Shinyanga ilinyimwa hela shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, nataka niliambie Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu huu wa kuzia hela ni kweli unamwumiza mwananchi lakini *at the end of the day* takwimu zime-*shift* kutoka 78 hivi leo tunazungumza Halmashauri nne, *we stand to be corrected here*, anaweza akaleta mawazo, lakini mimi nafikiri Mheshimiwa Diana Chilolo

tusaidiane wote kwa pamoja hela hizi ni za kwetu sisi wote Watanzania ni lazima tuwe na uchungu nazo. Hela zinavunwa watu wanafanya kama shamba la Bibi ndiyo maana tunafika mahali mnatuona tunakuwa wakali na sisi tumeamua kama TAMISEMI *we shall never leave any stone unturned*, tutakwenda katika Halmashauri tutafanya fujo za kila aina mpaka mtushike mkono mtuambie inatosha sasa.(*Makofî*)

SPIKA: Haya na mimi inatosha kwa swali hilo, sasa twende Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 28

Hajaji la Kurekebisha Sheria ya Usuluhishi

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Sheria ya usuluhishi (*Arbitration*) ni ya mwaka 1930 na kukua kwa uchumi hivi sasa kumesababisha migongano mingi ya kibiashara inayohitaji usuluhishi:-

Je, Serikali italeta lini Bungeni Muswada wa Sheria inayoendana na wakati?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usuluhishi (*Arbitration Act*), sura ya 15 Toleo la Sheria la mwaka 2002 ilitungwa mwaka 1931 kwa nia ya kuweka utaratibu wa kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Mbali ya Sheria hii kuna Sheria ya mwenendo wa madai, sura ya 33 ambayo nayo inaweka utaratibu wa kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi. Sheria zote hizi mbili zinatumwiwa katika kutatua migogoro hasa ya kibiashara. Yapo baadhi ya maeneo ya sheria hizo ambayo yanahitaji kurekebisha ili kuharakisha utoaji haki hasa kwa mashauri ya kibiashara.

Sheria hizi kwa ujumla wake zipo kwenye mchakato wa kufanyiwa marekebisho chini ya mradi wa mapitio ya Mfumo wa Haki katika Mashauri ya Madai (*Review of Civil Justice System*) ambao unafadhiliwa na mpango wa kuboresha mazingira ya biashara Tanzania (MKUMBITA) au Kingereza *BEST* na unatekelezwa kuititia Tume ya Kurekebisha Sheria katika Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huu ambao lengo lake ni kuharakisha mashauri na kupunguza msongomano wa kesi Mahakamani, kwa ujumla wake mpango huu unapitia sheria nane (8) tofauti zikiwemo Sheria ya Usuluhishi na Sheria wa Mwenendo wa Madai. (*Makofî*)

Sheria hizi zimeshapitiwa na zimeshapitiwa na Mtalaam Mshauri akishirikiana na Tume ya Kurekebisha Sheria na kwa sasa inaandaa taarifa ambayo itatoa mapendekezo na Rasimu ya Awali ya Marekebisho. Mchakato mzima ukishakamilika Muswada wa Marekebisho ya Sheria utawasilishwa katika Bunge lako Tukufu.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa (*National Construction Council*) Baraza la Ujenzi la Taifa nacho ni chombo cha usuluhishi hapa nchini kwetu.

Je, hayo marekebisho ambayo Mheshimiwa Waziri anasema wanafanya wametilia maanani kwamba chombo cha kwanza cha kupeleka usuluhishi kiwe kwenye *National Construction Council* badala ya kwenda kwenye chombo cha usuluhishi cha kimataifa kila wakati? (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba tumeshafanya mapitio, tumeshaongea na wadau mbalimbali na *draft* iko tayari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa kama atakuwa na la kuongeza sisi tutampa ile *draft* kama mdau ili aweze akatoa mapendekezo yake na nyongeza zake. (*Makofi*)

Na. 29

**Ukosefu wa Hakimu na Kuongezeka kwa Makosa ya Jinai
Tarafa za Kipeta na Mtowisa**

MHE. IGNAS A. MALOCHA aliuliza:-

Kuongezeka kwa makosa ya Jinai katika Tarafa za Kipeta na Mtowisa kutokana na wahalifu wa makosa ya jinai kuachiwa huru kwa sababu ya mashahidi kutokufika mahakamani kwani wamekuwa hawalipwi gharama zao kwa kukosekana kwa fedha za kugharamia mashahidi.

(a) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka kuongeza Bajeti ya Wizara ili kutatua matatizo kama hayo?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa Mahakama ya Mwanzo ya Kipeta kwa muda mrefu haina Hakimu na majengo yake yamechakaa sana na inachukua hatua gani kutatua matatizo hayo?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mbunge Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa sasa ni wakati muafaka kwa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kuongezwa ili pamoja na kutatua matatizo mengine ya fedha, fedha zitakazopatikana, zitumike kulipia mashahidi wakiwemo wale wa mashauri

yanayoendeshwa na Mahakama za Mwanzo. Aidha, Mheshimiwa Mbunge atakumbuka katika Mkutano wa Tatu wa Bunge lako Tukufu ilipitishwa Sheria ya uendeshaji wa Mahakama na kuanzisha Mfuko wa Mahakama ili Mahakama ziweze kupanga vipaumbele katika kutatua changamoto zinazowakabili ikiwa pamoja na hizi za kuwalipa mashahidi katika Mahakama za Mwanzo.

(b) Serikali inatambua kuwa Mahakama ya Mwanzo Kipeta haina Hakimu kwa muda mrefu kwa sababu Hakimu aliyeuwepo katika Mahakama hiyo hivi sasa yupo masomoni. Hata hivyo kutokana na uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, Mahakama ya Mwanzo Kipeta imekuwa ikitembelewa na Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa mara Mahakimu watakapoajiriwa Mahakama ya Mwanzo Kipeta itapatiwa hakimu.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Mahakama ya Mwanzo Kipeta yamechakaa sana na hayajafanyiwa ukarabati kwa muda mrefu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Wizara yangu ina mkakati maalum wa kuzifanyia ukarabati wa majengo yake yote ambayo yamechakaa awamu kwa awamu kutokana na kuanzishwa Mfuko wa Mahakama. (*Makofi*)

MHE. IGNAS A. MALOCHA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wazee wa Mahakama za Mwanzo ni muhimu sana katika kutoa ushauri mzuri kwa Mahakimu ili kufikia uamuzi ulio wa haki na kwa kuwa wazee hawa hulipwa shilingi 1500 mara baada ya kesi kumalizika tena kwa kuchelewa.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kiwango hicho ni kidogo mno kinaweza kufikia wazee hao kutoa ushauri mbaya kwa Mahakimu na hatimaye kwa kushawishiwa na rushwa akatoa uamuzi mbaya kwa kumshauri Hakimu kutoa uamuzi mbaya? (*Makofi*)

(b) Katika Kata ya Kaengesa na Kata ya Muze na Kata ya Ilemba ni Vituo vya Mahakama ya Mwanzo japokuwa vituo hivyo havina majengo wala watumishi, Serikali ina mpango gani wa kujenga majengo ya Mahakama na kupeleka watumishi?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza kuhusu Wazee wa Mahakama ni kweli Wazee wa Mahakama ni watu muhimu sana katika kutoa ushauri wa mashauri mbalimbali katika Mahakama kuanzia za Mwanzo mpaka Mahakama za Rufaa. Ni busara na ni vema wakalipwa kwa wakati ili haki itendeke kwa wakati. Serikali kwa kuliona hilo tayari imeshapandisha posho za Wazee wa Baraza kuanzia shilingi 1500 mpaka 5000 kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mfuko wa Mahakama mmeshatupitishia na kwa mwaka huu zimetengwa fedha kidogo kwa ajili ya kuanzisha Mfuko huo, nina uhakika kwamba tutajipangia vipaumbele hasa vile vya msingi ili tuweze kutatua kero mbalimbali katika sekta ya sheria.

La pili, kuhusu ujenzi wa mahakama katika Kata mbalimbali ni azma ya Serikali kwamba kila Tarafa na kila Kata iwe na Mahakama za Mwanzo. Tuna mpango wa muda mrefu wa kukarabati zile Mahakama ambazo zipo hasa Mahakama za Mwanzo na sasa hivi tuna mpango wa kujenga Mahakama mpya kwa sababu kama mnavyofahamu kwamba Mahakama nyingi za Mwanzo na za Wilaya zimejengwa kati ya mwaka elfu moja mia tisa kumi na mpaka mwaka 1950. Zimepitwa na wakati na sisi tunaliona kwamba ni jambo la kulizingatia hasa katika ujenzi wa Mahakama mpya. (*Makofi*)

MHE. DESDERIUS J. MIPATA: Mheshimiwa Spika, swali namba 29 linafanana na changamoto zilizopo katika Wilaya ya Nkasi. Wilaya ya Nkasi tangu kuanzishwa kwake mwaka 1979 haina jengo la Mahakama na pia Hakimu wa Wilaya jambo ambalo limesababisha Mahakimu kukosa *morale* ya kazi na kuchelewesha haki kwa wananchi amba wanakuwa na kesi zinazosikilizwa katika *level* hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani katika kuhakikisha kwamba changamoto hiyo inaondoshwa katika Wilaya ya Nkasi? (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Nkasi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mbunge, nakubaliana na wewe kabisa kwamba Wilaya ya Nkasi haina Mahakama. Kwa ujumla katika nchi nzima Wilaya 39 hazina Mahakama za Wilaya, wanatumia aidha majengo ya Halmashauri au majengo mengine.

Kwa hiyo, katika vipaumbele vyetu tumeliweka hilo la Wilaya ambazo hazina Mahakama kabisa zikiwemo Wilaya mpya pamoja na zile Wilaya za zamani ambazo hazina Mahakama kabisa.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hali ikituruhusu nina uhakika kwamba tutaanza na hizo Mahakama 39 ambazo hazina huduma kabisa ya Mahakama za Wilaya. (*Makofi*)

Na. 30

Matatizo ya Bodi za Mikopo ya Vyuo Vikuu

MHE. FELIX F. MKOSAMALI aliuliza:-

Mara kadhaa tumekuwa tunashuhudia migomo na maandamano ya wanafunzi katika Vyuo Vikuu nchini na malalamiko makubwa yakiwa juu ya Bodi ya Mikopo.

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani za haraka za kubadilisha mfumo wa mikopo kwa wanafunzi?
- (b) Je, ni nini sababu ya wanafunzi kutaka kuongezewa kiwango cha fedha ya kujikimu kutoka Shilingi 5,000/= hadi 10,000/= kwa siku?

- (c) Je, Serikali inachukua hatua gani za kinidhamu kwa wafanyakazi wanaochelewa kuingiza fedha za wanafunzi hao kwenya akaunti zao?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Mkosamali Mbunge wa Muhamwbe, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuboresha mfumo wa utoaji mikopo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, pamoja na utendaji wake. Tume maalum iliyoundwa na Mheshimiwa Rais kutazama na kutoa mapekezo juu ya kuboresha mfumo na taratibu za utoaji mikopo ikiwemo pia utendaji wa Bodi ya Mikopo imekamilisha kazi yake na kuwasilisha ripoti yake Serikalini. Kwa sasa Serikali inayafanya kazi mapendekezo yote yaliyotolewa ili kuainisha maeneo yanayohitaji kuridhiwa na Baraza la Mawaziri pamoja na yale ya kiutendaji.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za wanafunzi kuomba kuongezewa kiwango cha mikopo wa fedha za kujikimu kutoka Shilingi 5,000/= hadi 10,000/= kwa kila siku ni kwa sababu ya kupanda kwa gharama za maisha hususani bei vyakula na kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepokea ombi la wanafunzi na imelifanya kazi kwa lengo la kupandisha kiwango cha sasa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na hasa ikizingatiwa kwamba kiwango cha sasa kimekuwepo tangu mwaka 2007 bila kufanyiwa marekebisho.

(c) Mheshimiwa Spika, ucheleweshaji wa kuingiza fedha kwenye akaunti za wanafunzi unatokana na sababu mbalimbali zikiwemo mawasiliano hafifu kati ya Vyuo, Tume ya Vyuo Vikuu (*TCU*), Bodi ya Mikopo pamoja na mtiririko mzima wa fedha kutoka Hazina. Hata hivyo, Serikali inafuutilia kwa makini madai haya na kama ikitainika kwamba kuna ucheleweshaji wa makusudi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wahusika. Taasisi zote zinazohusika na uratibu wa fedha za Mikopo ya Wanafunzi zimeelekezwa kuwa na mawasiliano ya karibu ili kuondoa ucheleweshaji usio wa lazima. (*Makofî*)

SPIKA: Lakini unatakiwa u-delcare interest kwamba wewe ni mwanafunzi pia.

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Spika, ndio maana nimeuliza swali hili.

(a) Mheshimiwa Spika, tungependa kujua Wanafunzi wa Vyuo Vikuu kwamba ni kwa mwaka huu unaanza mwezi wa tisa wataanza kupokea shilingi 10,000 au lini fedha hizi zitaanza kutolewa?

(b) Kwa kuwa wanafunzi wa Chuo cha SAUT ambao wamekwenda *field* kutoka mwaka jana hawajapewa fedha zao na wengine chuo kizima wamemaliza kufanya *research* lakini hawajapewa fedha zao.

Pia Vyuo Vikuu vya Dodoma na Dar es Salaam wamemaliza na wanatakiwa wapewe fedha ya *field* mpaka leo hii hawajapewa wanataka kuingia barabara kufanya maandamano.

Je, haioni kwamba Serikali inasababisha vurugu zisizo na lazima inataka sisi vijana twende tuungane na wanafunzi wa Vyuo Vikuu kufanya maandamano huko mitaani? (*Makofi*)

SPIKA: Maandamano yasiingie katika eneo la Bunge ni *restricted area*. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbunge Felix Mkosamali, kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu kuongeza posho ya wanafunzi kutoka shilingi 5000 mpaka 10,000 kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi naomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote tusubiri siku ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi inaposomwa Serikali imesikia kilio hiki cha wanafunzi katika vyuo vyote tumedhamiria kuongeza lakini hapa siwezi kutaja kiasi ni shilingi ngapi tusubiri Bajeti, lakini tumeongeza. (*Makofi*)

(b) Kuhusu suala la *research* la Wanafunzi wa SAUT kama alivyosema kwamba wanafunzi hao wamemaliza lakini kama walikuwa na haki ya kupata fedha ya *research* na wamemaliza na Bodi ya mikopo iliridhia kwamba wangepata basi ni vizuri tukapata orodha hiyo na wana haki ya kulipwa.

Lakini hawa wanafunzi wengine katika vyuo vingine hasa Chuo cha Dodoma kama ulivyosema kuhusu *field*, Serikali imesikia ombi lao na nadhani siku mbili tatu hizi kulikuwa na purukushani kidogo ya wanafunzi wa kufanya mgomo juu ya hizo *field* lakini tumelishughulikia hizo program kama 13 ambazo ilikuwa wanafunzi wapewe fedha kwa ajili ya kufanya *field*, wanafunzi kama 1062 watalipwa posho za mafunzo kwa vitendo kwa gharama ya shilingi 389,000,088/=. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asubiri watalipwa. (*Makofi*)

Na. 31

Vifaa Mbalimbali vya Kuwasaidia Walemvu Katika Elimu

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR) aliuliza:-

wale mavu wanakabiliwa na uhaba wa vifaa mbalimbali vya kuwawezesha kujisomea,kama vile *Braille* kwa wasioona ,*Wheel Chair* kwa wale mavu wa viungo.

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutenga fungu la fedha kwa ajili ya kununulia vifaa hivyo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Al- Shaymaa John Kwegyir, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi fedha za kununulia vifaa vya kuwawezesha wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kujisomea hutengwa katika Bajeti ya Wizara kila mwaka. Hata hivyo, fedha inayotolewa haikidhi mahitaji yote yanayotakiwa. Kwa kuzingatia ufinyu wa Bajeti,Wizara yangu itaendelea kutekeleza mikakati ifuatayo:-

- (i) Kutoa ruzuku ya shilingi 20,000/= kwa kila mwanafunzi mwenye mahitaji maalum kupitia mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi awamu ya pili (MMEM II) kwa wanafunzi wa shule za msingi.
- (ii) Kutoa ruzuku ya shilingi 25,000/= kwa kila mwanafunzi mwenye mahitaji maalum kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMESII) kwa wanafunzi wa shule za sekondari.
- (iii) Lakini pia kutoa fedha za ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum katika Bajeti ya Serikali ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba fungu la ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi wenyewe mahitaji maalum linakidhi mahitaji, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi itaendelea kuwezesha upatikanaji wa vifaa na samani kwa ajili ya shule na vitengo maalum.

Baadhi ya asasi zinazoshirikiana na Wizara katika kutoa mchango wa fedha na vifaa ni Mamlaka ya Elimu Tanzania (*TEA*), *Dar es Salaam Mentally Handicapped Support Group, Tanzania Society for the Blind (TSB)*, Kampuni ya *TIGO,NMB,UNESCO* na *UNICEF*.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kabisa kuwashukuru wadau wote waliochangia na pia natoa wito kwa wadau wengine wa elimu kutoa michango ya fedha na vifaa ili kuwawezesha wanafunzi wenyewe mahitaji maalum kujisomea katika mazingira stahiki.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri na niipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua katika kuwasaidia walemaru. Lakini pamoja na majibu hayo mazuri nina swali moja.

Pamoja na mafungu haya ambayo yametolewa kwa shule za msingi na shule za sekondari katika kuwasaidia walemaru bado changamoto juu ya kuwasaidia walemaru bado ni kubwa. Walemaru wengi wanakosa haki maana yake elimu ni uwanja mpana.

Kwa mfano, Bunge linaonyeshwa *live* lakini hakuna mkalimali wa ishara anayeweza kusaidia wale ambao hawasikii ile lugha ya ishara, sijui inaitwaje lakini lugha ya alama.

Lakini pia taarifa za habari siku za nyuma kidogo kulikuwa kunaonyeshwa ile lugha ya alama.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kuweka watu hawa kwa sababu tunao watalaan hao ili waweze kufanya ukalimani huo na kuwasaidia walemaru waweze elimu hiyo? (*Makofî*)

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na mwenyewe mwenye swali kaja, kaingia atauliza swali moja tu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Simbachawene kama ifuatavyo:-

Nadhani kwanza ana *support* Serikali kwa mfumo mzima wa namna inavyosaidia hawa walemaru, lakini suala la mkalimali kwa hapa Bungeni na vilevile namna ya kutafsiri lugha yao hawa watu, mimi naomba nilichukue kama ushauri, Wizara ya Elimu itakaa na wataalam waweze kuona kama inafaa tutaendelea na zoezi hilo.

SPIKA: Mheshimiwa Al-Shymaa, huyu anasoma *Open University* ndiyo alianzia huko ndiyo maana amechelewa. Kwa hiyo, uliza swali la nyongeza moja sasa.

MHE. AL-SHAYMAA JOHN KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Samahani sana nilikuwa naudhuria mitihani, lakini naomba niulize swali moja. Nahema nilikuwa nakimbia. Swali moja la nyongeza. Kwa kuwa vifaa hivi vya visaidizi kwa watu wenye ulemavu ni vya gharama sana Serikali inaonaje kupunguza gharama za vifaa hivyo kwa sababu ni vya gharama mno kwa hiyo kodi yake itoke msamaha wa ushuru. Serikali inasemaje? (*Makofî*)

SPIKA: Waziri wa Fedha anaomba msamaha wa kodi kwenye vifaa visaidizi vya walemaru.

WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, tutaliangalia hilo, nataka nimhakikishie kwamba tutaliangalia kwa moyo wa huruma. (*Makofî*)

SPIKA: Waziri wa Kilimo, amesema wataliangalia lakini Waziri wa Kilimo naye kasimama.

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha kwa kujibu hili swali vizuri.

Vifaa hivi nya kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenyewe ulemavu havitozwi kodi kwa hiyo, sehemu ya gharama hizi ni ughali tu wa vifaa vyenyewe na kutohana na experience yangu kule Wizara ya Elimu, Serikali inafanya juhud kubwa sana kuhakikisha kwamba wanafunzi wenyewe ulemavu wanapata vifaa hivi na walimu wale ambao wanafundisha wanaongezeka ili kuhakikisha kwamba walemvu wanapata haki yao kama watoto ambao hawana ulemavu, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante, kwa hiyo, Serikali mkaagalie kinachoendelea huko kuhusu suala hilo. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Rajab Mbarouk atauliza swali.

Na.32

Bandari ya Musoma

MHE. RAJAB M. MOHAMED aliuliza:-

Bandari ya Musoma ni moja ya Bandari iliyokuwa inatoa mchango mkubwa katika pato la Taifa na mambo mengine kama ajira kwa vijana, kiungo na nchi jirani lakini hivi sasa hali ya Bandari hiyo ni mbaya kwa maana ya uchakavu wa vifaa, vitendea kazi, usalama wa abiria na ubovu wa miundombinu ya Bandari hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia matengenezo Bandari hiyo kwa kushughulikia kasoro zilizotajwa kwenye swali hili?

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa sasa miundombinu ya Bandari ya Musoma imechakaa. Bandari ya Musoma mpaka mwishoni mwa mwaka wa 1980 ilikuwa inatoa mchangano mkubwa katika uchumi wa Mkoa na pato la Taifa kwa kusafirisha abiria na mizigo kutoka ndani na nje ya nchi. Hali hii ilibadilika baada ya barabara ya lami kati ya Mwanza-Musoma kukamilika na hivyo kutoa ushindani mkubwa katika usafirishaji wa shehena na abiria. (*Makofii*)

Shehena iliyopita katika bandari kwa mfano, katika kipindi cha miaka minne iliyopita imekuwa ikipungua kwa wastani wa asilimia 17.4 kwa mwaka, kutoka tani 22,308 zilizohudumiwa mwaka 2007/2008 hadi tani 9,954 mwaka 2009/2010. Idadi ya meli katika kipindi hiki pia imepungua kutoka meli 58 hadi meli 28.

Bandari hii hivi sasa inajientesha kwa hasara na mapato yamepungua kutoka Bandari hii hivi sasa inajientesha kwa hasara na mapato yamepungua kutoka Tshs.54.74 milioni mwaka 2007/2008 hadi Tshs. 5.95 milioni mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa bandari ya Musoma, imepanga kufufua bandari hii sambamba na mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya Mwambani (Tanga), uboreshaji wa reli ya Tanga-Arusha na ujenzi wa reli mpya ya Arusha-Musoma. Mpango huu ni wa muda mrefu na lengo ni bandari hii iweze kuwa kuinganishi muhimu kati ya bandari mpya ya Mwambani Tanga na soko la Uganda. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali na Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu utawezesha Bandari kuhudumia asilimia kubwa ya soko la Uganda na nchi jirani za Rwanda, Burundi na Kusini mwa Sudan. Shehena kupitia bandari itaongezeka na hivyo kuchangia katika pato la Taifa na maendeleo ya Musoma ikiwa ni pamoja na ajira kwa vijana. Aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (*TPA*) imeanza maandalizi ya mradi huu ambapo hekta 30 zimeombwa kutoka Halmashauri ya Mji wa Musoma kwa ajili ya upanuzi wa Bandari. (*Makofii*)

MHE. RAJAB M. MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante. pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, sijui Mheshimiwa Waziri atawahakikishiaje wananchi wa Musoma hasa wale ambao wanapata riziki yao kutoka Bandari hii, kwamba lini Bandari hii itaanza kufanyiwa matengenezo kwa sababu kusema kwamba itaenda sambamba na ujenzi wa Bandari wa Tanga huo ni mradi mpya hiki kitu kipo na watu wanategemea riziki yao kutoka pale. Sijui Waziri atawaambia nini wananchi wa Musoma.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohamed, Mbunge wa Ole, kama ifuatavyo:-

Tayari TPA imeshateua mshauri, *consultant* na shughuli hiyo imekwishaanza hivyo wananchi wa Musoma wawe na uhakika baada ya upembuzi yakinifu shughuli zitaanza mara moja katika utekelezaji wa mradi huu.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa matatizo ya Bandari ya Musoma yanaonekana katika bandari mbalimbali ikiwemo bandari ya Kigoma pamoja na maeneo mengine na kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge tumeonekana kuweza kulalamikia kwamba tunapata posho nyingi, ni kwa nini Wizara ya Uchukuzi isishirikiane na Wizara ya Fedha na Uchumi kuweza kuridhia maombi yetu Kambi ya Upinzani kuhakikisha kwamba posho zetu za *sitting allowance* zinakatwa ili kwenda kusaidia kuboresha miundombinu ya bandari ili kuhakikisha kwamba sekta ya bandari inaweza kuimarika nchini? (*Makofî*)

SPIKA: Posho haijaingia rasmi, naomba ujibu habari ya hiyo ya Bandari tu, sio habari ya posho ya Mbunge kutengeneza Bandari. Mheshimiwa Naibu waziri au nani anataka kujibu? Jibu kuhusu Bandari.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba nijibu sehemu ya swali la Mheshimiwa Machali kwa Bandari ya Kigoma kama ifuatavyo:-

Utaratibu sasa hivi unafanyika ili tuweze kuboresha Bandari ya Kigoma na hasa tungewaomba Waheshimiwa wanaotoka Mkoa ule tusaidiane nao katika kuhamisha watu ambao wamejenga milimani pale na bandari ya Kigoma inaendelea kupata mchanga ili kina kiongezeke na meli nyingi ziweze kutoa huduma pale.

MHE. VINCENT J. NYERERE: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa majibu ya Waziri yanasema ni mpango wa pamoja na Serikali ya Uganda, lakini Bandari hii ni ya Tanzania na ni ya watu wa Musoma. Waziri haoni kwamba kusubiri Serikali ya Uganda itusaidie kuamua itachelewesa ujenzi wa Bandari hii mapema na kwa kuwa Bandari hii ni ya kwetu sisi Watanzania. Waziri haoni kwamba Serikali ya Tanzania inashindwa kuamua mambo yake yenewe mpaka isubiri Serikali ya nchi nyingine? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Bandari ya Musoma ni Bandari ya Tanzania, reli ambayo tunakusudia kujenga toka Musoma hadi Arusha na kuboresha ile iliyopo hadi

Tanga ni ya Tanzania na Bandari ya Mwambani ni ya Tanzania. Hivi ni vyombo ambavyo ni jukumu letu sisi wenyewe kuvijenga.

Lakini katika mfumo wa kutenda kazi na pia kuhakikisha kuwa tunapovijenga vyombo hivi ambavyo ni vya gharama kubwa sana vitarudisha pesa ambazo tumevijengea ndiyo hapo tukawa tunashirikiana na wenzetu wa Uganda ambao ndiyo wana mzigo mkubwa ambao ndiyo utapita katika vyombo hivi.

Katika kutafuta wawekezaji, sisi tunakwenda kama Watanzania, tunakaa na wenzetu wale ili wao nao kwa mahitaji yao zile nguvu ziwe ni kubwa ili tuweze kupata wawekezaji. Nataka kumhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kuwa hizi ni mali zetu na zitabaki kuwa mali zetu, ahsante sana. (*Makofi*)

Na. 33

Sera ya Umri wa Kustaafu kwa Wanajeshi

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA aliuliza:-

Serikali hutumia fedha nyingi kwa ajili ya mafunzo mbalimbali kwa wanajeshi na kwamba Sera ya Jeshi kuhusu umri wa kustaafu haiendi sambamba na ile ya watumishi wa Umma:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa wanajeshi waliopata mafunzo na wataalam mbalimbali kama vile udaktari na uhandisi wanalaazimika kustaafu mapema na taaluma yao kupotea?

(b) Je, ni wataalam wangapi wanajeshi wa JWTZ na JKT ambao wamestaafu kati ya mwaka 2005-2010 ambao walikuwa chini ya umri wa miaka 60?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni kweli huwafunza wanajeshi wake katika taaluma mbalimbali kwa gharama kubwa. Kwa kuzingatia hilo na mambo mengine kama umri wa kustaafu wanajeshi ulirekebishwa kuanzia tarehe 1 Julai, 2009. Kutokana na marekebisho hayo umri wa kustaafu kwa lazima hivi sasa ni kati ya miaka 50 na 62 kulingana na mpangilio wa vyeo vya kijeshi na taaluma. Kabla ya hapo umri wa kustaafu ulikuwa ni kati ya miaka 47 na 57. Baada ya maelezo haya ya awali sasa kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester Maselle Mabumba wa Dole lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, marekebisho ya umri wa kustaafu yaliyofanyika yamelenga kuwatumia kwa muda mrefu zaidi wanajeshi wenyewe taaluma mbalimbali. Kwa upande wa madaktari wa binadamu sasa wanastaafu wakiwa na umri wa miaka 62. Aidha, kwa wale wanaostaafu na bado wanaonekana kuwa na nguvu na uwezo wa kufanya kazi huitwa

kufanya kazi inayoendelea kwa mkataba maalum kwa mujibu wa kifungu cha 42 (2)(b) cha sheria ya Ulinzi wa Taifa (*National Defence Act*).

(b) Mheshimiwa Spika, wanajeshi wataalam waliostaafu kati ya mwaka 2005-2010 ambao walikuwa chini ya miaka 60 ni 384. Baadhi yao wameitwa kuendelea na kazi kwa mkataba. Aidha, Jeshi la Ulinzi linaajiri kila mwaka kuziba mapengo yanayoachwa wazi kutokana na kustaafu, vifo na sababu nyininge. (*Makofi*)

MHE. SYLVESTER M. MABUMBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza maswali mawili madogo ya nyogeza. Naipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini naomba niulize:-

(a) Kwa wale wanajeshi wataalam ambao hawakubahatika kuitwa ili wapate mkataba wa kuendee na taaluma zao kutoa huduma zao katika Taifa letu, Serikali ina mpango gani ili kuwatumia ili kuendeleza Taifa letu?

(c) Kwa vile wanajeshi wetu wamejitlea sana kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu, kwa wale wanajeshi wengi ambao wamestaafu na tunajua hali zao siyo nzuri sana. Serikali ina mpango gani kuanzisha mfuko maalum kwa ajili ya kuwaendeleza ili waishi kwa matumaini na kuendelea kuwa waaminifu kwa nchi yetu?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyogeza ya Mheshimiwa Mabumba kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni kwamba baadhi yao tunawatumia kwa mkataba, lakini si rahisi kuwatumia wote kwa sababu nafasi zilizopo hazitoshelezi. Hata hivyo wanajeshi hawa ambao wana taaluma wanaweza kuingia katika utumishi wa Umma, kama mtu ni *engineer* au ni dakitari bado ana nafasi ya kufanya kazi katika utumishi wa Umma au katika hospitali za binafsi kwa maana ya sekta binafsi.

Pili kuhusu mfuko maalum. Tatizo hapa ni la kibajeti tu tunaelewa matatizo yanayowakabili wataalam hawa, lakini kama ilivyo kwa pensheni kwamba hatujawezwa kuiongeza kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ni kwa sababu ya ufinyu wa Bajeti. Kwa maana hiyo, mfuko maalum vilevile utakabiliwa na matatizo hayo hayo ya kibajeti, lakini tunachoweza kusema ni kwamba wataalamu hawa pengine wangejingga katika kikundi maalum kungekuwa na wepesi wa kuwatafutia njia za kuwasaidia.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza awali tunazo kambi saba za jeshi kwa hiyo matatizo ya majeshi tunayaelewa sana, lakini moja tu ni Waziri anafahamu kwamba wale wanajeshi amba ni wataalam, lakini kwa bahati mbaya katika utaalam wao wamepata ajali wakaumia, hawapati hudumua zinazostahiki, una habari hiyo? Na kama unayo unachukua hatua gani?

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamda Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Zipo taratibu za kisheria za kuwahudumia wanajeshi waliopata maafa mbalimbali wakati wa utumishi wao. Pamoja na pensheni ya kawaida wanayoipata wanajeshi hao, kuna fedha au malipo ya ulemavu kwa kiwango cha mtu alichoumia. Kwa maana hiyo hoja iliyopo mbele yetu sasa hivi ni kwamba pengine malipo yale au posho ile ya ulemavu bado ni ndogo haikidhi haja kutokana na ufinyu wa Bajeti. Lakini utaratibu upo mtu ambaye anapata ulemavu akiwa kazini anafanyiwa *medical board* ambayo inatoa kiwango cha asilimia aliyopata ulemavu na hupata malipo kutokana na ulemavu aliokuwa nao.

Na. 34

Kilimo cha Umwagiliaji kwa Kutumia mto Chala

MHE. JOSEPH R. SELASINI aliuliza:-

Wilaya ya Rombo inakabiliwa na ukame hasa kwenye maeneo tambarare ya vijiji vya Malowa (Mamsera Chini), Ngoyoni, Ngareni, Ikuini, Muunga, Mahorosha na Msaranga ambao umesababisha ongezeko kubwa la njaa na umaskini kwa wananchi wa maeneo hayo:-

- (a) Serikali haioni haja ya kuanzisha Kilimo cha Umwagiliaji kwa kutumia maji ya mto Chala?
- (b) Je, kuna sababu zozote za kisayansi zinazozuaia maji hayo yasitumike?
- (c) Je, kwa nini Serikali isijenge miundombinu ili maji hayo yaweze kutumika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mbunge wa Rombo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Rombo hususan katika maeneo ya tambarare hayakubahatika kuwa na vyanzo vya maji vinavyoweza kutumika sana kwa kilimo cha umwagiliaji. Hata hivyo, liko Ziwa Chala katika mpaka wa Tanzania na Kenya ambalo ni maji shirikishi (*transboundary water*) ya nchi hizo mbili ambalo linafanyiwa uchunguzi ili maji yake yatumike.

(b) Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo katika kutumia maji shirikishi ya Ziwa Chala ni ukosefu wa takwimu za kihaidrolojia na kihaidojiolojia zinazowezesha wataalam kupanga mipango endelevu ya matumizi ya ziwa hilo.

Kwa kutambua tatizo hili, Serikali ya Tanzania inashirikiana na Serikali ya Kenya kufanya utafiti wa uwingi na ubora wa maji ili rasilimali maji ya Ziwa Chala iweze kuwanufaisha wananchi wa pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi unaofanywa unahusisha pia maji shiriishi yam to Umba na Ziwa Jipe ambalo linakabiliwa na uharibufu unaotokana na magugumaji.

Serikali za Tanzania na Kenya zinaendelea kufanya mazungumzo yanayojenga kuunda chombo cha pamoja cha usimamizi na kuendeleza rasilimali za maji shirikishi za Ziwa Chala, Ziwa Jipe na Mto Umba. Namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Rombo kuwa na subira wakati Serikali inatafuta ufumbuzi wa matumizi endelevu ya ziwa Chala.

(c) Mheshimiwa Spika, kukabiliana na ukame unaojitokeza mara kwa mara Wilayani Rombo, Serikali inendelea kuboresha mfereji wa Ikwini amba o una uwezo wa kumwagilia hekti 160 za mazao mchanganyiko. Aidha kuitia programu ya kuendeleza sekta ya maji Serikali inafanya utafiti wa kuchimba visima virefu ambavyo vitapunguza tatizo la upatikanaji wa maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna watu wanaojiita wawekezaji amba o wanayatumia maji ya Ziwa Chala bila kujali uchunguzi wa kitakwimu amba o Mheshimiwa Waziri ameueleza na wawekezaji hao wamekuwa wakiwauzia wananchi kutumia maji hayo pamoja na ardhii inayozunguka Ziwa Chala na wamewaweka walini wa jadi amba o wanawapiga wananchi hususan akina mama wanaokwenda kukata majani na kujiokotea kuni kwenye mazingira yanayozunguka Ziwa hilo. Je, Serikali iko tayari kuchunguza jambo hilo na ikiwezekana kuwaruhusu wananchi kutumia maji hayo katika shughuli za kilimo, kilimo kama cha mboga na matunda kama wenzetu wa Kenya wanavyofanya?

Pili, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ameeleza matumizi ya Bwawa la Ikwini kwamba yatawanufaisha wananchi kwa kiasi fulani. Ni sawa, lakini Wilaya ya Rombo ni Wilaya ambayo ina mito mingi ya msimu.

Hivi sasa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo imeleta maombi Wizarani, ili kuweza kupatiwa fedha za kujenga malambo katika mito ya misimu kule Rombo ili kuwasaidia wananchi wakatio wa kiangazi kwa ajili ya umwagiliaji.

Je, Waziri yuko tayari kuwaahidi wananchi wa Rombo katika Bajeti hii kwamba atawasaidia kutenga fedha ili malambo hayo yaweze kutengenezwa?

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu wawekezaji, ninayo taarifa kwamba kuna wawekezaji kwenye sekta ya mahotel. Moja ya Tanzania, moja ya Kenya ambao wanatumia maji haya. Lakini maji kwa matumizi ya nyumbani yanayotumika ni kidogo sana ukilinganisha na maji ya kilimo cha umwagiliaji.

Lakini kuhusu hawa ambao tayari anawaita wawekezaji kwamba wanatumia maji haya. Mimi nataka niseme mimi sina taarifa hizo. Lakini kama wapo watu ambao wanatumia maji shirikishi bila kufuata utaratibu, maji yote shirikishi kwa kawaida lazima nchi zinazohusika zikae pamoja tupange mipango ya pamoja ya kuyatumia.

Waziri wa Maji amesikia, naye yuko hapa. Mimi naomba nimhakikishie kwamba tutachunguza kama wapo watu tayari wanatumia Ziwa hili kinyume na taratibu, basi tutawasiliana na Serikali ya Kenya. Lakini pia kama kuna watu wananyanyasika vile vile Waziri wa Mambo ya Ndani yuko hapa amelisikia, yote haya tutayachunguza na tuchukue hatua zinazostahili.

Kuhusu kuendeleza mabonde haya ya mito ya misimu, hili nimelipokea Mheshimiwa Spika, utarataratibu wetu ni kwamba Halmashauri inatakiwa ilipitishe katika Mipango ya Maendeleo ya Wilaya yaani *DADIPs* kusudi tuanzie hapo sasa ili tuweze kuangalia namna ya kutekeleza miradi hii. Lakini kimsingi maombi yake yanakubalika.

SPIKA: Tunaendelea na swali linalofuata, zingatieni muda. Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, swali linalofuata.

Na. 35

Mabenki kukopesha wakulima kwa ajili ya ununuzi wa matrekta

MHE. PINDI H. CHANA aliuliza:-

Wakulima wengi wanetamani kutumia matrekta katika kilimo hususan wakati huu wa mpango wa kilimo kwanza, na jeshi la kujenga Taifa wanaauza matrekta ambayo yanafaa sana kwa kilimo:-

- (a) Je, Serikali imeweka mpango gani wa kuhakikisha kuwa wakulima hususan wa Ludewa, Njombe na Makete wanakopeshwa fedha na mabenki ili kuweza kununua matrekta hayo?
- (b) Je, riba za mikopo hiyo ya mabenki ni kiasi gani?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mikopo kwa ajili ya kununua matrekta na zana zake inatolewa na mabenki mbalimbali kama *NBC, CRDB, NMB, FBME* na kadhalika.

Pia zipo taasisi nyingine za kifedha kama vile *Private Agricultural Sector Support (PASS), Sero Leasing and Finance Ltd. (SELFINA)* na kadhalika ambazo zinatoa mikopo kwa ajili ya miradi ya kilimo ikiwemo ya zana za kilimo.

Masharti ya mikopo kutoka katika mabenki yanatofautiana na mengi ya mabenki hayo hayatoi mikopo ya muda mrefu hivyo kuwafanya wakulima wengi kushindwa kumudu masharti ya kupata mikopo hiyo. Riba inayotozwa na mabenki hayo ni kati ya asilimia 15 hadi 20 na muda wa marejesho ya mikopo hiyo ni kati ya miaka miwili hadi mitatu (2 - 3). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika juhudı za kuwasaidia wakulima, Serikali imefungua Dirisha Dogo la Kilimo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) ili kutoa mikopo kwa ajili ya miradi ya kilimo, zana bora za kilimo, kugharamia uzalishaji na usindikaji wa mazao na mauzo. Mikopo ya kati ya shilingi milioni 50 na bilioni moja inatolewa kwa makundi ya wakulima kwa riba ya asilimia tano kwa mwaka.

Taasisi zinazokopa kwa ajili ya kukopesha (*on-leanders*) zinatozwa riba ya asilimia nne kwa mwaka ambapo zinatakiwa kukopesha kwa asilimia isiyozidi nane kwa wakulima/wateja wao. Muda wa marejesho ya mkopo ni miezi 6 hadi miaka 15. Hadi tarehe 3 Juni, 2011 *TIB* walikuwa wametoa mikopo ya matrekta makubwa 100 na matrekta madogo ya mkono 82 kwa *SACCOS* mbalimbali katika mikoa ya Singida, Morogoro, Mwanza, Ruvuma, Iringa, Kagera, Mtwara, Dodoma, Pwani na Tanga.

Ili kusogeza huduma kwa wateja, *TIB* imefungua ofisi za Kanda katika Mikoa ya Arusha na Mwanza na wanatarajia kufungua Ofisi zingine huko Mbeya, Dodoma na Zanzibar kwa lengo la kuwafikia wakulima karibu zaidi. Hivyo wakulima wa Ludewa na huko Njombe na Makete watanufaika na utaratibu huo. Aidha, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo unatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kununua na kusambaza pembejeo, zana bora za kilimo, na nyenzo za umwagiliaji. Muda wa marejesho ya mikopo ya matrekta ni miaka saba na matrekta madogo ya mkono ni miaka mitatu. Riba ya mikopo hiyo ni asilimia sita kwa mwaka kwa vikundi vyta uzalishaji na asilimia saba kwa mwaka kwa watu binafsi. Wilaya ya Njombe imepata mikopo ya matrekta makubwa manne na madogo ya mkono, mawili kati ya mwaka 2007/2008 - na mwaka 2010/2011 kupitia Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia fursa hizi, wakulima wanaokidhi masharti ya mikopo kote nchini wanashauriwa kuwasiliana na asasi hizo ili waweze kuomba mikopo kwa ajili ya kununua zana bora na kuzitumia kwa ajili ya kuboresha kilimo chao. (*Makofi*)

MHE. PINDI H. CHANA: Ahsante Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, na jitihada ya Benki ya *TIB* bado takwimu zinaonyesha kwamba ni wakulima wachache sana ambao wamepata fursa hasa ukizingatia Tanzania tuna idadi ya watu zaidi milioni 40 ambapo kati ya watu zaidi milioni 40, asilimia 50 ya milioni 40 ni wakulima kutokana na riba kubwa zamana ambapo mabenki haya yanahitaji. Wizara na Serikali itakubaliana na ushauri wangu kama ifuatavyo:-

Waziri wa Chakula, Kilimo na Ushirika awasiliane na Waziri wa TAMISEMI waweze kutoa maagizo kwa Halmashauri zote nchini waweze kutumia matrekta kwa sababu bado wakulima wanatumia jembe la mkono ili matrekta yale yaweze kukodishwa kama jinsi ambavyo Halmashauri zinanunua vyombo vingine kama magari, *Land Cruiser* na kadhalika? (*Makofi*)

SPIKA: Haya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi, lilikuwa ni refu hata kama ni kilimo kwanza.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kweli wakulima wanaopata mikopo bado si wengi.

Lakini tunaendelea kutoa mikopo jinsi fedha zinavyopatikana na hata kilimo chenyewe kimepanda, labda nitoe tu takwimu tu kwamba wakulima waliokuwa wanatumia jembe la mkono, wametoka asilimia 70 wameshuka mpaka asilimia 64 na wakulima waliokuwa wanatumia wanyama kazi wamepanda kutoka asilimia 20 mpaka 22 na matrekta hivi sasa yametoka asilimia 10 mpaka 14. Maana sasa hivi yanaonekana hata hapo njiani ukienda Dar es Saalam unaona yamepangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuanzisha hivi vikundi vya matrekta, ni sera, ni utaratibu wetu kwamba tunawataka wakulima na vikundi, vijiunge kusudi viweze kutumia matrekta haya, *Service Centers*. Maana haitawezekana kila mkulima akope trekta. Kwa hiyo nakubaliana naye kabisa ushauri wake ni nzuri na ndiyo utaratibu ambao tunaufuata. (*Makofi*)

Na. 36

Ujenzi wa Daraja la Kudumu la Gulwe – Kibakwe

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE aliuliza:-

Daraja la Gulwe ambalo linaunganisha jimbo la Kibakwe na Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapwa, limetengenezwa kwa dharura mwaka 2009/2010 lakini limebomoka tena kutokana na mvua za mwanzo tu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga daraja la kudumu ambalo litahimili kiwango kikubwa cha maji yanayopata katika mto Kinyasungwi?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa George Biniface Simbachawene, Mbunge wa Jimbo la Kibakwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga daraja la kudumu ambalo litahimili kiwango kikubwa cha maji yanayopita katika mto Kinyasugwi. Kazi ya usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni unaendelea na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011. Inatarajiwa kwamba ujenzi wa daraja la kudumu utanza katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 endapo hali ya fedha itaruhusu.

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri na mafupi ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini hii kauli ya hii *statement* ya mwisho kwamba endapo hali ya fedha itaruhusu, inanifanya ninyong'onyee kabisa.

Mheshimiwa Spika, tofauti inayojitokeza baada ya lile daraja kuwa limekatika na kwamba magari hayaruhusiwi kupita ya karibu kilomita 40 hali ambayo imeongeza gharama ya maisha sana kwa watu wa Kibakwe. Njia pekee ya kupita ni hiyo tu ukiondoa hiyo Msagali inayotumika kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba kusema endapo hali itaruhusu na wakati watu wanaumia sana kwa sababu gharama ya maisha imeongezeka ni jambo ambalo kwa kweli linahitaji uwe na moyo mgumu kidogo kwa sababu sijui nitarudije kule, maana yake tulikuwa tunafahamu kabisa kwamba angalau kuna fedha hata zilizotengwa *almost 1.4* bilioni sasa sijui hali hii inakuwaje mpaka kauli hii itolewe kwamba endapo hali ya fedha itaruhusu?

Swali la pili, kwamba lile daraja kilichotokea ni kwamba ile *base* yake ime-sink tu chini na kwamba magari kwa sasa ambapo maji sasa hayapiti yamekwisha, magari yanaweza yakapita. Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari tuende wote tukaangalie lile daraja tukiwa na Wataalam ili tushauriane tuone kama je linaweza likatumika *temporarily* wakati tunangojea mpango wa kujenga daraja la kudumu?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ningemwomba Mheshimiwa Mbunge asinyong'onyee, awe na imani na Serikali yake ambayo toka mwanzo daraja lao lilipovunjika mwaka 2009 Serikali imeonyesha kwa kweli kuwajali sana wananchi jumboni Kibakwe. Kwanza kwa kuanzisha mchakato kwa kushirikiana na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kushirikiana na Wakala wa Barabara na kuweka pale daraja la chuma lililogharimu shilingi milioni 247 katika kipindii cha miezi mitatu tu.

Hilo daraja limeondoka juzi tu mwezi Desemba kutokana na kasi ya maji katika huo mto. Ningependa nimhakikishie Mheshimiwa Simbachawene kwamba Serikali sasa hivi ina mpango wa kujenga daraja la kudumu.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tuna mpango wa kulikarabati hata hili daraja wakati tunasubiri fedha ije. Tumetenga shilingi milioni 51.86 kwa ajili ya ukarabati wa hiyo nguzo iliyobomoka. Kwa hiyo, wananchi wa Kibakwe wawe na imani tu kwamba watapita. Tulichofanya ni kusitisha tu magari ya mizigo, magari ya abiria yasipite kwa ajili ya usalama wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwisho mimi kwenda naye Mheshimiwa Simbachawene sina matatizo, hapa ni karibu. Lakini la msingi tu ni kwamba tunasubiri maji yapungue kwenye huo mto, tuanze ukarabati wa hiyo nguzo, tukisubiri sasa ujenzi wa daraja hilo la kudumu.

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yameisha na muda umeisha sana. Sasa nina matangazo machache. Kwanza ninao wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Wapo Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Hawa sisi ndiyo jimbo lao.

Kwa hiyo, wamekuwepo hapa toka wakati wa Bajeti mpaka wakati wa Mipango. Nao ni wafuataao:-

Mheshimiwa Janeth Mmari, Mheshimiwa Dkt. Amani Kaburu na Mheshimiwa Abdallah Mwinyi. Hawa watatu tumekuwa nao toka mwanzo tunaanza kikao hiki na watapenda kuwa na sisi katika muda huu wote. Tuna wageni wengine 60 ni wachezaji wa mpira wa miguu wakiongozwa na Katibu wa TFF Wilaya ya Bunda. Wako wapi hao? Wachezaji 60 wa kutoka Wilaya ya Bunda. Ooh! Karibuni sana, mmetoka mbali, Bunda tunawatakia kheri katika mambo mnayoyafanya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 110 wa *Internal Ruminant Academy* kutoka Dar es Salaam na walimu wao 10. Naomba wasimame hapo, *okay!* Ahsante sana wanafunzi, karibuni sana na musome kwa bidii na nidhamu ya kutosha. Ahsante walimu kwa kuleta watoto. Halafu wako wengi, wengine wataingia kipindi cha jioni. Tuna wanawake 31 wa KKKT Dodoma, wenyewe wako wapi, labda wataingia jioni. Ahaaa wapo, *okay!* Haya karibuni sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Tuna wanafunzi 40 kutoka Shule ya Msingi Kibaha pamoja na walimu wao wanne, wanafunzi wa Kibaha wako wapi? Nadhani ni wale ambao watapata nafasi mchana. Kwa sababu tayari *Gallery* zimejaa. Basi karibuni na wageni wengine wote mnakaribishwa.

Shughuli za kazi tunaye Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana. Anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya

Katiba, Sheria na Utawala kuwa leo tarehe 13 kuanzia saa 7 mchana kutakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 231 saa saba (7) mchana.

Halafu nina tangazo lingine, hapa Washabiki wa Simba wanajipongeza hapa, wanasema kwamba kwa heshima kubwa naomba uliambie Bunge hili kumpongeza Mheshimiwa Aden Rage, Mwenyekiti wa Simba na Timu nzima ya Simba kwa kuifunga Motema Pembe. Kwa hiyo, kuendeleza kulinda heshima ya nchi kama ilivyo kawaida ya *Simba Sports Club* na mwenyewe Rage amevaa Simba leo. Basi nawapongeza kwa hilo. (*Makofi*)

Lakini nina taarifa nyingine ambayo ni taarifa ya msiba. Mwenzetu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, amefiwa na mtoto wake na wamemzika jana. Kwa hiyo, kama ulivyo utaratibu wetu tutafanya yanayohusika. Ahsanteni sana. Haya tunaendelea jamani. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1) mpaka cha (iii) za Kanuni ya Kudumu, Toleo la mwaka 2007. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kutengua Kanuni ya 64 ya Kanuni za Bunge, Toleo 2007 ili kuweza Bunge lako Tukufu likae kama Kamati ya Mipango katika Mkutano huu wa Bunge la Bajeti ili lijadili na kuidhinisha Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka mitano, Mwaka 2011/2012 mpaka mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, shughuli hii ya kujadili Mpango ulipshwa kutekelezwa katika Mkutano wa Pili wa Bunge mwezi Februari mwaka huu. Kwa kuwa katika kipindi hicho kazi ya utayarishaji wa Mpango huo ilikuwa haijakamilika na Serikali ilitoa taarifa na sasa imekamilisha na kuletwa katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Kanuni za Bunge zilitenguliwa ili Bunge likae kama Kamati ya Mipango na Kujadili Mipango ya Miaka Mitano*)

**Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano,
2011/2012 – 2015/2016**

WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977, Toleo la mwaka 2008, Ibara ya 63 (3) (c), inatuelekeza ifuatavyo: Nanukuu, “*Kwa mahumuni ya utekelezaji wa madaraka yake, Bunge linaweza kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi, unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza matakwa hayo ya Katiba, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Miaka mitano, yaani 2011/2012 na 2015/2016 kama ifuatavyo:-

(a) Bunge lako Tukufu liridhie Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 na Utekelezaji wake.

(b) Bunge lako Tukufu liridhie Mapendekezo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, uwe ni kipindi cha mpito katika utekelezaji wa mpango huu, ili kutoa fursa kwa mpango kuanza kutekelezwa kikamilifu kuanzia mwaka wa fedha 2012/2013.

(c) Bunge liridhie vipaumbele vyta ya mpango na mapendekezo ya raslimali zinazohitajika kwa utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu tangu kumalizika kwa uchaguzi Mkuu, napenda nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwatachia heri wananchi wa Tanzania wakati huu ambapo wanajiandaa kuadhimisha miaka 50 ya uhuru wetu.

Nawapongeza hasa kwa kuendelea kuenzi amani na umoja, uvumilivu na kustahimiliana pale palipokuwa na mitazamo tofauti. Hali hii imeifanya nchi yetu kuwa na sifa ya pekee Barani Afrika. Ninawasihi na kuwaomba Watanzania wenzangu tuendelee kuilinda sifa hii mwanana.

Mheshimiwa Spika, napenda kukumbusha kuwa mwaka jana tulifanya Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu. Ni jambo kubwa la kumshukuru Mungu, hivyo naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kwa kipindi kingine cha miaka mitano kuliongoza Taifa letu katika nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namwombea Mwenyezi Mungu amjalie afya njema, hekima na ujasiri zaidi katika kuiongoza nchi yetu. Napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mohamed Gharib Bilal kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Namtakia kila la heri katika kazi yake ya kumsaidia Rais katika majukumu ya kuliongoza Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, kwa kuteuliwa kwa mara ya pili na Rais, kuwa Waziri Mkuu na kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika Mwanamke wa kwanza katika historia ya nchi yetu. Ni imani ya Watanzania kwamba utaliongoza Bunge hili la Kumi kutimiza wajibu wake. Hususan katika kulisogezza mbele kimaendeleo Taifa letu kupitia mpango ninaouwasilisha hapa. Ninapongeza pia Mheshimiwa Job Ndugai kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Nawapongeza pia Wenyeviti watatu waliochaguliwa kukusaidia katika kuongoza Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uchaguzi wa mwaka 2010 ni zoezi ambalo halikuwa rahisi, hivyo niruhusu niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi walioupatu katika uchaguzi huo. Aidha, ninawashukuru sana wananchi wa Bunda kwa imani yao kwangu kwa kunichagua kwa mara nyingine tena kuwa Mbunge wao na kwa imani ya Rais, kunitfea kuendelea kutumika katika Serikali yake. Vile vile Nawapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, kuongoza Wizara zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kubaini haja ya Taifa letu kurejea utaratibu mzuri wa kuwa na Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano. Mpango huu wa Maendeleo wa miaka mitano ni sehemu ya utekelezaji wa mpango elekezi katika kufikia malengo ya dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 katika kipindi cha miaka 15 iliyobaki ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano umehusisha watu na makundi mbalimbali. Kwa namna ya pekee napenda kutambua na kupongeza mchango wa viongozi na wafanyakazi wa Ofisi ya Rais Tume ya Mipango, chini ya uongozi wa Katibu Mtendaji Dr. Philip Mpango na Naibu Makatibu Watendaji kwa kusimamia vizuri maandalizi ya mpango huu. Maandalizi haya yamefanyika kwa kipindi kifupi sana ikilinganishwa na muda unaotumiwa na nchi nyingine. Wakati sisi tumetumia muda wa takribani miezi sita, uzoefu wa nchi nyingi ni kuwa maandalizi ya muda wa kati wa maendeleo huchukua sio chini ya miezi 18. Ni wazi kuwa Watendaji wa Tume ya Mipango, wamejituma kwa bidii na kwa kutumia watalaamu wa ndani ya nchi yetu kutimiza jukumu hili kubwa.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchache wa fadhila kama sitatambua na kushukuru kwa dhati Mpango wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, chini ya uongozi shupavu wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kujadili na kutupatia ushauri pamoja na changamoto za kuzingatiwa katika kuboresha mpango na mkakati wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mantiki ya kurejea mpango wa muda mrefu na kati, upo usemi kuwa “*Kushindwa kupanga ni kupanga kushindwa.*” Viongozi waasisi wa Taifa letu, chini ya uongozi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, walilielewa hilo na kuzingatia mantiki ya usemi huo kwa vitendo. Mara tu baada ya uhuru tulikuwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitatu (1961 - 1964) ambao shabaha yake kuu ilikuwa ni kuelekeza juhudzi za jamii na Taifa katika kupambana na umasikini, ujinga na maradhi.

Mwaka 1964, Serikali iliona umuhimu wa kuwa na mpango wa upeo mrefu zaidi ili kuelekeza mipango ya mwaka mmoja mmoja na muda wa kati, kimkakati zaidi. Hivyo, mpango wa kwanza wa maendeleo wa muda mrefu (1964 – 1980) ulitayarishwa ambapo utekelezaji wake uligawanywa katika vipindi nya miaka mitano mitano. Mpango huo ulianza kutekelezwa kuititia Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (1964 – 1969) na kufuatiwa na ule wa 1969 – 1974 na wa mwisho 1975 – 1980.

Baada ya kipindi cha mpango wa muda mrefu wa kwanza kukamilika, Serikali iliandaa mpango wa muda mrefu 1981 – 2000. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo haukufanyika ipasavyo kutokana na msukosuko wa uchumi duniani uliosababisha nchi nyingi ikiwemo Tanzania, kuanzisha mikakati ya programu za muda mfupi za kunusuru na kurekebisha uchumi. Programu za muda wa mwaka mmoja hadi mitatu na zile za kisekta, zimeendelea kutekelezwa hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio kadhaa yaliyopatikana chini ya mpango na programu hizi za muda mfupi, ilibainika wazi kuwa mafaniko hayo hayakuwa endelevu na ya kutegemewa kama msingi wa kutufikisha katika malengo ya muda mrefu ya ustawi wa Taifa letu kiuchumi na kijamii. Msingi kama huo unahitaji falsafa ya muda mrefu ya usimamizi wa uchumi. Hivyo, mwaka 1999 Serikali ilikamilisha Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 kama chombo cha katuongoza katika kufikia maendelo ya uchumi na ustawi wa jamii kwa robo karne ya kwanza ya karne ya 21. Lengo la msingi la dira ni kuiwezesha nchi yetu kufikia hadhi ya nchi zenye kipato cha kati, yaani *Middle Income Country*, ifikapo mwaka 2025. Aidha, malengo mahususi ya dira ni:-

- (i) Kumwezesha kila Mtanzania kuishi maisha bora na mazuri;
- (ii) Kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa ya amani, utulivu na umoja;
- (iii) Kujenga msingi wa utawala na uongozi bora;
- (iv) Kujenga jamii iliyoelimika na inayopenda kujifunza; na
- (v) Kujenga na kuendeleza uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa dira ulipangwa kuzingatia mfumo wa mipango ya muda mrefu na wa kati, kuanzia mwaka 2000, hili halikuwezekana kwa kuwa wakati huo nchi yetu ilikuwa imefikia makubaliano na Shirika la Fedha Duniani (*IMF*), kufuatilia uchumi wa Taifa kwa karibu ili iweze kupata misamaha ya madeni. Aidha, kiasi cha fedha kilichopatikana chini ya msamaha wa madeni kilikuwa hakina budi kutumika katika mpango uliokuwa ukisimamiwa kwa karibu na *IMF* na Benki ya Dunia chini ya programu ya kupunguza umasikini. Tangu wakati huo, mfumo wa utayarishaji mpango uliendelea kuwa ni wa miaka mitatu mitatu. Hivyo, badala ya kupanga kwa malengo yenye vigezo na viashiria thabiti nya ufanisi, tukaanza kupanga kwa mfumo rejea (*Rolling Plan and Forward Budget*), kuwezesha malengo kufanyiwa marejeo kila

mwaka, kuakisi hali halisi ya mwenendo wa uchumi nchini na uhakika wa upatikanaji wa misaada ya wahisani.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 18 Novemba, 2010 wakati wa kuzindua Bunge lako la Kumi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais, alitumia fursa hiyo kuutangazia umma wa Watanzania juu ya uamuvi wa Serikali wa kurejea utaratibu wa kuwa na mipango ya muda mrefu na wa kati katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya maka 2025. Aidha, alibainisha kwamba kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa dira, ni muda mrefu na hivyo ipo haja ya msingi ya kufanya mapitio na tathmini ya utekelezaji. Dhamana ya kazi hiyo walipewa Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, ambayo katika kupitia dira, walipaswa kuzingatia maendeleo yaliyofikiwa nchini kikanda na Kimataifa ili kubaini kama malengo ya dira bado yanakidhi matakwa ya Taifa na wananchi na kuhuisha panapostahili. Aidha, kwa ajili ya kuweka utaratibu mahsuswi wa uratibu, ufuatiliaji na kufanya tathmini ya kina, Tume ilitakiwa kuandaa mkakati wa utekelezaji wa dira kwa kipindi cha miaka 15 iliyosalia na mkakati huo utekelezwe kupitia mipango mitatu ya miaka mitano mitano.

Mheshimiwa Spika, mpango ninaouwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, ni wa kwanza wa mlolongo wa mipango hiyo.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa dira katika kipindi cha muongo mmoja yamebaini matokeo mchanganyiko kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mwenendo wa Uchumi umekuwa wa kuridhisha, hasa katika viashiria vya uchumi jumla. Tangu mwaka 2001 licha ya athari ya msukosuko wa uchumi duniani kwa miaka ya 2008 na 2009, pato la Taifa lilikuwa kwa wastani wa 7%. Mfumko wa bei ulidhibitiwa chini ya kiwango cha 6% licha ya bei za mafuta ya petroli na chakula duniani kupanda kwa viwango vikubwa. Hali kadhalika, kumekuwa na mafanikio ya kuridhisha kwa upande wa makusanyo ya mapato ya kodi ya Serikali. Wastani wa makusanyo ya kodi kwa kipindi cha Julai, 2010 – Aprili, 2011 ulifikia shilingi bilioni 430 kwa mwezi, ukilinganisha na shilingi bilioni 84.7 mwaka 2001/2002.

Mafaniko hayo yalitokana na marekebisho ya mfumo wa ukusanyaji kodi, kuimarika kwa usimamizi na kuanzishwa kwa kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Mheshimiwa Spika, mafanikio mengine ni pamoja na kuongezeka kwa akiba ya Taifa ya fedha za kigeni. Hili lilichangiwa na kuimarika kwa mauzo ya nje kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2006 – 2010. Thamani ya mauzo ya bidhaa za nje yaliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 3,271.4 mwaka 2006 hadi dola za Kimarekani milioni 5,876.5 mwaka 2010. Kutokana na hali hii, akiba ya fedha za kigeni mwaka 2010 ilifikia dola za Kimarekani milioni 3,948 inayotosheleza mahitaji ya ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa muda wa miezi sita, ikilinganishwa na kiasi cha dola za Kimarekani milioni 3,552.5 mwaka 2009 kilichokuwa toshelevu kwa muda wa miezi mitano. Hata hivyo, bado ununuzi wa bidhaa kutoka nje ni mkubwa ukilinganisha na mauzo yetu nje ambapo kwa kipindi hicho, thamani ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje

iliongezeka kutoka dola za Kimarekani milioni 5,113.4 hadi dola za Kimarekani milioni 8,963.2 na hivyo kusababisha kuwepo kwa nakisi katika akaunti ya malipo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, wastani wa jumla wa mikopo kwa benki binafsi, umekuwa ukiongezeka kwa wastani wa asilimia 33.8 kwa kipindi cha mwaka 2002 – 2010, kuashiria kuanza kuimariika kwa sekta binafsi ya ndani. Kumekuwa na mabadiliko kiasi katika mfumo wa uchumi nchini, yakipimwa na mchango wa shughuli za kiuchumi katika pato la Taifa. Mchango wa sekta ya huduma na biashara umeongezeka kufikia asilimia 46.6 katika kipindi cha miaka mitano (2006 – 2010), ambapo mchango wa Sekta ya Kilimo umepungua kutoka asilimia 40 mwanzoni mwa miaka ya 2000 mpaka asilimia 25.3 mwaka 2010. Mchango wa shughuli za kilimo ulishuka kutokana na kuongezeka kwa kasi kwa shughuli nyingine za uchumi. Mchango wa sekta pana ya viwanda uliongezeka kufikia asilimia 22.4 mwaka 2010 ukilinganisha na asilimia 18 mwaka 2001.

(b) Mheshimiwa Spika, katika sekta za huduma ya jamii kulikuwa na mafanikio katika maeneo mengi, hususan katika upatikanaji wa huduma ya elimu. Udhili katika Shule za Msingi uliongezeka kufikia wanafunzi 8,419,305 mwaka 2010 kutoka wanafunzi 4,394,320 mwaka 2000. Udhili Shule za Sekondari ulifikia 1,500,000 kutoka wanafunzi 262,000 na udhili katika Vyuo Vikuu uliongezeka kutoka wanafunzi 20,740 hadi kufikia 118,000 katika kipindi hicho. Aidha, sehemu ya jamii inayopata huduma ya maji safi iliongezeka kutoka asilimia 53 hadi asilimia 58.7 kwa maeneo ya vijijini na kutoka asilimia 74 hadi asilimia 84 kwa maeneo ya mijini katika kipindi cha mwaka 2000 – 2010. Wastani wa umri wa kuishi uliongezeka kutoka miaka 51 hadi miaka 58. Vifo vya watoto chini ya umri wa miaka mitano vilipungua kutoka 112 hadi 81 kati ya watoto 1000 wanaozaliwa wakiwa hai, wakati vifo vya akina mama wajawazito vilipungua kutoka 578 mpaka 454 kati ya wajawazito 100,000.

Mheshimiwa Spika, mapitio pia yalibainisha kuwepo kwa changamoto ambazo hatuna budi kuelekeza nguvu zetu kuzitatua. Hizi ni pamoja na:-

- (i) Kiwango cha ukuaji wa uchumi, licha ya kuongezeka bado ni chini ya wastani wa 8% iliyokusudiwa;
- (ii) Kiwango cha umasikini nchini kimepungua kwa kiwango kidogo sana cha 2% tu ambayo haitoshelezi, kutoka asilimia 35.6 mwaka 2000/2001 hadi asilimia 33.4 mwaka 2007;
- (iii) Ongezeko la mapato ya ndani bado halikidhi mahitaji ya shughuli za Serikali, hivyo kuwepo kwa nakisi katika bajeti ya Serikali na hivyo kuendelea kutegemea kwa kiasi kikubwa cha asilimia 25 ya misaada kutoka nje;
- (iv) Sehemu kubwa ya sekta binafsi na nguvu kazi ya ndani kushindwa kushiriki katika shughuli za uchumi na biashara rasmi za kimataifa na hivyo kujikita katika mkondo wa uchumi usio rasmi;

- (v) Wigo mdogo wa mapato ya kodi na vyanzo visivyo vya kodi;
- (vi) Hali duni ya miundombinu, hususan ya umeme, usafirishaji na uchukuzi na hivyo ushindani wa nchi katika biashara ya kimataifa kuwa duni licha ya fursa nyingi tulizonazo;
- (vii) Kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kutokana na fursa finyu za upatikanaji wa mitaji na mikopo na upungufu wa rasilimali watu ya ndani yenye weledi na ujuzi kuweza kushindana au kushindania fursa za ajira zinazojitokeza katika shughuli za uchumi wa kisasa;
- (viii) Kiwango cha chini cha ubora wa mijji na makazi mijini na vijijini, ambapo zaidi ya asilimia 90 ya makazi mijini hayajapimwa na ugumu katika upatikanaji wa hati miliki. Makazi ya vijijini bado ni duni sana;
- (ix) Ukuaji wa mauzo nje umedumaa kwenye kiwango cha asilimia 12 kwa kipindi cha miongo miwili ikilinganishwa na ongezeko la ununuzi kutoka nje kutoka 4% kwa mwaka, miaka ya 1990 hadi takribani asilimia 15 katika miaka ya 2000; na
- (x) Sekta ya viwanda bado ni changa (asilimia 22.4 ya pato la Taifa mwaka 2010).

Mheshimiwa Spika, katika maudhui ya Mpango, kama nilivyosema punde, Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 ni wa kwanza katika mlolongo wa mipango mitatu ya miaka mitano ya utekelezaji wa mkakati wa kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 katika kipindi cha miaka 15 kilichosalia. Kitu kitakachotia matumaini ni kuwa mapitio ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 yamebainisha kwamba nchi yetu ina kila sababu ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025 kufikia kipindi kilichobakia, hasa kwa kuzingatia utajiri wa rasilimali uliopo. Hata hivyo hali hii inawezekana tuendapo, rasilimali hizo zitatumiwa vizuri. Hivyo, maudhui ya mpango huu ni kuturejesha katika utaratibu utakaotuwezesha kutumia rasilimali zetu kimkakati kufiki malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, dhana iliyobebwa na mpango huu ni kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Taifa. Hdhamira ya Serikali katika miaka mitano ijayo ni:-

- (i) Kutanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi vilivyopo;
- (ii) Kujenga uwezo wa nchi kukua kiuchumi na kuondoa umaskini kwa haraka inavyowezekana; na

- (iii) Kujidhatiti katika kutumia katika kutumia kwa ufanisi na kimkakati fursa zinazoibuka kutokana na mahusiano mapya ya kiuchumi, kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kutimiza dhana hiyo mpango huo umejikita katika nguzo nne zifuatazo:-

- (i) Kuendeleza utulivu wa uchumi jumla na kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji na kadhalika;
- (ii) Kutumia fursa za raslimali tele za Tanzania kama mota ya kukuza uchumi. Mkazo zaidi utawekwa katika mapinduzi ya kijani, yaani kilimo kwanza;
- (iii) Kutumia fursa nzuri ya Tanzania kijiografia ili kufanya nchi yetu kuwa lango kuu la biashara kuhudumia nchi za maziwa makuu. Tunalenga kuboresha bandari, reli na viwanja vya ndege; na
- (iv) Kukuza matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifufutu katika maendeleo ya kilimo na viwanda. Hapo msisitizo ni kuongeza kiwango cha elimu hasa ya sayansi na ufundi stadi na kukuza matumizi ya *TEHAMA* kama nyenzo ya kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, kama alivyowahi kutuasa hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, kupanga ni kuchagua. Ili tufikie tunakotarajia, lazima tuweze kuchagua maeneo machache ya kipaumbele yanayopendekezwa kutekelezwa katika miaka mitano ijayo. Maeneo hayo yamebainishwa kwa kuzingatia dhana ya kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa Tanzania ili kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi na hatimaye kutupatia uwezo zaidi wa kupunguza umaskini kwa kiasi kikubwa na kwa haraka zaidi, tofauti wa upatikanaji wa vipaumbele katika mpango wa programu mbalimbali.

Mpango huu hauweki vipaumbele vya sekta, badala yake vipaumbele vinabainisha kwa kuzingatia shughuli au miradi ya mkakati itakayotekerezwa ili kuimarisha usimamizi na utekelezaji. Mpango umebainisha malengo mahususi yatakayotumika kupima ufanisi wa utekelezaji na matokeo tarajiwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele na malengo ya utekelezaji katika kipindi cha 2011/2012 - 2015/2016 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Miundombinu, hasa upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu na ya uhakika kwa mahitaji na kuuza katika nchi jirani. Sanjari na hili mkazo umewekwa katika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji hasa bandari, reli na barabara kutuwezesha Tanzania kuwa lango kuu la kibiashara na huduma kwa nchi jirani zisizo na bahari. Malengo ya utekelezaji ni kuongeza uzalishaji wa umeme kufikia *Megawatt* 2780

mwisho wa mpango wa miaka mitano. Kuboresha njia ya usafirishaji umeme na usambazaji kujenga barabara za lami zeny urefu wa kilomita 5205 kuongeza uwezo wa kuhudumia mizigo bandarini kufikia tani milioni 9.87 kutoka tani milioni saba na usafiri wa anga kusafirisha tani 35,500.

(ii) Viwanda ni eneo mkakati hasa katika kuwezesha kuthamanisha mazao ghafi ya kilimo na maliasili. Vilevile katika kutoa soko la ajira na pia bidhaa za uzalishaji kwa maeneo mengine ya vipaumbele, mkazo umewekwa katika kuendeleza viwanda vya nyama, ngozi, maziwa na usindikaji wa mazao ya kilimo na maliasili. Malengo ya utekelezaji katika eneo hili ni kujenga angalau viwanda vitatu vya nyama mfano Ruvu, Dodoma na Shinyanga, kufufua viwanda vya kusindika ngozi Mwanza ambavyo viko tayari na Kilimanjaro na kupanua usindikaji wa mazao ya kilimo kufikia asilimia 40.

Malengo mengine ni kujenga angalau viwanda viwili vya kuzalisha mbolea kwa kutumia gesi iliyoko Mtwara na *Phosphate* iliyoko Arusha. Kupanua uzalishaji wa saruji na kuongeza angalau viwanda viwili vya bidhaa nyingine za ujenzi na uunganishaji wa matrekta ili kuongeza uwekezaji na ufanisi katika viwanda. Mkazo umewekwa katika kupanua maeneo maalum ya viwanda, yaani *Special Economic Zones* ambapo kiasi cha maeneo matano yataongezwa Bagamoyo, Mtwara, Tanga, Kigoma na Arusha pamoja na yale mengine ambayo tayari yapo.

(iii) Kwa kuwa kilimo ni sekta mama na kiungo muhimu katika kukua kwa sekta nyingine zinapoipatia pembejeo na yenewe kutoa malighafi kwa sekta nyingine na kwa kuzingatia kwamba karibu asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kilimo, Mpango huo unasisitiza kilimo na biashara na uongezaji thamani. Aidha, kwa kuzingatia mabadiliko ya tabia-nchi msukumo umewekwa katika kuongeza maeneo ya kilimo cha umwagiliaji na kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji na kupanua miundombinu ya umwagiliaji.

Malengo ni pamoja na kupanua eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni moja na kufikia utoshelevu wa mahitaji ya chakula asilimia 120. Mpango unapendekeza kujikita katika maeneo machache ya kilimo na yenyе fursa kubwa. Kwa mantiki hii, kilimo kitaanza kuendelezwa kikanda na kutoa msukumo kwa mazao maalum, ambapo ukanda maalum wa kilimo Kusini mwa nchi yetu, yaani *SAGCOT* utaanzishwa na mkazo utakuwa katika mazao ya chakula hasa Mahindi na Mpunga na pia matunda, miwa, maua na mboga mboga. Mazao yatakayotiliwa mkazo katika maeneo mengine ni viungo, zabibu, mbegu za mafuta na kilimo cha miwa. Aidha, msukumo umewekwa katika kuongeza uzalishaji wa mazao ghafi ya uzalishaji viwandani hasa pamba, miwa na katani sawia na kuendeleza ufugaji wa mifugo na uvuvi ikiwa ni pamoja na kujenga viwanda vya uongezaji thamani wa mazao hayo. Hatua hizi zitaongeza ajira mpya kufikia 140,000 katika kipindi cha miaka mitano. Hizo ni ajira rasmi.

(a) Rasimali Watu, hasa katika kuboresha elimu ya sayansi na ufundu na kuongeza matumizi ya sayansi, teknolojia na ufundu na kuongeza matumizi ya sayansi, teknolojia na ugunduzi. Uendelezaji wa rasimali watu utazingatia mahitaji, hususan katika maeneo ya vipaumbele kwa sasa na katika muda mrefu. Baadhi ya malengo katika

eneo hili ni pamoja na kuongeza udahili wa wanafunzi katika ngazi za Vyuo vya Elimu ya Juu kufikia asilimia nne, udahili wa walimu wa ngazi ya diploma na daraja ‘A’, kufikia 133,000 kwa mwaka; ujenzi wa Chuo cha MUHAS - Mlonganzila, Shule Kuu ya Udaktari katika Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Butiama sawia na ukarabati na upanuzi wa uwezo wa Vyuo vitano vya Elimu ya Juu; Vyuo vya Teknolojia Mbeya na Dar es Salaam na Ufundu Stadi VETA na uimarishaji wa Shule za Kata, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii pamoja na uendelezaji wa walimu katika Vyuo hivyo.

(b) Maji, kwa maana ya kuongeza hifadhi ya maji ya mvua na vyanzo vya maji na ujenzi wa miundombinu ya ugavi wa maji ili kumaliza tatizo sugu la upatikanaji maji kwa ajili ya uzalishaji viwandani na matumizi ya kawaida, vijijini na mijini na kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Mpango umetilia mkazo wa uendelezaji wa miundombinu ya majitaka. Malengo ni kuongeza upatikanaji wa majisafi mijini kufikia asilimia 95 na asilimia 65 vijijini. Aidha, upatikanaji wa huduma za majitaka utafikia asilimia 80 kwa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, mpango pia unabainisha masuala ya msingi ambayo ni lazima yazingatiwe kuleta ufanisi katika utekelezaji wake. Masuala haya ni pamoja na:-

- (i) Kuhakikisha utengamavu wa uchumi jumla ikiwa ni pamoja na kudhibiti mfumko wa bei katika viwango stahimilivu kwa uwekezaji na gharama za maisha;
- (ii) Kudumisha na kuboresha utawala bora unaozingatia sheria ikiwa ni pamoja na uwajibikaji kwa mali za umma na maslahi ya nchi na wananchi;
- (iii) Kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji; na
- (iv) Mipango ya ardhi kwa matumizi ya uwekezaji, mijini na vijijini, na kwa uendelezaji wa miundombinu na makazi ikiwa ni pamoja na kuongeza kasi ya upimaji na kuimarisha upatikanaji wa hatimiliki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mabadiliko ya uchumi ya mfumo wa uchumi, inakusudiwa kuwa ifikapo mwaka 2015/2016 mchangwa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa ufikie asilimia 26.5 toka asilimia 24 mwaka 2009 na bidhaa za viwanda kufikia asilimia 12.9 toka 9% mwaka 2009. Ili tuweze kwenda kasi, inabidi tuimarishe na tujenge viwanda vipyta vya kusindika mazao kuongeza ubora na thamani ya bidhaa na pia viwanda vya msingi. Aidha, mchangwa sekta ya huduma na biashara unatakiwa kuongezeka kutoka asilimia 47.6 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 48.6 mwaka 2015/2016. Wakati mchakato wa sekta hizo ukitarajiwa kuongeza, mchangwa sekta ya kilimo utapungua kutoka asilimia 28.4 mwaka 2009 hadi asilimia 20.7 mwaka 2015/2016 wakati wafanyakazi wengi watakuwa wanahama katika kilimo na kwenda katika viwanda.

Mheshimiwa Spika, mpango huu unajipambanua kwa kuweka vigezo bayana vya kupima ufanisi wa utekelezaji. Vigezo hivi vimepambanuliwa katika maeneo ya uchumi jumla, mabadiliko ya mfumo wa uchumi kisekta na matarajio katika utekelezaji wa vipaumbele vya mpango wenyewe. Mathalan, katika eneo la uchumi jumla inakusudiwa kuwa ifikapo mwaka 2015/2016:-

- (i) Uchumi wa Taifa uwe unakua kwa wastani wa 8% hadi 10% kwa mwaka;
- (ii) Mfumko wa bei udhibitiwe chini ya kiwango cha 5%;
- (iii) Thamani ya mauzo ya nje ifikie asilimia 23 ya pato la Taifa;
- (iv) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kufikia asilimia 19 ya pato la Taifa;
- (v) Akiba ya fedha za kigeni yenye uwezo wa kukimu uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi sita;
- (vi) Wastani wa kipato cha mwananchi kuongezeka hadi dola za Kimarekani 650 na;
- (vii) Kupunguza utegemezi wa wahisani hadi asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, mpango unasisitiza kufanyika kwa mabadiliko makubwa katika utayarishaji wa mipango na bajeti kukidhi hitaji la kupanga kimkakati. Unasisitiza pia kuwa, katika kupanga, ni muhimu kuanza kwa kubainisha fursa zitakazowezesha kufikia kwa malengo ya muda mrefu badala ya tunavyozoea kwa kupanga kukidhi mahitaji ya muda mfupi na ya kadri upatikanaji wa fedha za ndani na misaada ya wahisani ambayo mara nyingi ni kidogo. Mpango huu utazitaka Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na pia Mikoa na Halmashauri kufungua ukurasa mpya wa utayarishaji wa mipango kwa kuzingatika malengo na vipaumbele vya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mpango huu unazingatia sera za jumla za uendeshaji na usimamizi wa uchumi nchini unaojielekeza katika mfumo wa soko na ushirikishwaji wa sekta binafsi hata katika maeneo ambayo awali yalikuwa maalum kwa Serikali tu. Kwa mantiki hii, sekta binafsi katika mpango huu inapewa fursa ya kutambua mapema mwelekeo na vipaumbele vya Serikali kuiwezesha kuijandaa kushiriki kwa karibu zaidi katika utekelezaji wa mpango. Kwa ajili hii, sera ya uwekezaji kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, yaani *PPP* inakuwa nyenzo mahususi katika utekelezaji wa mpango huu. Sawia na hili, suala la kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji linapewa umuhimu wa kipekee.

Mheshimiwa Spika, moja ya kasoro zinazobainishwa katika mapitio ya utekelezaji wa dira ni kukosekana mfumo bayana wa ufuatiliaji na kutathmini utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Mpango huu umejielekeza katika kufuta kasoro hii na hivyo unabainisha mpangilio mzima wa utekelezaji, utaratibu wa ufuatiliaji wa namna

ya kupima matokeo. Pamoja na kutathmini yaliyofanyika mwisho mwa kipindi cha mpango, uchambuzi wa kina utafanyika kila mwisho wa mpango na bajeti ya mwaka kwa kila Wizara, Idara na Wakala wa Serikali. Pia kwa Mikoa na Halmashauri, uchambuzi huu utazingatia viashiria viliwyowekwa ili kujua hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa majukumu kitaasisi, ni vyema nikasisitiza hapa kwamba sekta na taasisi zote za utekelezaji zina wajibu wa msingi na hivyo zitahusika katika kupima utekelezaji wa mipango yao. Hata hivyo, Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha zitaendelea kuwa taasisi viongozi katika kuratibu utayarishaji na kutathmini utekelezaji wa mpango na bajeti. Tathmini itafanyika kila mwaka kabla ya kutoa mwongozo wa utayarishaji wa mpango wa bajeti ya mwaka unaofuata. Wizara, Mikoa na Taasisi nyingine za Serikali, asasi za kiraia na sekta binafsi zitakuwa na wajibu wa kuratibu na kutathmini utekelezaji katika ngazi zao.

Mheshimiwa Spika, ni vema nikaweka wazi pia kufanikiwa kwa mpango huu kwa kiasi kikubwa kutategemea sana ushiriki wa makundi yote ya Watanzania kwa nafasi zao. Hivyo lengo la mpango huu ni kuhamasisha na kuratibu ushirikiano wa makundi yote ya Watanzania katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Kwa mantiki hii muhimu kwa Watanzania wote kujenga dhana ya “Tunaweza” na kuondokana na fikra za kutegemea. Dhana ya utegemezi wa wananchi kwa Serikali au wafadhili siyo endelevu, hivyo, ni muhimu kwa kila kundi kufahamu na kutimiza wajibu wake kikamilifu kwa nafasi yake na kwa kushirikiana na wadau wengine. Makundi haya ni pamoja na Serikali, sekta binafsi washirika wa maendeleo, vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ni wa kwanza katika mlolongo wa mipango ya kufanikisha malengo ya dira. Kilicho dhahiri ni kuwa, mabadiliko ya ushirikishwaji mpana utahitajika kuwawezesha wadau waelewe na kuunga mkono mwelekeo huu. Serikali ina wajibu wa msingi wa kutoa mwongozo na maelekezo ya jumla kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. Pia Serikali itakuwa na wajibu wa kutunga sera na kubuni vivutio vya uwekezaji na kusimamia utekelezaji wake.

Vilevile wajibu wa Serikali ni kutangaza maeneo ya vipaumbele vya uwekezaji. Kwa kuwa upatikanaji wa fedha utakuwa kikwazo kwa utekelezaji wa mpango huu, Serikali inabakia na wajibu wa msingi kupanua vyanzo vya fedha kwa ajili ya utekelezaji ikiwa ni pamoja na kuimarisha vyanzo vipyta vya mapato ya ndani na nje na kujenga mahusiano mapya ya kimaendeleo na biashara na nchi za nje.

Kwa ujumla Serikali ina wajibu wa kuongoza tafsiri ya dira na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii yanayohitajika. Serikali vilevile ina wajibu wa kujenga, kuimarisha na kuhakikisha uwepo wa mazingira bora kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huo. Mazingira hayo ni pamoja na kuwepo kwa utawala bora, utawala wa sheria, demokrasia, haki za binadamu, kuzuia rushwa, uwazi na uwajibikaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi, Serikali inapaswa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kama vile kutenga ardhi iliyopimwa na yenye miundombinu inayotakiwa, kupunguza urasimu na kuondoa kero zote katika huduma zinazohusiana na utaratibu wa uwekezaji ili kuwezesha sekta binafsi kukua na kuimarisha ipasavyo na kushirikia kikamilifu katika utekelezaji wa mpango huo. Serikali inapaswa kudumisha misingi ya ustahimilivu wa uchumi jumla, yaani *macro economic stability* kwa kuhakikisha sera bora za kodi na za kifedha zinaendelezwa, kukuza kasi ya ukuaji wa uchumi, kudhibiti mfumko wa bei na kuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, kuagiza bidhaa nje, pamoja na kuongeza kiwango cha mauzo ya bidhaa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo sekta binafsi haiwezi kuwekeza, Serikali itajenga, itaboresha na kukuza miundombinu kama vile kuhakikisha uwepo wa umeme, maji, barabara pamoja na miundombinu ya usafirishaji Vijiji na kuendeleza kuboresha raslimali watu.

Mheshimiwa Spika, mpango unatoa fursa kwa sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za kiuchumi hususan uzalishaji na usambazaji wa bidhaa na huduma. Mchango wa sekta binafsi unatazamiwa kwa kiasi kikubwa kuwekezwa katika kilimo ikiwa ni pamoja na miundombinu ya umwagiliaji, usambazajiwa pembejeo za kilimo, kilimo cha mazao yenye thamani kubwa (maua, mboga mboga, matunda, viungo na zabibu), mazao ya kipaumbele ambayo ni pamba, miwa, katani, mahindi na mpunga pamoja na Uvuvi na ufugaji.

Vilevile sekta binafsi imepewa fursa ya kuwekeza katika viwanda vitakavyosaidia kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na maliasili. Kuwekeza katika viwanda ambavyo vitawezesha utumiaji wa malighafi zinazopatikana humu nchini. Mfano, viwanda vya mbolea (vitatumia gesi asilia na fosfati) viwanda vya saruji (vitatumia chokaa) na viwanda vya chuma (vitumia madini ya chuma kutoka Mchuchuma na Liganga).

Vilevile mpango unatoa fursa ya uwekezaji katika viwanda vinavyotumia vipuri kutoka nje kwa ajili ya kuunda mitambo na vifaa mbalimbali (*Assembling Plants*) ambavyo vinahitajika kwa wingi nchini mfano matrekta na pipipiki. Vilevile, sekta binafsi ina nafasi kubwa ya kuwekeza katika ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ambayo watumiaji kwa malipo kama vile uzalishaji na usambazaji wa umeme kibashara na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano kati ya Serikali na sekta binafsi utazingatia sera, sheria na kanuni za ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Wajibu wa sekta binafsi katika sera, sheria na kanuni hizi ni pamoja na kufanya upembuzi yakinifu wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ukusanyaji wa raslimali zinazohitajika, upimaji na tathmini ya utekelezaji, kutoa utaalamu wa kiufundi na usimamizi.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa mpango huu, inategemewa kuwa, washirika wetu wa maendeleo watasaidia kujaza pengo la raslimali-fedha pale ambapo raslimali za ndani zitakuwa hazikutosha inatarajiwa kuwa misaada hii itatolewa katika

wakati na kiwango kitakachoahidiwa. Aidha, washiriki wa maendeleo watatoa misaada ya kitaalamu kwa namna ambayo itajenga uwezo wa utaalamu wa ndani wa kuendesha kazi mara wataalamu wa nje watakapoondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vijana wanachukua karibu 60% ya nguvu kazi ya Taifa na hivyo ushiriki wao katika utekelezaji wa mpango huu unategemewa kwa kiasi kikubwa katika nyanja zote za uchumi. Maeneo yote ya kipaumbele katika Mpango huu (kilimo, viwanda, uendelezaji wa miundombinu na maji) yatatoa fursa mbalimbali kwa vijana kuajiriwa na kujajiri. Mkakati wa kutekeleza mpango huu umejielekeza katika kuwaandaa na kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika fursa zote zitakazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine, mpango unazingatia kuwajengea vijana uwezo wa uongozi, ujasiriamali na stadi za maisha, kuhamasisha na kuwawezesha programu za ubadilishanaji ujuzi na teknolojia. Kuwapa vijana uwezo wa kifedha na mitaji kwa kuhimiza uanzishwaji wa *SACCOS* za vijana, kuanzisha programu zinazotumia nguvukazi katika maeneo ya vijiji na kuongeza udahili wa vijana katika Vyuo vya Ufundii, *VETA* na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Hivyo, ili kuweza kuzitumia fursa hizi ipasavyo, vijana wanapaswa kuwa na moyo wa uzalendo, maadili mema, utayari wa kulitumikia Taifa kwa uaminifu, wenyе maono na ubunifu, wenyе chachu ya mabadiliko chanya ya kimaendeleo na wenyе uthubutu katika kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi zilizoainishwa katika mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2002, maoteo ya nguvukazi nchini kwa mwaka 2010 ilikadiriwa kuwa na watu takribani milioni 43 ambapo asilimia 75 wanaishi kwa kutegeMEA kilimo na nusu yao ni wanawake. Hivyo, mwanamke anayo nafasi kubwa katika utekelezaji wa mpango huu.

Mpango umejielekeza katika kuhakikisha kuwa jinsia zote zinashiriki kikamilifu katika fursa zitakazojitokeza ndani ya mpango huu. Hivyo, wanawake wanategemewa kukunganishwa nguvu zao katika vikundi na kutekeleza miradi ya pamoja kwa kutumia vema fursa za huduma za fedha zinazotolewa na Benki ya Wanawake na taasisi nyingine za fedha. Inatarajiwa kwamba watoto wa kike watatumia vyema fursa ya kuijendeleza kielimu. Ikumbukwe kuwa nguvu kazi ya wanawake inawezesha nchi kujitosheleza kwa chakula. Serikali itaelekeza utaalamu kupitia mafunzo ya kilimo bora kwa wanawake ili waongeze uzalishaji na kuondokana na umaskini wa kipato. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, watu wenyе mahitaji maalum. Tanzania kama nchi ilivyo kwa jamii nyingi duniani, ina watu wenyе mahitami maalum yanayohitaji kuzingatiwa. Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) linakadiria kuwa na Tanzania ina karibu 10% ya watu wenyе ulemavu wa mwili. Hii ina maana kuwa, kwa sensa ya mwaka 2002, Tanzania ina takribani watu milioni 3.4 wenyе mahitaji maalum kutokana na ulemavu wa mwili. Tathmini zilizopo hata hivyo zinabainisha kuwa wapo watu wa kundi hili, licha ya changamoto zinazowakabili, wamemudu kukabiliana nazо hata kufikia mafanikio makubwa katika nyanja mbalimbali za maisha. Wapo wajasiliamali, viongozi wenyе taaluma na stadi maalum za kazi, wasanii na kadhalika. Hali hii inawashawishi kuwepo

kwa mtazamo mpya juu ya kundi hili. Ukweli ni kuwa, wakiwezesha kupata fursa stahiki wanaweza kuchangia kikamilifu katika ujenzi wa uchumi na maendeleo ya taifa letu. Mpango huu umezingatia na hivyo kujielekeza kutoa fursa zaidi za kuijendeleza na kujitutia maisha kwa watu wa kundi hili.

Mheshimiwa Spika, Umma wa Watanzania unaishi vijijini na katika mitaa mijini. Hivyo, kila kijiji na kila mtaa vinatakiwa kuwa na mpango wake wa kutekeleza mpango huu. Kadhalika, kila familia itekeleze mpango katika mazingira yao. Hal mashauri za Wilaya na Miji nazo zipange na kusimamia utekelezaji wa mpango katika mazingira yao.

Mheshimiwa Spika, aidha, wananchi wote tunao wajibu katika utekelezaji wa Mpango huu kwa kufanya kazi kwa bidii, kudumisha amani na utulivu, kutii sheria za nchi na kubadilisha fikra na mitazamo ambayo siyo rafiki kwa wajasiriamali, wawekezaji na uwekezaji nchini. Serikali inategemea wananchi tuamshe ukereketwa wa kimaendeleo na kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji kwa nia ya kutumia fursa hizi katika kupata ujuzi na kuongeza kipato na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, mahitaji na vyanzo vya raslimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu ni kiasi cha takribani shilingi trilioni 42.9 kwa kipindi cha miaka mitano, sawa na wastani wa shilingi trilioni 8.5 kwa mwaka. Fedha za Serikali katika utekelezaji wa mpango huu kwa miaka yote mitano ni takribani shilingi trilioni 13.5, sawa na wastani wa shilingi trilioni 2.7 kwa mwaka ikilinganishwa na na wastani wa sasa wa takribani shilingi trilioni 1.0 za bajeti ya maendeleo kwa mwaka katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Inapendekezwa pia kuwa kiasi cha asilimia 35 ya bajeti ya Serikali iwe kwa ajili ya maendeleo na fedha hizi zilindwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wa Serikali, vyanzo vingine katika kukimu utekelezaji wa mpango huu ni ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*PPP*), uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi, mikopo na misaada kutoka nchi wahisani, uwekezaji utakaofanywa na Watanzania wanaoishi nje, mifuko ya ushirikiano kama vile *China-Afrika, India-Africa, TICAD, OPEC na Benki za Maendeleo kama China-Exim, India-Exim, Korea-Exim na China Development Bank*.

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea maeneno ya hekima ya Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyyoyatoa kupitia hadhara ya Viongozi na Wazee wa Dodoma hivi karibuni wakati anautangazia umma hatua iliyofikiwa katika utayarishaji wa mpango huu. Nanukuu: “Haitawezekana kushinda mbio kama hujathubutu kushiriki katika mashindano ya mbio na haiwezekani kuwa na mshindi kama hujathubutu kuingia vitani.” Aliyasema na akarudia kwa Kiingereza kwamba: “*It is impossible to win the race unless you venture to run, impossible to win the war unless you dare to battle.*” (*Makof*)

Nayarejea maneno haya hapa kwa ajili ya kuweka bayana umuhimu wa Watanzania, kwa nafasi zao, kuunga mkono kwa vitendo mpango huu. Maendeleo ni vita, tena ya muda mrefu. Jemadari hata awe na nguvu kiasi gani, katu hawezikana kushinda vita

hii peke yake. Ushiriki mpana wa wananchi ndiyo msingi wa kwanza katika kupambana na umaskini na katika kutekeleza agenda yetu ya maendeleo ya kuwa mionganoni mwa nchi za uchumi wa kati, ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, huu ni mpango wa Taifa. Kila mtu au kikundi bila kujali itikadi za kisiasa tushiriki katika utekelezaji, usimamizi au uongozi wa wananchi kufikia azma hiyo. Hii ni sahihi, kwa vile wote tulipo hapa Bungeni tumechaguliwa ili kuwasaidia wananchi kujiletea maendeleo. Tunaweza kuhitilafiana katika mengine, lakini siyo katika lengo kuu la kuwapatia wananchi maisha bora. Wote tunajua maisha bora hayaweezi kupatikana bila kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania tuna ushuhuda wa nguvu ya mshikamano katika kushinda jambo lolote hata liwe kubwa na la dharura kiasi gani. Mwaka 1978 tulivamiwa na Nduli Idd Amin. Hatukuwa tumetarajia na hivyo hatukuiandaa kwa vita vile. Lakini kwa vile tulipovamiwa, kilichofanyika ni kuchukua wajibu wa msingi wa kizazi chochote kile, kulinda heshima na mipaka ya nchi yao. Tulishikamana na kushirikiana kwa kila hali kwa lengo la kumtoa mvamizi huyo. Sababu tulikuwa nayo, nia tulikuwa nayo, na uwezo pia tulikuwa nao.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Bunge lako Tukufu, ambao ndiyo wawakilishi wa umma wa Watanzanai. Safari hii tumejiandaa na kubainisha mkakati wa mapambano yetu. Hakika tutashinda. Tunalopaswa kuwa nalo ni kuambiana ukweli ili kila mmoja atimize wajibu wake. Maisha bora kwa kila Mtanzania yanawezekana, lakini ni kwa wale tu watakaothubutu kushiriki kupambana na umaskini na kupigania heshima ya nchi yao. Kama alivyosema Mwalimu, inawezekana, kila mtu atimize wajibu wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa mpango huu umehusisha makundi mbalimbali ya jamii ya Watanzania na wale wote wenye mapenzi mema na nchi yetu. Hivyo, sina shaka na uungwaji wake mkono katika hatua za utekelezaji. Kama ilivyo ada, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru wale wote walioshiriki katika kufanikisha maandalizi ya mpango huu chini ya uongozi wa Tume ya Mipango. Taasisi nyingine zilizokuwa na uwakilishi katika kikosi kazi ni Benki Kuu ya Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Idara ya Uchumi, Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii (*ESRF*), *Daima Associates* na *International Growth Centre (IGC)*. Kikosi kazi kilikuwa na baadhi ya Maafisa waandamizi wastaa fuwa Serikali, Taasisi mbalimbali za Serikali na sekta binafsi. Aidha, ningependa kutambua na kuthamini mawazo na ushauri mzuri wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Wizara za Kisekta, Idara na Taasisi za Umma na binafsi katika kubainisha vipaumbele vya mpango huu na mahitaji ya raslimali fedha.

Mheshimiwa Spika, nimewataja hawa kwa vile, mimi binafsi na Watendaji wa Tume ya Mipango, tunawiwa kwa ushiriki na michango yao ambayo kwa dhati imetusaidia sana kubainisha mwelekeo, maeneo ya vipaumbele na hatua mkakati za utekelezaji wa mpango. Kupitia meza yako naomba kuwashukuru kwa dhati kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba niwasilishe rasimu ya Mpango 2011/2012 - 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja Ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa*)

SPIKA: Hoja hii imeungwa mkono na sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia hoja hii yaani hoja ya Uchumi na Fedha, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda.

Wakati huo huo, napenda kuwataarifu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu amemkaimisha shughuli za Bungeni Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha Waziri wa Mambo ya Ndani. Naona kwa upande wa pili Kiongozi wa Kambi ya Upinzani amemkaimisha Mheshimiwa Vicent Nyerere, wana shughuli maalum, watakapokuja watachukua nafasi zao. Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda karibu!

MHE. DR. ABDALLAH O. KIGODA – MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 96(6) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025. Kamati yangu ilikutana na Tume ya Mipango zaidi ya mara mbili na kupata fursa ya kuchambua Mpango huu. Kamati ilitoa maoni yake ambayo kimsingi yamejumuishwa katika Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inampongeza Mheshimiwa Dr. Jakaya M. Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa taarifa ya kina tarehe 7 Juni, 2011 ya tamko la kisera kwa Taifa, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kuanzia Mwaka 2011/2012 hadi 2015/2016. Maeleo aliyoynaita kuhusu Mpango yameeleweka, hasa baada ya kuzingatia kuwa utaratibu wa awali wa nchi kupanga mipango yake kwa muda mfupi, lengo lilikuwa ni kuijandaa na utengamavu wa uchumi mkuu ili tuweze kuanza na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kamati inaishauri Serikali kufanya utaratibu wa kupata nakala ya hotuba ya Mheshimiwa Rais hapa Bungeni, iwe kama ni kubrashi rejea tunapoendelea kutathmini Mpango huu uliowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pili, Kamati inampongeza Mheshimiwa Stephen Wassira - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) pamoja na Wataalam wake na Tume ya Mipango kwa kuandaa Mpango Mzuri wa Maendeleo ya nchi yetu. Mpango huu uliandaliwa vizuri, ni tofauti na mipango mingine hasa ikizingatiwa kuwa uandaaji

wake umefanywa na Watanzania wenyewe, bila ya kutumia Wataalam kutoka nje ya nchi.

Kauli mbiu ya Mpango huu “Kufungulia Fursa za Ukuaji Uchumi Tanzania” inatoa mtazamo mpya wa kuelekeza nguvu za kitaifa katika maeneo ambayo yataibua viwango vya jumla na vya kisekta, kiuchumi na hatimaye kuendelea kupambana na changamoto kubwa la kupunguza umaskini wa mahitaji muhimu na ule wa kipato. Taarifa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Semina mbalimbali hapa Bungeni juu ya Mpango huu zimesaidia sana kuelewa na kutathmini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 48 hadi 70 wa Rasimu ya Mpango imetoa maelezo ya kina juu ya hatua za mkakati zitakazochukuliwa na Mpango katika maeneo muhimu. Maeneo ya kimkakati yatakayoshughulikiwa pamoja na utekelezaji wa uchumi mkuu/jumla utahusisha maeneo yafuatayo:-

Masuala ya utawala bora, ardhi, nyumba na makaazi; miundombinu kwa maana ya nishati, reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari, *TEHAMA*; Kilimo, Uvuvi na Mifugo; Viwanda; Maji na Majitaka; pamoja na Maendeleo ya Raslimali-watu na huduma za jamii. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa ukaribu matokeo ya utekelezaji wa malengo yaliyowekwa kufikiwa kwa Mpango.

Mheshimiwa Spika, mpangilio ni mzuri na unagusa maeneo muhimu ya kufungulia fursa za ukuaji wa uchumi wa nchi. Kulingana na vipaumbele vilivyowekwa changamoto kubwa ni uimara wa usimamizi, ufuutiliaji na utekelezaji wa Mpango na Malengo yake kwa ngazi zote, kitaifa, Mikoa, Halmashauri za Wilaya hadi ngazi za Vijiji; wananchi wakiwa ni wadau wakubwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) ni Awamu ya Kwanza ya Mpango Elekezi (*Roadmap*) wa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 kwa kipindi cha miaka 15 iliyobaki. Hii ni kwasababu katika kipindi cha miaka 10 iliyopita, utekelezaji wa malengo ya Dira pamoja na mafanikio yaliyopatikana yapo maeneo ambayo yangelifanya Taifa liwe katika nafasi nzuri ya kuwa Taifa lenye hadhi ya nchi zenye kipato cha kati ifikapo mwaka 2025, lakini hatukuweza kufikia malengo yaliyowekwa. Baadhi ya maeneo hayo ni pamoja na kudumaa kwa ukuaji wa kilimo(wastani wa asilimia 4.2 kwa mwaka), mchango mdogo wa Sekta ya Viwanda wa asilimia 24 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 31 kwa nchi zenye hadhi ya kipato cha kati, gharama kubwa ya kufanya biashara kutokana na mapungufu ya kisheria, urasimu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi, uamuzi wa Serikali kurejea katika utaratibu wa kuwa na mipango ya miaka mitano mitano, umechochewa na azma ya Serikali ya kuongeza kasi ya kupunguza umaskini, kuimarisha mafanikio yaliyopatikana katika huduma za jamii hasa elimu na kuimarisha uchumi ili uweze kukabiliana na mabadiliko ya uchumi Duniani.

Mheshimiwa Spika, mpango huu ni wa kitaifa ambao utahitaji juhudu kubwa na maarifa ya kuleta mabadiliko sisi wenyewe. Unahitaji tujenge uzalendo mkubwa baina yetu, hasa kwa vile Watanzania wote ni Wadau. Mpango huu ni Mwongozo utakaotekeleza vipaumbele vichache vitakavyoharakisha ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini, pamoja na kuboresha na kuendeleza huduma za jamii. Kamati imeridhika kuwa vipaumbele vilivyowekwa ni vichache vinavyozingatia mahitaji ya dharura na ya lazima na vina matokeo tarajiwa na yatasaidia walengwa yakitekelezeka kwa usimamizi na ufuutiliaji mzuri.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele hivyo, kwanza ni miundombinu, lengo likiwa ni kuondoa vikwazo hasa umeme, huduma za bandari, usafiri wa anga, sayansi, teknolojia na ubunifu, barabara na reli.

Pili, Kilimo, Ufugaji na Uvuvi, lengo likiwa ni kuongeza tija na kuwanufaisha maskini ambao wengi wanaishi vijijini kwa kutegemea sekta hizi tatu. Tatu, Viwanda, lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji wa bidhaa na kutoa fursa za ajira hasa kwa vijana. Msisitizo ukiwekwa kwenye eneo la kuongeza thamani ya bidhaa zetu za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Nne, maji, lengo likiwa kuboresha huduma za maji mijini na vijijini kwa matumizi ya nyumbani, viwandani, kilimo na kuzalisha umeme. Tano, maendeleo ya raslimali watu, lengo likiwa kuwekeza katika miundombinu ya elimu ya juu na Vyuo vya Ufundu Stadi, upatikanaji wa huduma za afya na matumizi bora ya raslimali iliyopo yenye ujuzi.

Mheshimiwa Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu mpango ni kuwa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016) ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025. Maoni ya Kamati kuhusu Mpango ni kuwa mpango tunaoujadili umeandaliali vizuri baada ya kuuchambua na kuupitia malengo yake, vipaumbele vyake na mikakati ya utekelezaji. Tathimini iliyofanywa na Kamati inaiongoza kutoa maoni na mapendekezo yafuatayo:-

- (1) Usimamizi, ufuutiliaji na utekelezaji;
- (2) Upatikanaji wa raslimali za mpango;
- (3) Maeneo ya haraka ya kuangaliwa;
- (4) Mpango na uwiano wa maendeleo; na
- (5) Uwajibikaji wa wadau wote wa mpango.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha na kuimarisha mfumo wa utaratibu wa kufuatilia, kusimamia na kutekeleza mpango huu, upo umuhimu kwa Serikali kuifanyia marekebisho Sheria ya Mwaka 1989 ilioanzisha Tume ya Mipango kama chombo cha kuratibu mipango ya nchi. Sheria hii ihuishwe na itoe nguvu zaidi kwa Tume ya

Usimamizi na Uratibu wa Mipango ya Nchi. Aidha, sheria itakayohuishwa iipe Tume nafasi ya kujenga uwezo wake (*capacity building*), iwe na uwezo wa kifedha, na ipate wataalam wengi na wa kutosha. Tume itakapopata nguvu zaidi itaondoa hisia ya utendaji kazi kama *kawaida* (*business as usual*). Ni lazima Tume kupitia Serikali iwezeshwe ili itekeleze kikamilifu wajibu wake kama *think tank* na isukume utekelezaji wa Mpango huu muhimu. Tume itakumbana na tatizo kubwa la kutokufanya kazi zake kwa tija na ufanisi kama uhuishaji wa sheria husika hautafanyika.

Mheshimiwa Spika, hoja inayojengwa na Kamati ni kuwa baada ya kuandaan Mpango huu, sasa umefika wakati kwa Wizara zote na Taasisi za Serikali kupata maelekezo muhimu ya utekelezaji wa mipango kutoka Tume ya Mipango badala ya kutekeleza mipango kwa kadiri wanavyoona wao. Nchi nyingi kama China na India zimefanikiwa kuwa na nguvu kubwa ya uchumi kwa kuwa na Tume za Mipango zenye nguvu kubwa ya ushawishi wa mipango na utekelezaji pamoja na kupewa kipaumbele kwenye maamuzi ya kiuchumi. Aidha, Wizara na Taasisi za Serikali zishirikiane na Tume hii ipasavyo ili kuhakikisha inatimiza malengo yake iliyojiwekea na kuhakikisha inakuza uchumi na kupunguza umaskini. Hili litawezekana kwa Tume kupewa nguvu hii kisheria.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nchi nyingi zinazoendelea kuandaan mipango mizuri, tatizo ambalo Kamati ina uzoefu nalo ni lile la uandaaji wa mipango mizuri ya Serikali lakini utekelezaji wa Mipango hiyo wake huwa ni hafifu. Kamati inaishauri Serikali ili kuepukana na tatizo hili na kuathiri mpango huu, taratibu za usimamizi na utekelezaji ziimarishe kwa kuzingatia yafuatayo:-

Kwanza, ushirikiano kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha uimarishwe zaidi kuliko hivi sasa. Wizara hizi mbili ni lazima ziimarishe utaratibu wa uratibu wa Miradi ya Kimkakati ya Taifa ya Wizara, Mikoa na Halmashauri za Wilaya ili malengo na matokeo yanayotarajiwa yasimamiwe na kutekelezwa kikamilifu katika ngazi hizi husika.

Pili, Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha ziendelee kubuni mbinu mbadala za kujiiondoa katika utegemezi mkubwa wa kuibua mapato ya ndani kwa kutegemea vyanzo vya kodi ya ndani pekee yake (*tax revenue*), badala yake ziangalie vyanzo vingine visivyo vya kodi (*non tax revenue*) vitakavyosaidia kugharamia Mpango huu kwa kiwango kikubwa. Utegemezi wa kodi za ndani pekee hautakidhi malengo ya utekelezaji wa tija.

Tatu, Wizara hizi mbili zihakikishe kuwa zinashirikiana kikamilifu katika utengenezaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti (*Planning and Budget Guidelines*) kulingana na misingi na malengo ya mpango huu.

Nne, Wizara hizi mbili zihakikishe kuwa Bajeti inawiana na mipango itakayopangwa kila mwaka. Hili litawezekana kwa kuanzisha Kamati ya Pamoja (*Joint Committee*).

Tano, Kamati hii ya pamoja ihakikishe kuwa wakipitisha mawasilisho ya Bajeti za Wizara, ziendane na mipango iliyokusudiwa. Mantiki ya utaratibu huu ni kuondoa pengo la utendaji (*disjoint*) kati ya Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha ili kuimarishe utendaji, ufuatiliaji na utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano ulioandaliwa.

Sita, Tume ya Mipango ikishirikiana na Wizara ya Fedha zijenge mawasiliano na Wizara zote hasa zile za kipaumbele ili kufuatilia na kutathmini (*monitoring and evaluation*) kila baada ya hatua ya utekelezaji wa Mpango uliofikiwa na Wizara husika. Uimarishaji wa kutoa na kupata taarifa utaboresha kwa kiwango cha juu shughuli za uratibu zitakazofanywa na Tume kwa uchumi na mipango ya nchi.

Mheshimiwa Spika, hatua za kuimarishe na kujenga Taasisi ya Mipango (*Institutional strengthning*) ni hitajio muhimu katika kusimamia na kutekeleza Mpango huu wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa Mpango huu utakuwa wa gharama kubwa. Mpango utagharimu shilingi trilioni 42.9 kwa wastani wa shilingi trilioni 8.6 kwa mwaka. Kati ya kiasi hiki, Serikali itatafuta Shilingi trilioni 2.6 kila mwaka. Kamati inaishauri Serikali ili kufanikisha mpango huu ni lazima ibadilishe utaratibu wake na kufanya yafuatayo:-

Kwanza, ipo haja ya kupanua wigo wake wa mapato, Serikali imekuwa ikitegemea sana vyanzo vya kodi kuamsha mapato yake (*Tax revenue*). Utekelezaji huu wa kukusanya mapato kutegemea *tax revenue*, bila ya kupanua wigo wa kodi, umepelekea Serikali kubuni vyanzo vingi vya kodi na utitiri wa tozo ambazo nyingine zinakuwa kodi/tozo zenye kero (*nuisance taxes/levies*). Kodi nyingi zinadumaza ari za uzalishaji, ujasiriamali na uwekezaji. Aidha, kodi nyingi na ndogo ndogo zinashawishi ukwepaji wa kodi na kutolipa kodi. Hali hii itashusha viwango vya mapato ya Serikali. Upo umuhimu sasa kwa Serikali kubuni na kuimarishe mikakati yake ya kuibua vyanzo vingi vya mapato visivyo vya kodi (*non – tax revenue*) pamoja na vyanzo vingine. Kwa mfano, katika kipindi cha Julai, 2010 hadi Machi, 2011 mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 4,256.3 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3,910.3 ni mapato ya kodi, wakati shilingi bilioni 227.4 ni mapato yasiyo ya kodi. Hiki ni kiwango kidogo sana na hivyo kupunguza kasi ya mpango huu kutegemea fedha za wahisani.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni kupata mapato kuitia *PPP's* na Sekta Binafsi. Haya yanahitaji hatua za dhati na za haraka za kupunguza gharama za biashara (*cost of doing business*) *eneo* ambalo bado ni kikwazo. Bado yapo matatizo ya urasimu, kuchelewa kutoa maamuzi, Sheria zilizopitwa na wakati pamoja na miundombinu haffifu. Sekta Binafsi na *PPPs* zinapata uzito wa kuchangia maendeleo kwa kujihusisha katika miradi kwenye mazingira haya. Ipo haja ya kuboresha mazingira ya utekelezaji ili kuvutia taasisi hizi kuchangia fedha katika utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano, yumkini hata vyanzo vingine mbadala vilivyopendekezwa kwa mfano kodi kwenye biashara za kifedha, *sovereign Bonds*, kodi kutoka makampuni makubwa, yote hii inategemea mazingira mazuri ya uwekezaji katika nchi. Uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara liwe ni zoezi la dharura na la haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini kuwa Mpango huu utatekelezwa vizuri kama utazingatia kwa karibu mfumo wa idadi ya watu nchini. Takwimu zinaonyesha kuwa asilimia 44.4 ya watu wote ni wenye umri chini ya miaka 15. Idadi ya wenye umri kati ya miaka 15 - 24 wanakadiriwa kuwa 8,580,351 sawa na asilimia 19.9 ya watu wote. Hivyo, asilimia 64.3 hivi, ni vijana. Aidha, inakadiriwa kuwa wanafunzi wa shule hivi sasa wamefikia zaidi ya takribani 11,000,000. Shule za msingi milioni 8.6, Sekondari milioni 1.4 na Vyuo Vikuu milioni 1.0. Mpango wa miaka mitano unahitajiwa kuzingatia hali hii kwa maana zifuatazo:-

Kwanza, kuhakikisha elimu tunayotoa inawezesha kujenga jamii tunayotaka, yenye tija na stadi. Pili, takribani, vijana milioni mbili wanamaliza shule kila mwaka na wanaopata ajira ni robo na karibu robo tatu hawajui la kufanya. Changamoto ni kuwa Mpango ni lazima ulenge katika kujenga seti za *stadi (skills set)* ambazo zinahitajika na zitadumu kwa kipindi cha Mpango mzima. Tatizo la ajira ni kubwa na ni changamoto kwa Mpango tulionao. Ipo haja ya Mpango huu kuwawezesha vijana, nguvu ya Taifa wawe wabunifu na wajuzi ili watekeleze wajibu wao kama Wadau katika kuchangia kujenga uchumi wa nchi.

Tatu, mikakati ya uwezeshaji vile vile ilenge kuwajenga watu 31,809,808 au asilimia 73.7 ya Watanzania wote wanaoishi vijijini wakitegemea kilimo, ufugaji na uvuvi. Mpango utambue kuwa hizi ndizo sekta za wananchi. Kilimo kwa ujumla wake, kama kipaumbele kipewe msukumo mkubwa. Hivi sasa ukuaji wa Sekta ya Kilimo umedumaa. Ipo haja ya kusisitiza maendeleo vijijini kupitia uboreshaji wa miundombinu ya umeme vijijini, uboreshaji wa barabara vijijini, uboreshaji wa maji safi na salama vijijini pamoja na huduma za kifedha na mikopo na uboreshaji wa masoko. Kutokana na hali hii, Mpango hauna budi kuonyesha raslimali za kiuchumi za nchi ki-mkoa ili tujue tuna nini, na tufanye nini.

Pamoja na uwezeshaji wa jumla, Kamati inashauri, kama Mpango ulivyoonesha, ujielekeze katika kusaidia walemvu. Rasimu ya Mpango kutoka ukurasa 148 -160 inayozungumzia Wizara ya Afya, hakuna *specific intervention* inayowagusa Walemvu. Wapo walemvu moja kwa Sita (1/6) ya idadi ya Watanzania wote, mpango lazima uangalie eneo hili.

Nne, Huduma za kifedha ziboreshwwe toka ngazi ya Taifa hadi ngazi za chini (*financial intermediation*). Utaratibu huu utasaidia Mpango kuweshera kila mwananchi kushiriki kuutekeleza na Wadau wengine kutimiza wajibu wao. Mpango ulenge katika mkakati wa kujenga/kutengeneza ajira na kuzalisha mapato (*Employment Creation and income Generation*). Changamoto ni kuwa wakulima bado hawajanufaika na huduma za kibenki. Takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia 14 tu ya Watanzania wote ndio wanaopata huduma za kibenki (mikopo). Hali hii haichochei uzalishaji wa kutosha katika Mpango.

Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme bado inaendelea kuwa ni kikwazo kikubwa katika kuleta maendeleo ya nchi hususan kutokana na uhaba wa nishati hii. Kamati

inadhani Mpango wa miaka mitano umeweka malengo barabara (*ambitions targets*) kwamba katika kipindi cha Mpango tutazalisha MW 2870.

Swali ni kuwa, kwa utaratibu gani? Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita nchi imejenga mradi mpya wa MW 145 tu. Mantiki ya hali hii inaashiria kuwa sekta binafsi ihamasishwe kuwekeza katika uzalishaji wa umeme na mkakati huo ukiambatana na uboreshaji wa mazingira yatakayotoa msukumo wa uwekezaji (*investment drive*). Mipango ambayo hivi sasa iko tayari ianze kutekelezwa. Kwa kuzingatia umakini (*seriousness*), mradi wa Kiwira unaweza kuzalisha MW 200 katika kipindi kifupi kijacho. Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) liko tayari kuzalisha MW 300 Mchuchuma. Serikali itoe maamuzi miradi hii na mingine itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, moja ya lengo la Mpango ni kubadili muundo wa uchangiaji wa Pato la Taifa ili mchango mkubwa utokane na viwanda badala ya kutegemea kilimo. Bila ya mikakati ya makusudi, azma hii ya kubadili sekta ya Viwanda kuwa mchangiaji mkubwa wa uchumi (*sectoral shift*) haitawezekana tukiendelea na kasi ya uzalishaji, usafirishaji na ugavi wa umeme tulionao hivi sasa. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuendeleza haraka vyanzo mbadala vya umeme kutoka kutegemea sana maji, na kuendeleza umeme unaotokana na makaa ya mawe, jua, upepo na kadhalika. Nchi ilenge kuwa na akiba ya umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kujielekeza katika suala la uwiano wa maendeleo wa maeneo katika nchi. Bado lipo tatizo la maendeleo yasiyowiana baina ya maeneo na maeneo na hivyo kuleta tofauti kubwa za kiuchumi na uwekezaji, yaani maendeleo (*regional economic and investment disparities*). Mwelekeo huu sio tu kwamba unadumaza maendeleo ya Mikoa kadhaa, ikilinganishwa na Mikoa mingine, bali vile vile inachochea umasikini. Mpango ni budi ujibu tatizo hili kupitia uelekezaji wa raslimali katika yale maeneo yasiyo na maendeleo. Hatua hii pia itapunguza malalamiko baina ya watu, katika nchi moja. Ni kweli misingi ya kiuchumi inahitaji maendeleo kuelekea katika maeneo yaliyokwisha piga hatua za maendeleo, lakini masuala ya usawa (*equity issues*) lazima yawe ni kigezo muhimu kwa Mpango mzuri.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa miaka mitano usiwe *top-down* peke yake, kama utakuwa na vipengele vya *bottom-up* utaweza kugusa utajiri wa maeneo husika na hapo hapo kubuni mikakati ya kutumia raslimali hizo na kuwekwa kwenye Mpango wa Taifa. Ipo haja ya Mpango kubuni utaratibu wa kuhuishwa na kufanyiwa mapitio ya mara kwa mara ili kuepuka kuyaacha maeneo ambayo ni muhimu katika kuendeleza masuala ya usawa na uwiano wa maendeleo (*equity issues*).

Mheshimiwa Spika, Mpango huu kama ilivyoonyeshwa awali, ni Mpango wa kitaifa na unahusisha kila mwananchi, vijana, sekta binafsi, Serikali katika kuboresha mazingira wezeshi na raslimali, Bunge na Taasisi za Elimu ya Juu, utafiti na AZISE. Ili kutekeleza kwa ufanisi Mpango huu, ni lazima tujenge utamaduni wa nidhamu na kuitekeleza (*discipline and enforcement*) pamoja na uwekezaji. Suala la kila mtu katika ngazi husika kufanya kazi kwa bidii linabakia kuwa la msingi.

Nidhamu ni lazima iendane na uaminifu na uadilifu ambavyo ni vigezo vya lazima katika kuleta tija baina ya wadau wote. Yote haya yatapata nguvu kutokana na kubadili mtazamo wetu hususan wa kudhania kuwa Serikali itatutekelezea na kutupa kila kitu. Hali hii inabidi tuibadilishe (*change of mentality*). Ubunifu wa kila mwananchi ni muhimu katika kuibua mapato kupitia kufanya kazi kwa bidii. Hata hivyo, kwa kauli mbiu ya kuibua fursa zilizofichika za kukuza uchumi wa Tanzania, ni lazima iambatane na mihami, nidhamu, umakini na nguvu kubwa ya Serikali ya kuusukuma Mpango tajwa.

Mheshimiwa Spika, uzoefu umetuonyesha kuwa mitikisiko ya uchumi nchini na duniani, inaathiri sana mwenendo wa kukuza uchumi wetu. Kudorora kwa uchumi duniani na matatizo ya kifedha yaliyojitokeza, yanatufundisha kuwa siasa sasa siyo uchumi bali uchumi ndiyo siasa. Kamati inashauri kuwa Serikali itakapoimarisha uchumi wake hata eneo la siasa litaendelea vyema. Ukosefu wa ajira, kupanda kwa gharama za maisha, ukosefu wa mapato ya kutosha uhaba wa umeme, vyote, suluhisho na ufumbuzi wake ni uchumi ulio imara. Hali hii ni changamoto kwa Mpango huu wa miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, nguvu zote zielekezwe kwenye kuimarissha uchumi. Uchumi utakapoimarika wananchi wakiwa wadau na tukiendelea kuimarissha usalama na utulivu pamoja na uzalendo, nchi itapiga hatua kubwa ya maendeleo. Uchumi utakapoimarika, tutazungizia mikakati ya kuvutia uwekezaji.

Tutaweza kushughulikia amani na usalama na hivyo kuweza kutekeleza mipango yetu hasa ikizingatiwa kuwa Mpango pia unahitaji ushiriki wa wahisani katika utekelezaji wake. Dhana hii ni ya msingi kuhakikisha mafanikio ya Mpango tunaoujadili. Uchumi ni siasa. Aidha, utekelezaji wa Mpango huu utapata mafanikio kupitia uimarisshaji wa Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Mpango wa Miaka Mitano utahitaji kuwekewa taratibu za kuhakikisha utekelezaji wake, Kamati inashauri kuwa yale maeneo muhimu yanayogusa wananchi walio wengi hususan vijana na akina mama, yanasisitizwa katika taratibu hizo:-

- (a) Mpango lazima usaidie vijana kwa kuwapa mazingira wezeshi na uwezeshaji wa kutumia ubunifu na nguvu kazi yao;
- (b) Mpango lazima usaidie na utoe msisitizo katika kusaidia shughuli za wanawake hususan zile za kiuchumi na jamii hasa ikizingatiwa kuwa wanawake ndio wazalishaji wakubwa hasa katika sekta za kilimo na ufugaji; na
- (c) Mpango kwa makusudi ulenge katika kuboresha sekta za wananchi, kilimo, ufugaji na uvuvi.

Kimsingi Mpango utatekelezwa ikiwa urasimu utaondolewa na maamuzi kufanyika kwa haraka na wakati. Mpango utafanikiwa ukieleweka na kila mdau atimiza wajibu wake. Ili Mpango huu utekelezwe kwa tija na ufanisi, utahitaji msukumo mkubwa

kutoka Serikalini pamoja na kuondoa vikwazo vyta utekelezaji kama vilivyobainishwa katika Mpango.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia kwa kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya na ushirikiano wao walionipa. Naomba nitumie fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Abdallah Omari Kigoda, Mwenyekiti na Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Maulidah Anna Valerian Komu, Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mheshimiwa Devotha Mkuwa Likokola, Mheshimiwa Martha J. Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amour Amina Abdulla, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Makamu Mwenyekiti, kwa kunisaidia kuiongoza Kamati, Mheshimiwa Steven Masato Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Dr. Philip Isdor Mpango, Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango. Aidha, naomba niwashukuru Watendaji Wakuu wa Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Tume ya Mipango, kwa kuandaa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia miongozo na maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge, Dr. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mwisho, nashukuru kwa ushirikiano mkubwa ninaoupata kutoka kwa wananchi wa Jimbo la Handeni, kwa kazi tunazozifanya za kuleta maendeleo katika maeneo yetu. Ujumbe wangu ni uleule, mambo mazuri hayataki haraka.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kuidhinisha Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12-2015/16) ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2025 kama alivyowasilisha mtoha hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante kwa uwasilishaji mzuri. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu hoja hii, Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse.

MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE – MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU: Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7) Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani wakiongozwa na Kiongozi wetu wa Kambi, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Naibu wake, Mheshimiwa Zitto Kabwe, Waheshimiwa viongozi wengine pamoja na Wabunge wote wa Kambi yetu, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kuwalilisha na kutetea maslahi ya wananchi walionituma.

Mheshimiwa Spika, kwa uzito huohuo, nakishukuru Chama changu, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) pamoja na wapigakura wa Jimbo la Karatu kwa imani, heshima na wajibu mkubwa walionipa wa kunifanya kuwa mwakilishi wao. Naahidi nitaendelea kuwa nao pamoja na Watanzania wote kwa ujumla katika kusukuma mbele maendeleo ya Taifa letu. Hakika, sitawaangusha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika shukrani zangu lakini kwa umuhimu mkubwa, nakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Kamati zote, kwa kazi mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili. Mungu azidi kuwatia busara na hekima katika kutekeleza wajibu wenu huo kwa haki na usawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuwasilisha masikitiko ya Kambi ya Upinzani kuhusiana na mpango huu. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 63 (3)(c) inasema kuwa majukumu ya Bunge ni:-

“kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu au wa muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa katika Jamhuri ya Muungano, na kutunga sheria ya kusimamia utekelezaji wa Mpango huo”.

Wakati Ibara ya Katiba ikitamka hivyo, Mpango huu tayari ulishasainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania tangu tarehe 7 Juni 2011 na kuwasilishwa Bungeni tarehe 8 Juni kama Hati ya Kuwasilisha Mezani, bila kuelezwaa ndani ya Mpango wenyewe kama kilichowasilishwa ni rasimu. Aidha, kwa mujibu wa mpango wenyewe, Rais ameshashukuru wadau kwa maoni yao yaliyowezesha kukamilisha Mpango na ameshalishukuru Bunge kwa mchango katika kukamilisha Mpango husika.

Mheshimiwa Spika, wakati Rais akisema hivyo, Kambi ya Upinzani haijawahi kushirikishwa wala kushiriki kikao chochote cha Bunge kilichojadili na kupitisha

Mpango huu. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri aeleze ni kikao kipi cha Bunge na ni Mkutano wa ngapi wa Bunge, uliowahi kujadili na kupitisha Mpango huu wa Maendeleo na hata kumpelekea Mheshimiwa Rais kulishukuru Bunge kupitia dibaji yake iliyochapwa kwenye Kitabu cha Mpango huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inalitaka Bunge lifanye kazi zake kikamilifu na Serikali iwe na utamaduni wa kuheshimu hilo. Tunaitaka Serikali isiwe na utamaduni wa kuamini kuwa kila jambo litakalowasilishwa hapa Bungeni basi Bunge italipitisha tu. Tunaitaka Serikali kuhakikisha kuwa maoni ya Wabunge yanazingatiwa na kuingizwa kwenye Mpango huu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni kuhusiana na lugha ambayo imetumika katika kuuandaa Mpango huu. Huu ni Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa miaka mitano ijayo ila haulengi kufikishwa kwa Watanzania ambao wanapaswa kuutekeleza, kwani lugha iliyotumika haifahamiki kwa zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wote. Tunapenda kuikumbusha Serikali kuwa hakuna Taifa lolote hapa ulimwenguni lililowahi kuendelea kwa kutumia lugha ya kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali baada ya Mpango huu kujadiliwa na kupitishwa na Bunge basi uandikwe kwa lugha ya Kiswahili na usambazwe kwa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao kama Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa, Vitongoji, Madiwani na Wabunge ili waweze kupanga mipango yao ya maendeleo kulingana na mpango huu. Kila mwenye kuidhinisha maamuzi anapaswa kuhakikisha kuwa maamuzi yake yanaendana na Mpango wa Taifa wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni kuwa, pamoja na Mpango huu kuwa na mikakati na malengo katika vipaumbele mahsus, Mpango huu hauna shabaha za ujumla za kutuwezesha kujipima kama Taifa kuhusu mafanikio tunayotegemea kuyafikia baada ya kutekeleza Mpango huu.

Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa baadhi ya shabaha kuu za mpango huu ziwe kama ifuatavyo:-

- (i) Kupunguza umasikini vijijini kutoka asilimia 37% ya sasa na kufikia asilimia 20%.
- (ii) Kumaliza tatizo la umeme kabisa na kuzalisha umeme wa ziada kwa asilimia 20%.
- (iii) Kuwa Taifa linalozalisha gesi kwa wingi barani Afrika.
- (iv) Kuhakikisha kuwa asilimia 80% ya Watanzania wanapata maji safi na salama.
- (v) Kuhakikisha kuwa barabara za vijijini zinapitika kwa wakati wote wa mwaka.

(vi) Kupunguza vifo vya akina mama na watoto.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Maendeleo wa 2011/2012 -2015/2016. Upembuzi wa kina uliofanywa na Kambi ya Upinzani, umebaini kuwepo kwa upungufu mwingi na dosari kadhaa nzito zinazoweza kuathiri utekelezaji wake au kukwama kabisa. Mipango ya aina hii si mipyä katika nchi yetu, tumeshakuwa na Mipango ya Maendeleo ya miaka mitano-mitano tangu mwanzoni mwa miaka ya 60, lakini hatimaye mingi ilisusua au kukwama kabisa kwa sababu mbalimbali, kubwa ikiwa ni kutokuwepo kwa uwajibikaji wa kutosha ndani na baina ya Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mionganî mwa mahitaji muhimu ya Taifa letu ni hitaji la Katiba Mpya, wananchi wanachotaka ni kuanza mapema kwa mchakato shirikishi wa kuandikwa kwa Katiba Mpya ili wapate haki ya kuweka mifumo thabiti ya kusimamia uwajibikaji wa utawala kwa umma. Kambi ya Upinzani, imeshangazwa na Mpango huu wa Maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 - 2015/2016) kutolipa kipaumbele hata kidogo hitaji la Katiba Mpya wala kutenga fedha maalum kwa ajili ya mchakato huo nyeti, katika kuamua hatma mpya ya mwelekeo wa Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nguzo kuu ya utekelezaji wa mipango na malengo yote mazuri ni uwepo wa utawala bora na wenye kuwajibika kikamilifu. Kambi ya Upinzani inatambua kuwa Mpango huu umetenga fedha kwa ajili ya kuimarisha mifumo ya kisheria na kitaasisi ili kuchochaea demokrasia, utawala wa sheria na utawala bora kwa kufanya mambo yafuatayo:-

- (i) Kuzijengea uwezo wa kiutendaji Taasisi za Kiserikali na watendaji wake.
- (ii) Kukabiliana na tatizo la rushwa,
- (iii) Kuchochaea uwazi, uwajibikaji na maadili kwa Watumishi wa Umma.
- (iv) Kukamilisha mradi wote wa mfumo wa Vitambulisho vya Taifa na kuhakikisha vinatumika ifikapo mwaka 2015.
- (v) Kuchochaea ushiriki mpana wa wananchi na usawa wa kijinsia katika utekelezaji wa mpango wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli zote hizo zilizoainishwa kwa ajili ya kuboresha uongozi bora na utawala wa sheria, kama moja ya mikakati ya utekelezaji wa Mpango wenyewe, bado Kambi ya Upinzani inaona kuwa mchakato wa Katiba Mpya ulipaswa kupewa uzito mkubwa kwa upekee wake, kama nguzo kuu ya maboresho yote ya ndani ya mfumo wa utawala yanayokusudiwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, hata kama Serikali itasema kuwa kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya Tume ya Kurekebisha Sheria kiasi cha shilingi 945 milioni, bado Kambi ya Upinzani inataka kuona fedha za kugharamia mchakato wa Katiba Mpya zikitengwa na

kuonyeshwa waziwazi. Kwa mujibu wa maelezo ya Mpango huu, fedha hizo za kurekebisha sheria zinatarajiwa kutoka nje ya nchi. Kambi ya Upinzani inaona ni aibu kubwa kwa Taifa kufikia hatua ya kuomba fedha za kurekebisha sheria kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo la umaskini na mwelekeo wa Mpango. Moja ya matatizo makubwa ya kiuchumi yanayoikabili nchi yetu katika zama hizi, ni kuwa na uchumi mpana (*macro-economy*) unaokua bila kupunguza umaskini wala kuwanufaisha wananchi walio wengi. Katika kipindi cha mwaka 2001 – 2010, uchumi wetu umekuwa ukikua kwa wastani wa asilimia saba. Kwa mfano, kipimo cha umaskini (*Head Count Index*) kinaonesha kuwa umaskini ulipungua kidogo sana kutoka asilimia 35.7 mwaka 2001 hadi kufikia asilimia 33.6 mwaka 2007, ingawa uchumi umeelezwa kuwa ulikua kwa wastani wa asilimia 7.1 ndani ya kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo hilo la uchumi kukua huku umaskini ukiendelea, Mpango huu umeeleza kuwa utajikita katika kutekeleza nadharia kuu mbili. Mosi, ni kuvutia uwekezaji mkubwa, hususan kuitia maeneo au sekta zinazogusa zaidi maskini na pili, kudumisha na kuendeleza ukuaji wa uchumi mpana kwa kuhakikisha Pato la Taifa linakua kwa wastani wa asilimia nane kwa miaka mitano ijayo na kwamba Mpango utakaofuatia utaiwezesha nchi kulenga ukuaji wa Pato la Taifa kwa wastani wa takribani asilimia 10 kuanzia mwaka 2016 hadi 2025.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shabaha hizo, Kambi ya Upinzani inaona kuwa Mpango huu umeshindwa kuweka bayana jinsi utakavyoinua uchumi wa vijijini (*rural economic growth*), ambao kimsingi ndio utakaoweza kupunguza moja kwa moja umaskini wa wananchi walio wengi. Mpango umejikita katika kushughulikia vipaumbele vilivyoainishwa kwa ujumla wake kwa kuanzia juu kwenda chini.

Mheshimiwa Spika, Mpango umetenga fedha za utekelezaji wa vipaumbele kadhaa vya kisekta kwa ujumla wake, lakini haujaweka mfumo mzuri wa mgawanyo wa rasilimali za kimaendeleo kati ya Halmashauri na Serikali Kuu, jambo ambalo kwa muda mrefu limekuwa ni changamoto katika utekelezaji wa mipango na mikakati mingi ya kimaendeleo, hivyo kusababisha mikakati hiyo kukwama inapofikia kwenye utekelezaji wake. Kambi ya Upinzani inaelewa kuwa pamoja na machapisho na maandiko mazuri ya Mpango wenye we kisoro kubwa ni kuwa yanatayarishiwa Dar es Salaam maofisini na kuwanyima wananchi fursa katika kuumiliki Mpango huu ili waweze kuutekeleza kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) kama lilivyo jina na malengo yake, unapaswa kuanza kufanyiwa utekelezaji kwa kutengewa fedha za bajeti kuanza mwaka wa fedha wa 2011/2012, ili ifikapo mwaka 2016 uwe umetimiza miaka mitano. Ukurasa wa 72 wa Kitabu cha Mpango huu (chapisho la Kiingereza) unaonesha kuitia jedwali lililopo, kuwa zinahitajika jumla ya shilingi trilioni 8.2 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 tunaokwenda kuuanza siku si nyingi.

Mheshimiwa Spika, wakati utekelezaji wa Mpango huu ukiwa umepangwa kuanza mwaka wa fedha wa 2011/2012, mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2011/2012 yaliyowasilishwa na Waziri wa Fedha wiki iliyopita, yanaonesha kuwa hakuna fedha zilizotengwa za jumla ya Shilingi trilioni 8.2 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu kwa mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jumla ya bajeti yote inayopendekezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2011/2012, ni Shilingi trilioni 13.5. Katika hizo, fedha za Matumizi ya Kawaida ni Shilingi trilioni 8.6 na Matumizi ya Maendeleo yametengewa Shilingi trilioni 4.9. Hata kama fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo (Sh. trilioni 4.9) zitashughulikia pia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo kama vilivyowekwa, bado utekelezaji wa Mpango huu kwa mwaka wa fedha 2011/2012 utakuwa umepungukiwa Shilingi trilioni 3.7, sawa na upungufu wa asilimia 43% ya fedha zote zinazohitajika kwa Mpango huu kuanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mahesabu hayo ya kibajeti, utekelezaji wa Mpango huu utakwama kwa asilimia 43 katika mwaka wa kwanza wa kuanza kwake. Kauli kwamba, mwaka wa fedha wa 2011/2012 utakuwa ni kipindi cha mpito katika utekelezaji wa Mpango huu, haina mashiko kwa Taifa. Kambi ya Upinzani inaona kuwa kufanya hivyo ni kupoteza muda wa utekelezaji ambao tayari umo ndani ya Mpango wenye - kwamba utatekelezwa kwa miaka mitano na sio miaka minne. Hii ni dalili kuwa Mpango huu umeanza kufeli kabla hata ya kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imebaini kuwapo dosari kadhaa kuhusiana na gharama zilizokadiriwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango huu wa miaka mitano. Moja ya dosari hizo ni gharama za jumla za kutekeleza Mpango huu ambazo ni Shilingi trilioni 42.98, kutowiana na uwezo halisi wa Serikali kujipatia mapato yake. Ili Mpango huu utekelezek, Serikali itapaswa kuwa na Bajeti ya Maendeleo inayozidi au isiyopungua Shilingi trilioni 8.6 kila mwaka ndani ya kipindi chote cha miaka mitano cha utekelezaji wa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali ikipaswa kuwa na Shilingi trilioni 8.6 za Maendeleo kila mwaka ili kutekeleza Mpango huu, uzoefu unaonesha kuwa imekuwa vigumu kwa Serikali kuweza kukusanya fedha za kutosha ili Bajeti ya Maendeleo iwe kubwa. Kambi ya Upinzani inahoji ni miujiza gani ambayo Serikali hii (yenye uwezo mdogo wa kukusanya mapato) itafanya hadi kuwa na Bajeti ya Maendeleo ya Shilingi trilioni 8.6, ikiwa imekuwa ikishindwa kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ipo mipango mingi ambayo ilikwishapangwa lakini haikuonesha matokeo ambayo yalitarajiwa, kwa mfano ni utekelazaji wa MKUKUTA I ambapo ni programu ambayo hata ushirikishwaji wa wananchi ulikuwa ni mdogo sana na hivyo kutojenga msingi na matarajio yaliyokuwa yakitegemewa. Kambi ya Upinzani, inahoji ni kwa kiasi gani wananchi wameshirikishwa kwenye kutayarisha na kuandaa Mpango huu? Au tumeendelea na utamaduni wa kutowashirikisha wananchi katika hatua za matayarisho na badala yake tunataka washiriki kwenye utekelezaji? Mipango mingi

inakwama kwa sababu wananchi wanaachwa kwenye hatua za utayarishaji na hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, fedha zinazotarajiwa kutumika ni kiasi kikubwa sana kuliko vyanzo vya mapato vilivyoainishwa. Jumla ya fedha zinazotarajiwa kutumika ni shilingi trilioni 42.9 fedha za Kitanzania, ambapo kati ya hizo, Serikali inategemea kuchangia kiasi cha shilingi trilioni 7.8 tu. Kwa uwezo wa sasa wa Serikali wa kukusanya mapato yake na fedha zinazotengwa kwenye Miradi ya Maendeleo ni vigumu sana kufika lengo hilo kwa muda uliowekwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inahoji, je, nakisi hii ya mapato itazibwa na vyanzo gani vya uhakika vya kuuwezesha Mpango huu kutekelezeka ili tusiendelee kuwa mabingwa wa kutengeneza mipango mizuri inayoishia kufungiwa kwenye makabati ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukisoma Mpango huu utaona kuwa hakuna ufanuzi wa Wadau wa Maendeleo ambaa Serikali imewaainisha kuwa watachangia katika kutekeleza Mpango huu. Hili litaleta shida ikiwa wadau wengi watashindwa kutekeleza ahadi zao au kutekeleza wakiwa wamechelewa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka bayana orodha ya wadau ambaa wameonesha nia ya kuuchangia Mpango huu ili wajulikane na kiasi cha ahadi walizoahidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona haja ya Mpango huu kutekelezwa kuanzia ngazi ya Halmashauri huku jukumu la Serikali Kuu likibakia kuwa ni la kuratibu utekelezaji. Kwa kufanya hivyo, utekelezaji wa Mpango huu utaweza kugusa wananchi moja kwa moja kuliko kuweka mamlaka ya utekelezaji kwenye ngazi ya Serikali Kuu pekee. Utekelezaji wa ushauri wetu huu utaufanya ile dhana nzima ya Serikali ya ugatuaji wa madaraka itekelezeké.

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2009/2010 inaeleza kuwa Deni la Taifa limeongezeka kwa asilimia 38%. Kambi ya Upinzani imestushwa na hali hii kwani kwa mujibu wa taarifa za Serikali, hadi kufikia Disemba 2010, Deni la Taifa lilikuwa limefikia dola milioni 11,948.0 ambazo ni sawa na zaidi ya shilingi trilioni 17 za Kitanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, malipo ya Deni la Taifa katika kipindi cha robo tatu ya mwaka ulioishia Machi 2011 yalikuwa shilingi bilioni 803.64. Malipo ya deni la nje kwa kipindi hicho yalikuwa shilingi 73.66 bilioni na kat i ya hizo shilingi 29.06 zilikuwa ni malipo ya mtaji na shilingi bilioni 44.6 zilikuwa ni malipo ya riba. Swali la kujiuliza hapa ni, je ikiwa tunalipa riba kubwa kiasi hicho, yako wapi masharti nafuu ambayo Serikali mara zote imekuwa ikiyasema?

Mheshimiwa Spika, hali hii ya kulipa riba kubwa ipo pia kwenye ulipaji wa madeni ya ndani, kwani kwa kipindi hicho hicho kinachoishia mwezi machi 2011, deni la ndani lilipiwa kiasi cha shilingi 730.3 bilioni na kat i ya hizo, shilingi bilioni 556.7

zilitumika kulipia dhamana za Serikali zilizoiva na riba ilikuwa jumla ya shilingi 173.6 bilioni. Kambi ya Upinzani, inashauri kuwa huu ni wakati muafaka wa kuhakikisha kuwa inatungwa sheria itakayoliwezesha Bunge kuidhinisha mikopo yote ambayo Serikali inakopa kwenye taasisi za ndani na nje ya nchi. Hii itasaidia kupata taarifa juu ya lengo la mikopo hiyo na itadhibiti kuhakikisha kuwa tunakopa kwa ajili ya Maendeleo na sio vinginevyo. Huu ndio utakuwa wajibu wa Bunge katika kuisimamia Serikali kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei umezidi kuongezeka mwaka hadi mwaka huku ukigusa bidhaa muhimu hasa chakula. Serikali bado inasuasua kuchukua hatua thabiti za kuzidbiti hali hiyo. Tusipochukua hatua za kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unadhibiti kikamilifu, utekelezaji wa Mpango huu utakuwa ni ndoto. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza kwa kina kuna mkakati gani wa kudhibiti mfumuko wa bei hapa nchini, hasa ikitiliwa maanani kuwa mfumuko huu kwa kiasi kikubwa umesababishwa na kupanda bei kwa bidhaa za nishati hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, thamani ya shilingi yetu kwa mwaka 2010 ilishuka kwa asilimia 8.5 kulinganisha na dola ya Kimarekani. Ili kutekeleza Mpango huu na kufikia lengo la kutumia shilingi trilioni 8.2 kwa mwaka wa kwanza, tutajikuta katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango huu unafika kiasi cha fedha kinachotarajiwa kitakuwa sio Shilingi trilioni 9.1 tena kama kilivyopangwa sasa. Hii itavuruga kabisa utekelezaji wa Mpango huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ileze kwa kina ina mikakati gani ya kukabiliana na kushuka kwa thamani ya shilingi ya nchi ili kuhakikisha kuwa Mpango huu unatekelezwa kikamilifu ndani ya miaka mitano kwa makadirio ya fedha yaliyowekwa sasa. Vinginevyo, Mpango huu utakuwa hautekelezeki na tutajikuta tukilazimika kuufanya duruso/mapitio (*review*) ili kuweza kukabiliana na kushuka kwa thamani ya shilingi. Vinginevyo, kiasi cha pesa kilichotengwa kwa utekelezaji wa mpango huu si kiasi halisi kinachoweza kutegemewa katika kuutekeleza Mpango huu, ikiwa anguko hili la thamani ya shilingi litatokea. Tunaitaka Serikali iwe inakokotoa makadirio yake ya thamani ya mipango yake kwa kutumia shilingi za Kitanzania na pia kwa kutumia dola ya kimarekani, ili iwe rahisi kuweza kupima thamani halisi ya mpango kutokana na kushuka kwa thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, uboreshaji rasilimali watu. Mionganoni mwa vipaumbele vya mpango wa maendeleo wa miaka mitano ni uboreshaji wa rasilimali watu. Kwenye hili, mkazo umewekwa kwenye kuboresha shule zilizopo, kujenga nyumba za Walimu na kadhalika. Kambi ya Upinzani inataka Mpango uweke wazi kuwa kipaumbele cha kwanza ni elimu bora ili kuhakikisha kuwa rasilimali watu inaandaliwa kukidhi haja ya kuwa na Taifa lenye watu walioelimika. Hili litaendana sambamba na kuifumua mitaala yetu ya elimu ili ikidhi haja ya wakati uliopo na ujao katika nchi yetu. Tunaitaka Serikali ihakikishe kuwa kama Taifa tunakuwa na mkakati maalum wa kuandaa wataalamu kwenye sekta nyeti katika kukuza uchumi na hasa turejee kwenye utamaduni wetu wa kupeleka vijana wetu nje ya nchi na kuwapatia utalaam kuhusu madini, gesi, mafuta, lugha hasa Kichina, Kihindi, Kihispaniola. Lengo ni kuhakikisha kuwa tunakuwa na

wataalamu wa kutosha na ambao watashiriki moja kwa moja katika kuvuna rasilimali za Taifa letu kwa manufaa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani, inataka Mpango huu uainishe ndani ya miaka mitano tunataka kuwa na wataalamu wangapi na kwenye sekta gani. Hili lifanywe na Balozi zetu kufanya tafiti kwenye nchi ambazo wametumwa kujua ni Vyuo gani vinyavyotoa taaluma adhimu. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali iwe inawatuma vijana wetu kusoma nje na hatimaye kuweza kulikomboa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ni wa miaka mitano, ila haujazingatia popote kuhusiana na changamoto ya kuhakikisha kuwa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinaandalialiwa kikamilifu katika kukabiliana na changamoto mpya na za kisasa. Kambi ya Upinzani, inataka Serikali kuhakikisha kuwa inazingatia katika kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama ili kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo na zijazo ndani ya miaka mitano ya utekelezaji wa mpango huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, namshukuru Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa kuwakilisha taarifa ya Kambi ya Upinzani vizuri. Sasa kwa sababu tunaingia sisi wenyewe kama Kamati ya Mipango, kwa hiyo, itanibidi mimi niondoke hapa nikabadilishe mavazi, nikae hapo, kwa sababu sasa tunakuwa kwenye Kamati ya Mipango lakini ikifika uwakilishi wa Bunge nitarudi tena kuva nguo, nitakuja kuahirisha.

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunayo orodha kubwa sana ya wachangiaji, muda wa kuchangia ni mfupi, kwa hiyo mchangiaji wa kwanza nitamwita Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Freeman Mboge na atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Mpina.

MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba hii muhimu ya Mpango wa Maendeleo. Pili, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali, nimpongeze Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kuleta Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa sababu moja ya mambo ambayo nchi nyingi za Afrika zimeendelea kuwa maskini ni pamoja na kuwa nyuma katika masuala mengi na Mpango huu unaleta ufumbuzi wa masuala hayo. Mpango huu umelenga kutatua matatizo yanayowakabili wananchi na Taifa kwa ujumla kama umeme. Serikali imeleta mapendekezo kwamba ili tufanikiwe kuondoa tatizo la umeme ni lazima tupange na kupanga ni kuchagua, kwa hiyo, Serikali inapendekeza miradi nane. Miradi ya Ubungo, Mtwara, Ruhubi, Mchuchuma, Kiwira, Kinyerezi na Mwanza. Lengo ni kuongeza umeme ule ufike *Megawatt 2780* na tukishafanikiwa pale maana yake

tunaruhusu uwekezaji, tunaruhusu wananchi kupata umeme na mambo mengine yote yanayowezekana. Nadhani hili ni suala zuri lazima tuipongeze Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo limesababisha nchi nyingi za Afrika kuendelea kuwa nyuma ni kutokana na uwekezaji mdogo kwenye maeneo ya Sayansi na Teknolojia. Mpango huu unaweka kipaumbele kuwekeza kwenye Sayansi na Teknolojia na umetenga fedha za kutosha na maana yake ni kwamba tutafanikiwa kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ya tatu ambayo nchi nyingi za Afrika zimeendelea kuwa nyuma kimaendeleo ni katika tatizo zima la mazingira. Mpango huu unaelekeza nguvu zote kuhifadhi vyanzo vyanzo nya maji, kuweka mazingira mazuri na hivyo kuiwezesha Sekta ya Kilimo kuendelea hasa katika umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ambayo inafanya nyingi za Afrika ziwe nyuma kimaendeleo na hasa tuendelee kuwa masikini ni elimu. Mpango huu umeweka mikakati kabambe kwa ajili ya kuendeleza rasilimali watu na vyuo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba nchi nyingi za Afrika tuna matatizo ya njaa na tunapokuwa na njaa huwezi ukawaambia watu wajenge nchi kwa sababu wanahitaji chakula. Mpango huu unaelekeza kuweka chakula cha kutosha cha akiba ili waweze kufanya kazi na tuweze kujenga nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niipongeze Serikali kwamba huu ni Mpango wa watu, ni Mpango wa Taifa, ni Mpango wa Watanzania na ni Mpango wetu sote na ye yote anayewapenda Watanzania na ye yote mwenye nia ya kujenga nchi hii, asaidie utekelezaji wa Mpango huu ili uweze kufanikiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mpango huu kuna mambo ambayo napenda kupata maeleo kidogo. Kulikuwa na *Master Plan* ya TANESCO ambayo ililetwa kwenye Bunge tukaijadili. Ilianisha baadhi ya miradi ambayo haikuchaguliwa katika ile nane hapa. Kwa hiyo, napenda kupata maeleo ni kwa namna gani ile miradi ambayo haimo humu kama ile ya Mto ulioko Makete, Rumakalya utaingizwa vipi na mengine ili kuweza kusaidia kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninayo maoni kwenye sehemu ya rasilimali watu, ukurasa wa 33 - 35 wa hiki kitabu cha *version* ya Kiingereza. Yapo mapendekezo, kwamba Mpango umedhamiria kuona kwamba kunakuwa na wataalamu, kwa mfano kufikia mwaka 2015 tuwe na Wanasyansi 26,000, tuwe na Wahandisi 88,000, tuwe na Wanasyansi wa Elimu ya Viumbe 22,000, tuwe na Madaktari, 64,000 na tuwe na Wanauchumi 30,000 na Walimu 320,000, Mpango unaelezea vilevile mkakati wa kuongeza idadi ya wale vijana ambao wanakwenda kwenye Vyuo nya Ufundis yaani VETA, kufikia mpaka laki sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Mhandisi afanye kazi ni lazima awe na *Technicians*, wale Wasaidizi wake na upo uwiano kwamba kuwe na Mhandisi mmoja na *Technicians*

watano na *Craftsmen* 25 kufikia mwaka 2025. Nilidhani wenzetu wa Mpango wangeainisha hivyo, kwamba tunataka Wahandisi 88,000 mwaka 2015 kutakuwa na *Technicians* na *Craftsmen* wangapi. Vilevile hata Madaktari 64,000, Daktari hafanyi kazi peke yake, lazima kuna Manesi na Waganga. Kwa hiyo, nadhani kwenye ule ukurasa wa 35 - 36 waone namna ya kuweka *table* inayoonesha namna ya kuendeleza hizo *middle* kada, ambazo ndiyo Vyuo vya Kilimo vya Uyole ambavyo ni kweli vinakufa, Vyuo mbalimbali vya *Medical* navyo vinatakiwa viingizwe kwenye Mpango ili wataalam waweze kufanikisha kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Wasira, ni Waziri msikivu na kwa kweli nimefarijika sana baada ya kuona kwamba Taasisi za Ufundu sasa zimetiliwa maanani kuingizwa kwenye Mpango kwa maana ya kuendelezwa ikiwemo Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na *Arusha Technical College*. Ni vizuri basi, kama ililivyojitekeza kwenye hotuba basi ionekane hadi kwenye Mpango kwamba Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya iwe kwenye *transformation* ya kutoka kwenye Taasisi kwenda kwenye Chuo Kikuu ifikapo mwaka 2015 kama inavyojonesha kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais kwamba Taasisi hii itakuwa Chuo Kikuu. Vilevile kuna Taasisi moja ambayo imeachwa ambayo inatoa taaluma kuhusiana na ardhi, Chuo Kikuu cha Ardhi hakimo kabisa mahali popote. Sasa utaendelezaji mipango ya ardhi kama huwezi kuwa na Rasilimali watu wa Ardhi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusu elimu ya ufundi stadi. Nashukuru Serikali imeweka mkazo mzuri sana. Hii ni Serikali sikivu inayojali watu wake lakini, napendekeza kwamba ni lazima tuwe na mkakati unaoeleweka kwa sababu sasa hivi tunazo shule karibu kila Kata na kila Wilaya ina shule siyo chini ya 20 mpaka 30. Kwa hiyo, maana yake tunaongelea wanaomaliza shule za sekondari Kidato cha Nne siyo chini ya 300,000 na kuendelea katika nchi nzima na wanaokwenda Kidato cha Tano hawawezni kwenda wote maana yake, idadi kubwa ya vijana inabaki na hao ndio tunawakuta leo hii kwa sababu hawana *skills* zozote zile, kuanzia asubuhi mpaka jioni wanacheza *pooltable*. Hao ndio vijana ambao tunawaita vijana wa *dot com* kwamba huwezi kumwambia achukue jembe kwenda kulima kama hujamwezesha *ki-skills*. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa jitihada zake za kupunguza tatizo la kutenga fedha za mikopo katika Bodi ya Mikopo ya Vyuo Vikuu kwa kuwapa asilimia nne, nawapongeza sana, ni mkakati mzuri utakaopunguza matatizo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile iweke kipaumbele sasa ni namna gani zitapatikana fedha za kujenga Vyuo vya Ufundu vya VETA katika kila Wilaya kama ilivyoazimiwa ili hawa vijana wanaomaliza Darasa la 12, waweze kupewa *skills* za maeneo mbalimbali kama kilimo, ufundi, ufugaji na waweze kujajiri au kuajiriwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niishukuru sana Serikali na niwahakikishie wananchi wangu wa Makete kwamba kwenye Kitabu kile cha Mpango, Makete haikusahauliwa, barabara yetu ya Njombe hadi Makete kwa kiwango cha lami imo na itajengwa kwa kiwango cha lami. Naishukuru sana Serikali. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa, niwaombe wenzetu wote kwamba huu ni Mpango wa Taifa na kwa yeote mwenye nia njema na Taifa hili, basi tusaidiane kutekeleza Mpango huu. Ni vizuri ukamsaidia mwenzako ili na wewe upate baadaye uzoefu na Serikali hii ndiyo yenyе uzoefu pekee, ndiyo maana imeainisha mambo kama haya yote yanayoolewaka. Naunga mkono hoja, nashukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Freeman Mboge sijamwona, namwita anayefuata, Mheshimiwa Luhaga Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia Mpango huu wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa dhamira yake ya dharti ya kuwaleta maendeleo Watanzania. Tutamkumbuka na atatuachia *record* nzuri ya mtiririko mzima wa uletaji maendeleo kwa wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Tume yetu ambayo pia ni wazo lake aliloamua kuianzisha Tume hiyo ya Mpango, kwa mipango hii mizuri ya mkakati mzima wa kuwaleta Watanzania mandeleo kwa muda wa miaka mitano ya kwanza na baadaye mitano ya kati na baadaye mitano ya mwisho, jumla ya miaka 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wetu huu tulioletewa ni mzuri na ninaanza kwanza kabisa kwa kuunga mkono, isipokuwa Wabunge sisi tumeletewa leo kwa jukumu kubwa la kuuboresha na tulishataarifiwa toka awali kwamba umeishaletwa Mpango huu, tunauboresha ili uweze kuendana na hali halisi.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, kuna wasiwas ikwamba labda kwa sababu hii ni bajeti ya mpito na hivyo sasa haijazingatiwa katika Mpango. Suala lililojitekeza hapa ni kwamba, wakati Mpango unakamilishwa, ni wakati huohuo bajeti na yenyewe iko kwenye hatua za mwisho. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba na kwa sababu hii ilikuwa ni *draft*, wataalam wetu baadaye sasa wataenda kuainisha yale yaliyopangwa katika bajeti ya mwaka huu na zile fedha ambazo zitakuwa haziko *covered* na bajeti ya mwaka huu, maana yake kwamba zitagawiwa katika ile miaka mingine inayofuata minne. Kwa hiyo, sidhani kama tunashindwa, isipokuwa huu ni mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wetu unayo mambo ambayo yanahitaji kuboreshwa, yanahitaji kuongezwa. Kwa mfano, Mpango huu umezungumza vizuri sana juu ya mapato yetu kwamba tuna rasilimali za kutosha, lakini mapato yetu hayawiani na rasilimali tulizonazo. Vilevile umezungumzia juu ya matumizi yetu ya Serikali lakini Mpango mzima katika majedwali haujaonesha hiyo kazi muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri suala la kutafiti kuona vyanzo vya mapato yetu, *loopholes* ambazo zinapoteza fedha zetu, ni Mpango ambao unatakiwa kuingizwa humu lakini vilevile kupitia mapitio ya matumizi katika Mashirika yetu ya Umma, katika

Serikali Kuu na katika Serikali za Mitaa. Ni vizuri hii ikawa ni kazi maalum ya kufanyiwa mapitio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linapendekezwa hapa kwamba hatushuki asilimia 35 ya matumizi yetu ya maendeleo, nadhani kwamba huku tunarudi nyuma, tulishapiga hatua, tumekuwa na hii asilimia 35, asilimia 30 kwa kipindi kirefu lakini niipongeze sana Serikali kwa kukubali. Nilisimama hapa mara nyingi kuiomba Serikali ipunguze matumizi yake na nikapendekeza na *percentage*. Serikali katika bajeti ya mwaka jana ilikuwa na matumizi ya kawaida asilimia 33 leo katika bajeti inayopendekezwa, Serikali yetu imepandisha matumizi ya maendeleo kutoka asilimia 33 mpaka asilimia 37. Kwa hiyo, siyo hatua ya kubeza, tunaipongeza Serikali. Naomba sasa katika Mpango huu, tusirudi tena kwenye asilimia 35, isipokuwa tuhakikishe kwamba miradi yetu ya maendeleo inatekelezwa kwa asilimia 40 na kuendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa napitia majedwali, niligundua kwamba kuna upungufu kwamba lengo lililokusudiwa na fedha zilizotengwa zinaleta mkanganyiko mkubwa. Lingine katika Mpango wetu, Miradi ya Maendeleo inayopendekezwa na miradi inayotekelozwa, napo bado kuna mkanganyiko. Naomba watu wa Tume waende wakapitie vizuri, kwa sababu unapoendeleza mradi, lakini kuna miradi mingine ambayo inatekelezwa, mradi unatekelezwa leo kwa miaka mitano, ni vizuri ikazingatiwa sana katika suala zima la mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi hawana sifa za kukopesheka. Watanzania wengi ambaeo leo tunataka sasa sekta binafsi tuikuze, lakini upatikanaji wa mikopo bado ni tatizo. Sasa ukienda katika mpango wetu, umeainisha vizuri sana namna ya kuwawezesha Watanzania hawa ardhi zao ziweze kupata hati miliki na kisha wawe na sifa za kukopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizotengwa katika shughuli hiyo ya kuwawezesha Watanzania wengi, kwanza tukasema tutoke asilimia 5 mpaka asilimia 10 ya Watanzania kuwa na mashamba, kuwa na viwanja vilivyo na hati miliki. Hicho ni kiwango kidogo mno, hatuwezi kupiga hatua kama tunavyotarajia. Mimi ningeshauri, tulenge kuwa na asilimia kubwa, Watanzania wengi tuwawezeshe, waweze kukopesheka, waweze kuwekeza kwa sababu tukifanya mzaha, shughuli za uwekezaji hapa ndani ya nchi, Watanzania watakuwa watazamaji, watakuja watu wengine kuwekeza. Tuweke fedha za kutosha, Halmashauri zetu zihakikishe kwamba zinanunuliwa vifaa vya kupima mashamba, vya kupima viwanja na gharama ya kupima hivyo viwanja na mashamba iwe ni rahisi sasa. Sasa hivi taratibu za kupata hati miliki ya mashamba ni ngumu mno, wananchi wetu wengi wa kawaida wanashindwa. Hela zilizopendekezwa hapa ni bilioni 141.9, hizi ni fedha ndogo, watu wetu wa Tume waende wakafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tumekuwa hatuna Benki ya uhakika kwa ajili ya kupata mikopo kwa ajili ya uwekezaji. Benki yetu ya *TIB*, ukienda katika utekelezaji wa mpango wetu tumeipangia bilioni 100 tu kwa miaka mitano, kwa maana kwamba tutakuwa tunapeleka bilioni 20 kila mwaka. Fedha hizi hazitoshi kuwawezesha Watanzania kupata sehemu ya kujipatia fedha kwa ajili ya kuwekeza. Mimi nilikuwa

napendekeza na naomba kwamba lile agizo la Mheshimiwa Rais la kupeleka bilioni 100 kila mwaka kwa mfululizo wa miaka minne katika Benki yetu ya *TIB* litekelezwe. Mwaka huu tumepeleka bilioni 50, lakini naomba kabla hatujamaliza mwaka huu wa fedha, ile bilioni 50 iliyobaki na yenyewe ipelekwe. Hapa ndipo pale Mwenyekiti wangu wa Kamati alikuwa anasema kwamba utekelezaji hafifu wa mipango. Tuanze sasa, tulishaamua na tulishapanga, tupeleke hizo fedha ili Watanzania waendelee kupata fedha kwa ajili ya mikopo yao. Vilevile katika Mpango huu tukiendelea kupeleka kwa muda wa miaka mitano, tukipeleka bilioni 100, tutakuwa na bilioni 500 kwa kipindi cha miaka mitano. Tayari tutakuwa tumewafungulia mlango mkubwa wa kujipatia fedha nyingi za kutosha kwa ajili ya kukopa na kuwekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala lingine ni ile Benki ya Kilimo, tumezungumza hapa tunapeleka bilioni 100 katika mpango wetu. Mimi naomba sana tupeleke bilioni 100 na yenyewe kila mwaka, napo tutakuwa tumepeleka fedha zetu za ndani bilioni 500 katika Benki hiyo ya Kilimo. Hata tukipata wafadhili wengine, maana tunazungumzia kwa miaka mitano, tutakuwa na fedha katika Benki yetu ya Kilimo zaidi ya trilioni moja. Tutaweza kupiga hatua, ukizingatia kwamba mikopo ya kilimo ni mikubwa na ni ya muda mrefu. Kwa hiyo, inahitajika *capital* kubwa ili Watanzania wengi waweze kukopesheka. Hivi sasa ninavyozungumza, mikopo iliyoombwa katika Dirisha la Mikopo katika Benki ya Rasilimali (*TIB*) ni bilioni 107, wakati fedha zilizopo pale ni bilioni 42 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la usafiri hasa usafiri wa vijijini, mpaka sasa hivi tunavyozungumza, ukizungumza na wananchi wa Kisese leo hii, asilimia 70 ya wananchi wa Kisese hawana barabara za vijijini kwa maana hiyo, tunalolizungumza hapa la kuwezesha kusafirisha mazao kutoka *point A* kwenda *point B* haliwezekani. Nimepitia Mpango wetu, nikaangalia Kifungu hicho kimetengewa kiasi gani, ndiyo maana pale mwanzo nikasema lengo letu haliendani sawasawa na fedha zilizotengwa. Zimetengwa bilioni 18.9, kwa maana ya kwamba kwa muda wa miaka mitano kila Halmashauri itapata milioni 177.8 tu. Fedha hizi hazitoshi, tunahitaji kupata fedha za kutosha ili kuwezesha vijiji vyote viweze kupitika, wananchi wetu waweze kufanya biashara, waweze kukuza uchumi pamoja na kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali makini, imeweka utaratibu mzima wa kuweka mtandao mkubwa wa barabara karibu nchi nzima lakini kuna barabara muhimu ambayo nataka niwakumbushe. Kuna ile barabara ya kutoka Lamadi mpaka Bariadi iko kwenye Mpango huu na inajengwa kwa lami lakini barabara ile ikiishia Bariadi tu haitakuwa na matokeo mazuri. Nashauri sasa ile barabara ya kutoka Lamadi – Bariadi - Kisessa – Mwandoya – Mwanhuzi - Arusha na upande mwingine ikaenda Singida, itafunga kwa kiasi kikubwa sana shughuli za uchumi katika Mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Singida na Arusha. Hapa tunafanya shughuli nyingi; tunalima pamba kwa wingi, tunalima mahindi kwa wingi, madini, utalii na watu wa Singida wanazalisha vitunguu kwa wingi. Kwa hiyo, tukiimarisha barabara hii, ni barabara muhimu sana, naomba iingie katika Mpango huu wa miaka mitano, isisubiri baadaye kwa sababu ni ya muhimu mno kwa ukuaji wa uchumi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la maji ambalo ni visima 10 kila Wilaya. Mpango wetu huu umetengewa shilingi bilioni 272 kwa ajili ya shughuli hiyo. Sasa bilioni 272 ukizigawa kwa miaka mitano na ukizigawa kwa Wilaya, maana yake ni kwamba kila Wilaya itakuwa inapata milioni 513 kwa kila mwaka, maana yake ni kwamba tutajenga mradi mmoja tu wa maji kati ya ile miradi 10 ambayo inatekelezwa kila Wilaya. Kwa Mpango huu, maana yake tutakuwa tunajenga kisima kimoja kimoja tu. Niwaombe watu wa Mpango waangalie kipengele hiki ili waweze kuongeza fedha za kutosha, tuhakikishe kwamba hivi visima tulivyowaahidi ambavyo sasa hivi vinachimbwa kwa baadhi ya maeneo, tunapeleka fedha nyingi za kutosha ili miradi hii iweze kuisha mapema na wananchi wetu waweze kupata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali, Kiwanda cha Nyama Shinyanga kimetajwa na Mheshimiwa Waziri, Serikali yetu imeamua kwa dhati na mimi nisisitize tu kwamba utekelezaji wa mradi huu ufanyike mapema iwezekanavyo ili kuwanusuru wananchi wa Shinyanga wanaohangaika kila leo kwa kukosa mahali pa kuuzia mifugo yao. Wanahangaika Arusha, Dar es Salaam, sijui wapi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Kupanga ni kuchagua sasa!

MHE. ROSWEETER F. KASIKILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nakushukuru kwa nafasi hii uliyonipa ili niweze kuchangia. Pia nimshukuru Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuwa na wazo la kurudisha tena huu utaratibu wa kuwa na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Tunajua kwamba Mpango huu ni wa kutekeleza Dira ya Maendeleo ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na naupongeza Mpango huu. Naunga mkono Mpango huu kwa sababu kwa uhakika umewajali wananchi wote kwa ujumla, wanawake kwa wanaume. Ukiusoma Mpango huu kuanzia ukurasa wa kwanza mpaka wa mwisho, umewajali vijana na hata ukisoma ukurasa wa 49 na 69 wa toleo hili la Kiingereza, umezungumzia ni jinsi gani ambavyo unakwenda kuwapatia ajira vijana. Pia umezungumzia hata wale mabinti ambao kwa bahati mbaya masomoni wanapata ujauzito, wanarudi nyumbani lakini umeweka mikakati ni namna gani haitawatupa wasichana hawa ila itakwenda kuwasaidia katika ajira mbalimbali na kuwaendeleza. Kwa hiyo, umewajali vijana, wasichana kwa wavulana. Pia mpango huu umewajali wakulima wadogo na wa kati, umewajali wafanyabiashara na umewajali hata na wafanyakazi. Kwa hiyo, ni mpango ambao ukitekelezwa vizuri, kwa kweli utakuwa umewasaidia watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makundi tete (*vulnerable groups*) hayakusahauliwa. Wajawazito wamezungumziwa kwamba watasaidiwa watoto chini ya miaka mitano, hata

walemavu watasaidiwa. Ukiangalia katika mpango Mpango huu, ukurasa wa 70, umezungumzia katika kipengele cha sekta ya afya, mpango umezungumzia ni jinsi gani utakavyoweka mikakati ya kupunguza vifo vinavyotokana na malaria, vifo vinavyotokana na ujauzito na vifo vya watoto wachanga, Mpango umezungumzia yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea ukurasa wa 51 mpaka 70, Mpango umetaja vipaumbele vikuu vitano ambavyo ni miundombinu, kilimo, viwanda, maji na rasilimali watu. Katika miundombinu, mpango umezungumzia masuala ya umeme, bandari, barabara, reli, masuala ya anga, uchukuzi wa anga, kwamba utekelezaji utakapokuwa umefanyika na haya yakaboreshwa, kwa kweli hata hawa wafanyabiashara kutoka nje ambao wameanza kutuacha Tanzania wanakwenda kuingia kwenye bandari za nchi jirani, sasa hawatakwenda tena, ila wataendelea kuja nchi ya Tanzania na uchumi wetu utaendelea kukua. Kwa kuboresha barabara au Reli ya Kati, ni kwamba wananchi hasa wale waliokuwa wanaelekea Kigoma (Watani wangu) sasa watakuwa hawana tena tabu ya kwenda kwa kutumia mabasi kwa sababu mabasi ni ghali sana lakini reli hii itasaidia kwenda Kigoma na hata Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mpango umezingatia mambo mengi. Naweza kudiriki kusema kwamba umekuwa ni Mpango wa Kitaifa kwa sababu umeshirikisha Wizara na Idara mbalimbali (*agencies* mbalimbali) katika kuuandaa au katika kukusanya mawazo. Mpango haukuacha tena Halmashauri za Wilaya, umewashirikisha katika kuchanganya mawazo yao ili mpango huu uweze kupatikana. Huu ni Mpango ambaoumeweka mikakati na shughuli mbalimbali ambazo kama zitatekelezwa vizuri, itakuwa inaleta maendeleo katika nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni jambo moja, lakini utekelezaji pia ni jambo lingine. Mimi kwa upande wangu naomba huu Mpango ulivyowekewa hizi *interventions* utekelezwe, usibaki kuwa ni mpango tu unaokaa kwenye makabati, uende ukatekelezwe kama kweli tunataka maendeleo ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji, watendaji wote na kila atakayehusika katika utekelezaji itabidi zile *mindset* zetu za kukaa na kuangalia sijui huu mpango unamhusu nani zibadilike, kila mmoja kwa nafasi yake aweze kusimama na kuwajibika kweli na kwa uadilifu mkubwa katika kutekeleza huu mpango ili tuweze kuona mafanikio yake mazuri. Kwa hivyo, mpango utekelezwe kwa uadilifu na kwa uwazi zaidi, mafungu yanapokuwa yamepitishwa hapa halafu yakinudishwa kwenye Halmashauri au kwenye Wizara na Idara mbalimbali, hizo pesa ziweze kuoneshwa kwa uwazi zaidi, ikiwezekana basi ziweze hata kuoneshwa kwenye mbaa za matangazo ili kila mwananchi aweze kujua kazi iliyokuwa imepangwa na pesa zilizotolewa ni kiasi gani. Uwazi huo uendelee mpaka ngazi ya Vijiji na Kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utekelezaji ni muhimu tuwashirikishe na wananchi kwa sababu mara nyingi hawa tumekuwa tukiwatumia katika kutambua vikwazo na katika kutambua fursa na hatimaye wameweka mipango yao shirikishi ya vijiji, mipango ambayo imeundwa ikatoa mipango ya Halmashauri na hatimaye mipango

ya Wizara na Kitaifa sasa hivi. Kwa hiyo wakati wa utekelezaji tusiwaweke wananchi pemberni, tuwashirikishe katika kutekeleza na hata katika kutathmini na ufuatiliaji wa kazi hizi ambazo walikuwa wamezipangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa suala la pesa kupelekwa kwenye Wizara na Halmashauri mbalimbali, naiomba Serikali wakati wa kutekeleza Mpango huu, Serikali iwe makini katika *ku-release funds* mapema. Isije ikawa kwamba labda shughuli ambazo zingeweza kutekelezwa katika robo ya kwanza na robo ya pili hazifanyiki kwa sababu tu Serikali haijatoa mafungu. Mafungu yatolewe mapema ili watendaji wasiwe wa kulaumiwa, maana wakati mwingine tunawalaamu watendaji lakini kumbe wangefanyaje wakati hawajapelekewa pesa. Serikali iangalie hali hii, itoe pesa mapema ili kazi iende kutekelezwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi yangu machache ni hayo, naunga mkono Mpango huu kwa asilimia zote mia moja. (*Makofî*)

MHE. PINDI H. CHANA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nianze kwa kukiri kwamba naunga mkono hoja hii, nikimpongeza Waziri Mtoa Hoja na timu yake na Mawaziri ambao wanashirikiana naye katika Ofisi ya Rais. Aidha, nichukue nafasi hii pia kuipongeza sana Tume ya Mipango na kuridhia malengo matatu ya hoja hii wakati inawasilishwa kwamba Bunge liridhie Mpango wa Maendeleo, Bunge liridhie Mapendekezo kwamba mwaka 2011/2012 iwe ni kipindi cha mpito, lakini pia Bunge liridhie vipaumbele vilivyowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu Mpango huu, kwanza kabisa, vile vipaumbele vimezingatia haja za wananchi. Katika vipaumbele, ni ngumu sana kusema unahitaji masuala ya kilimo, maji na barabara kama hujazingatia haja za wananchi. Kwa hiyo, naungana kabisa na azma nzima ya Wizara na Serikali ya kutuletea Mpango huu na hususani kwa kutambua kwamba imizingatia vipaumbele. Ni imani yangu kwamba Mpango huu umetokana na *Vision 2025* ambapo sote tulijadili *Vision* ile na kwamba 2025 tutakuwa na malengo haya. Sasa yale malengo ni muhimu yakawepo katika vipindi vidogo vidogo, kwa hiyo, naungana kabisa na azma hii ya Mpango huu katika kipindi hiki na hivyo ni wajibu wangu kama mwakilishi wa wananchi kuunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo ningeomba kusitiza ni juu ya yale maeneo ambayo tumeoneshwa kwenye Mpango yanayohusiana na suala zima la changamoto, changamoto ambazo zimeainishwa wakati Waziri anawasilisha hoja. Nimefurahi kwa sababu kitendo cha kujua changamoto zipo ni nusu ya kutatua tatizo, baada ya kufahamu kwamba changamoto hizo zipo na mikakati ambayo imewekwa ni mikakati ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo changamoto za namna gani ya kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja, kipato cha vijana na kwa kuwa vijana ni asilimia 60 na mimi niungane kabisa na azma hiyo lakini niendelee tu kushauri kwamba Mpango huu sasa baada ya sisi Wabunge kuupitisha kama ilivyoelezwa kwenye hotuba uende kila

Halmashauri, *Local Government Authorities*, kila wakala wa Serikali, yale maeneo ambayo yanawahuhsu iwe ni Kilimo, Maji, Miundombinu wanaya-*summarize* kuendana na eneo lile ili utekelezaji wake ufahamike kulingana na eneo lile. Sambamba na hilo tuwe na *framework* kwamba baada ya kipindi fulani tunakwenda kutathmini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi wananchi wa Ludewa Mkoa wa Njombe tunashukuru sana maeneo mengi yamezingatiwa ikiwa ni pamoja na Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo, masuala yale tutaya- *summarise* kutokana na Wilaya husika na jambo hili likienda kila Wilaya, yale maeneo ambako miradi ile imeainishwa, ile Wilaya ndiyo ishiriki pamoja na Waheshimiwa Madiwani kusimamia mpango huo ndani ya kipindi kilichopangwa utekelezaji wake uwe umefanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo mengine ambayo ningependa kusisitiza ni suala zima la kuongeza mapato. Tunaposema kuongeza mapato, ni muhimu sana tukaongeza suala zima la *export* bidhaa lakini ili tufanikiwe bidhaa za kwenda kuuza nje ya nchi ni lazima bidhaa hizi zianzie ndani, maana tunapokuwa na masoko ya uhakika ndani kwa mfano suala la kilimo tukawa tuna masoko ya uhakika ndipo hapo masoko hayo yanapokuwa yanaeleweka, ni rahisi kuchukua bidhaa zile tukazipeleka kwanza kwenye Soko la Afrika Mashariki (*East Africa Common Market*) na baada ya hapo tukapeleka kwenye masoko ya nchi za jirani ambazo ni *landlocked* kama Congo, Rwanda, Burundi na kadhalika. Kwa hiyo, nilidhani hayo ni maeneo ambayo ni muhimu sana wakati tuna-*summarise* Mpango huu ushuke kwenye *Local Government Authority* (Serikali za Mitaa) ili maeneo yale ya msingi tuweze kuyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo suala zima la elimu, maana Vijana ni asilimia 60 ya idadi ya watu milioni arobaini na wao wanahitaji stadi za kazi. Kwa hiyo, suala zima la elimu, tukubaliane kisera kama tulivyokubaliana tuwe na sekondari kila Kata, basi Vyuo vya Ufundidi Stadi tuwe navyo kila Wilaya. Tunaweza tukakubaliana kila Wilaya kama tulivyosema tuwe na *VETA* na vyuo mbalimbali tukaweka utaratibu huu na wale wadau wa kwenye Wilaya hizo au maeneo hayo husika wakaweza kuyasimamia na hivyo Mpango huu ukawa ni mpango ambao unatekelezeka, unasimamika na bajeti zake zinaeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu sana ni pamoja na suala zima la miundombinu, yapo masuala ya barabara za aina mbalimbali zote hizi ni lazima tuzingatie. Naomba kuendelea kusisitiza suala hili la barabara, ni lazima tujenge zile barabara ambazo zipo kwenye kiwango. Kwa hiyo, suala la kusimamia Mpango huu kama tulivyokubaliana liwe ni jukumu la kila mwananchi kama Waziri alivyoeleza wakati anatoa hoja, liwe ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti sambamba na hilo, ningeomba barabara ambazo tutakuwa tunaendelea kuzijenga ziwe kwenye viwango na kama ilivyotokea asubuhi kwamba tunaposema kwenye viwango vitu kama madaraja yanapojengwa yasiwe madaraja ya mbao, yale madaraja ya mbao yaye *phased-out*, kwa hiyo, haya masuala yakiingia vizuri kwenye sera, utaratibu wake unakuwa mzuri. Aidha, nichukue nafasi hii pia kushauri ushirikiano wa *Public Private Sector*, katika Mpango huu tumekubaliana

kwamba tutashirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta binafsi. Ningombwa kushauri hili suala ni la msingi. Kwa hiyo, katika utekelezaji ni muhimu sana tukawa na *data*, tunaposema tutashirikiana na sekta binafsi, kama ni Idara ya Afya hawa watu wa sekta binafsi ni akina nani? Tunapokwenda Idara ya Miundombinu, *Public Private Partnership* ni akina nani? Kama ni mabenki katika kutekeleza masuala ya kukopesha vikundi, wanawake na vijana tunaendaje? Pia *Private Sector* hizi ni lazima tuzungumze nao ili waweze kuwasaidia wananchi kama jinsi azma ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya taasisi ambazo ni *private sector* unakuta kama ni wakati wa mikopo, riba zao zinakuwa zipo juu sana. Kwa hiyo, maeneo hayo ni lazima tuwashauri. Kama ni benki basi wanapotoa riba ya mtu anayefanya biashara isifanane na yule mjane au kijana ambaye azma yake ni kupunguza umaskini. Haiwezekani mwananchi mmoja anaenda kuchukua mkopo labda wa kununua trekta anaambibiwa riba ni asilimia kumi na sita, akienda mfanyabiashara mkubwa naye riba ni asilimia kumi na sita kwa kiwango chochote kile. Kwa hiyo lazima tukubaliane tukae na sekta binafsi ili tunapotekeleza Mpango huu, sekta binafsi zisiangalie upande wa faida tu, tuwe na *win win situation*. Nadhani jambo hili ni la msingi sana tuendelee kuangalia ni namna gani tunashirikiana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ni muhimu ni suala la kuongeza kiwango cha fedha na wataalamu zaidi katika Tume, *Non Tax Revenue*. Tukiongeza wigo ni jambo ambalo litawezekana, kwa sababu eneo kubwa sana la mapato, rasilimali ambazo zitatumika kwenye mpango tunategemea kodi na tozo mbalimbali, hivyo ni muhimu sana tukabuni ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi kuna taratibu nyingi sana za kutekeleza mipango, baadhi ya maeneo kuna masuala ya *Build Operate And Transfer*, baadhi ya maeneo kuna *Build Operate And Use The Property*, kwa hiyo tutakapokuwa tunaingia katika masuala hayo, tutakaposhirikisha sekta binafsi itatusaidia sana. Mipango hii ni muhimu inabidi tuiunge mkono. Kwa mfano katika masuala ya ujenzi, tumeona maeneo mengi sana tumeshirikiana na sekta binafsi kujenga, Chuo chetu cha Dodoma tumeshirikiana na sekta binafsi. Sasa utaratibu huu wa kushirikiana na sekta binafsi ukienda hadi kwenye masuala ya miundombinu ya barabara itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii na ninawaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa kweli kama tuna nia njema ya kumsaidia Mtanzania, Mpango huu ni muhimu na tunaendelea kuwa na mipango mbalimbali katika nchi yetu lakini mpango huu hususani kwa kipindi hiki umekuja wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kuunga mkono hoja. (*Makofit*)

SPIKA: Kwa kuwa muda uliopo hauwezi kutosha kumwita msemaji mwagine, tutaendelea mchana, tukirudi mchana ataanza Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Mbewe na Mheshimiwa Charles Mwijage.

(*Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nina matangazo machache, ninawatangazia kwamba Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT, wameleta fomu za mkopo wa matrekta na zana zake, yejote anayehitaji kukopa anashauriwa kuchukua fomu hizo zilizopo katika Ofisi ya Katibu wa Bunge, nadhani unaweza kuchukua fomu kwa ajili ya wapiga kura wako pia kama inawezekana. Ipo *opportunity* hiyo, hata kwenda kujua habari zake pia ni muhimu, utakapojuwa habari zake utawaza kuwashauri wapigakura wako namna gani ya kuweza ku-access hiyo habari.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa sina tangazo lingine, napenda kusitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.55 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikalia Kiti

KAMATI YA MIPANGO

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa David Z. Kafulila, karibu.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa mara ya kwanza jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kwa heshima zote nashukuru kwa mara ya kwanza nikiwa Mbunge nashiriki kujadili mpango mkubwa ambao tunasema kwamba ni mpango wa kiuchumi kwa miaka mitano. Kwangu nasema kwamba hii ni siku yangu ya kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya kusema kwamba, siku yangu hii ni ya kipekee, napenda kusema kwamba, imekuwepo mipango mingi ya kujenga uchumi wa Taifa hili tangu tulipopata uhuru. Ni bahati mbaya sana kwamba inawezekana kwa muda mrefu kama Taifa hatujaamua kubainisha dira na mikakati, ni kwa namna gani dira yetu na mikakati yetu itakuwa. Nakumbuka katika soma yangu nilisoma kwamba, Waasisi wa Taifa hili walikusudia kujenga Taifa ambalo wanaipata *Egalitarian Society*. Kwamba ni *society* ambayo pamoja na kutofautiana kiutajiri, lakini kila mmoja anayo nafasi ya kupata huduma za kimsingi kama elimu na afya kwamba mtoto wa maskini hakosi elimu bora kwa sababu ya umaskini wa familia yao wala mke wa mkulima maskini hakosa huduma bora ya afya kwa sababu ya umaskini wa mume wake au familia yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine hii ingekuwa ndio dira kwa kuwa hii ndio ingekuwa ya tangu awali tokea Taifa hili likiwa linaasisiwa mpaka sasa tukiwa

tunatimiza miaka 50. Kimsingi huu mkakati umekuja ikiwa ni miaka 50 tangu tupate uhuru, tungeona ni kwa kiasi gani tumefanikiwa kufikia lengo hilo. Nimeona nianze na hapo kwa sababu moja ya changamoto kubwa ambayo inakabili uchumi wetu kwa sasa na kwa zaidi ya miaka 20 ni ongezeko la wasio nacho na walio nacho linakua siku hadi siku, kwenye uchumi wanaita *gene concentration*, nilikuwa nasoma vitabu vya uchumi sasa hivi inaelekea kuwa nne, *rank* ambayo ni ya juu sana. Kwa maana ya kwamba tofauti ya asiye nacho na aliye nacho kadri ambavyo inaongezeka ndivyo ambavyo mnazidi kuongeza uwezekano wa migogoro mikubwa iwe ya kisiasa, ya kiuchumi na hata kimaisha kwa sababu kimsingi wale wasio nacho mwisho wa siku huwa wanaelekeza hasira zao kwa walio nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji kujenga uchumi ambao utapunguza *gape* hiyo. Kitu ambacho ni bahati mbaya sana kwenye mkakati huu sijakiona. Kwa hiyo, ningependa kushauri kwa sababu tunajadiliana, watalaan waangalie ni kwa namna gani wanaweza kupunguza tofauti ambayo inaongezeka kwa kasi kati ya wasio nacho na walio nacho na waweke *indicator* kwamba katika miaka mitano tutahakikisha tofauti kati ya walio nacho na wasio nacho inaelekea kuwa 0.4%, pengine katika miaka mitano tutapunguza ibaki asilimia 0.2 au 0.1 kwa kadri ambavyo inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo haliwezekani kama tutakwenda na mazoea ya mfumo wa kiuchumi na mikakati ambayo tumekuwa tukiifanya tangu miaka ya 1990 baada ya kuingia kwenye uchumi wa soko huria lakini bahati mbaya sana kwamba tuko kwenye soko holela. Maana hata nchi ambazo zimekubuhu kwenye uchumi wa soko huria bado kuna nidhamu ya kuhakikisha kwamba wanaangalia tabaka la chini ni kwa kiasi gani ambavyo linaweza likajaliwa japo katika huduma za msingi ambazo kila binadamu anahitaji kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, moja ya changamoto kubwa ambayo ningependa kuitoa katika mpango huu, tuangalie ni kwa namna gani tutapunguza tofauti hiyo. Lakini tofauti hiyo, haiwezi ikapunguzwa kama lengo kubwa au lengo namba moja kama inavyozungumzwa hapa itakuwa ni kuhakikisha tunazidi kuongeza au kukuza uchumi. Dokta Mipango nilimwambia siku ile wakati tunafanya semina, ukweli ni kwamba tatizo la Taifa hili siyo ukuaji wa uchumi, siyo kweli. Ukweli tatizo la uchumi wa Tanzania siyo ukuaji wake, tatizo ni kwa namna gani ule ukuaji unabeba tabaka kubwa la watu siyo *broad based*, ni *narrow based*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatima yake mtakuza uchumi hata kwa asilimia 50 lakini mnajenga maskini zaidi ya asilimia 50. Leo tunajipongeza kwamba Tanzania ni mionganoni mwa nchi 20 duniani ambayo kasi yake ya ukuaji wa uchumi iko juu. Lakini wakati huo huo Tanzania hii hii ni mionganoni mwa nchi 20 duniani kwa umaskini. Kwa hiyo, lazima tuangalie hapa *equation* ambayo bado hatujaipatia majibu. Uchumi unakua, tunapata rekodi ya dunia, lakini wakati huo huo tunapata rekodi ya umaskini duniani. Sasa ni kwa namna gani tunaweza tukatanzua mgogoro huo. Kimsingi njia pekee ya kuufanya ukuaji wa uchumi ubebe sehemu kubwa ya watu wengi ni kuhakikisha kwamba shughuli za watu wa kawaida kwa maana ya kilimo katika dhana

pana katika dhana ya uvuvi, katika dhana ya ufugaji, katika dhana ya kilimo cha mazao inasukumwa ikue kwa asilimia ya kutosha. Tusilenge tu kukuza uchumi kwa asilimia nane ifikapo mwaka 2015, hebu tujaribu kulenga kukuza kilimo kifike asilimia nane ifikapo mwaka 2015 tuone. Mpaka leo kilimo kinakua kwa asilimia takriban nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na watu wa *Research on Poverty Alleviation* wanasema kwamba tukikuza kilimo kwa asilimia 10 kwa miaka mitatu mfululizo tunapunguza umaskini kwa asilimia 50, hatusomi? Kwa nini tusielekeze nguvu kubwa ya ukuzaji wa uchumi wetu kwenye kilimo? Kuna Mataifa mengi ambayo *growth* yao kwa maana ya *GDP*, ukuaji wao wa uchumi uko chini ya asilimia saba lakini *standard of living*, kile kiwango cha ubora wa maisha kipo juu. Tunasema kwamba tunaziiga nchi kama za *Singapore* au *Malaysia* ambao leo ni *mini tigers* lakini *Singapore growth* yao iko around 5.8% hawajafikia asilimia 6.0. Malaysia wako asilimia 7.0. Kwa hiyo, wakati wao bado hawazungumzii kufika pengine asilimia 10 wanazungumzia ni kwa namna gani wanaweza wakawekeza kwenye sekta ambazo zina *multiply* kwa kiwango kikubwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba uchumi ule unakuwa mpana kwa maana ya kubeba watu wengi, uchumi hata ukikua kwa asilimia nne kama uchumi ule unabeba watu wengi ni wazi kwamba watu wengi watafaidika na uchumi ule.

Kwa hiyo, ningeomba Tume ya Mipango, *agenda* namba moja iwe ni kuwekeza kwenye sekta pana ya kilimo hata kama uchumi utabaki asilimia saba au hata kama utashuka asilimia sita lakini kama ukuaji ule utakuzwa na sekta ya biashara ndogo utakuzwa na sekta ya kilimo katika dhana pana ni wazi kwamba Watanzania watafaidika na matunda hayo ya uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuishauri Tume hii ya Mipango, bado naona kwamba wameshindwa kuonyesha ni kwa namna gani tunaweza tukajitegemea zaidi na ni bahati mbaya kwamba tulikusudia kujenga Taifa ambalo ni la ujamaa na kujitegemea, miaka 50 tumeshindwa kujitegemea na hata ujamaa umetushinda. Mpango huu unaonyesha kwamba takriban asilimia 30 tu ya mapato kwa ajili ya *ku-finance* miradi ya maendeleo ndio ambayo itatokana na mapato ya ndani, haiwezekani. Tujiulize hivi kweli huu utajiri wa Taifa hili ambao tunao hauwezi ukatuwezesha *ku-finance* miradi ya ndani hata kwa asilimia 50 kiasi kwamba hata kwenye kupanga, maana hawa watu wakati wanapanga walisema kwamba walipanga kwa kufikiria makubwa hivi hata wenye kupanga hawakuweza kufikiria makubwa kwenye kutafuta uwezo wa ndani zaidi kuliko uwezo wa nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kupanga kwa kutumia matarajio ya watu wa nje kwenye mipango ya ndani, tena mpaka sasa fedha ya ndani ni *around 35%*, kwa hiyo mpaka sasa bajeti ya ndani ni hiyo hiyo, tunakuja tunapanga mkakati wa miaka mitano tunabaki pale pale kufikiria dhana ile ile ya kwamba pato la ndani libaki asilimia 35, haiwezekani! Tuna migodi, je, katika hii migodi kweli utafiti umefanyika kuona kwamba wanalipa kiasi cha kutosha? Watu wanatangaza hasara miaka 20 lakini bado wanabaki, si waende kwao! Haiwezekani! Tuna Makampuni ya Simu, sasa hivi takriban Watanzania milioni 20 ni wateja wao, hivi kweli utafiti umefanyika kuhusu kodi, kweli wanalipa kodi ya kutosha? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zaidi ndugu zangu kama kuna kitu ambacho kinasikitisha ni namna ambavyo, moja sisi kama viongozi tunakuwa na dhamira ya kusimamia hii bajeti. Nidhamu katika usimamizi wa bajeti bado mgogoro. Kwa hiyo, miongoni mwa mambo ambayo ningeyapendekeza katika hili, pengine tufike mahali tupate Kamati ya Bunge, ambayo inasimamia nidhamu katika bajeti. Hii Kamati iwe inafanya kazi siku hadi siku kufanya *monitoring* kuhakikisha kwamba bajeti inakwenda kwa kadri ilivyopangwa. Jambo hili ni muhimu kwa sababu siku zote fedha huwa haitoshi. Lakini kuamua mwelekeo wa namna gani vipaumbele vizingatiwe kunahitaji nidhamu ya hali ya juu kuangalia ni kwa namna gani kile ambacho tulikipitisha ndicho ambacho kinafanyiwa utekelezaji siku hadi siku. Tofauti na hapo tutakaa Bungeni, tutapitisha mipango, tutakuja mwisho wa siku kilichotekelizwa ni kingine, matokeo yake kila siku tunapanga kushusha umaskini lakin unaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2005 maskini walikuwa milioni 11. Chama Tawala kikapanga kupunguza asilimia 50 ya umaskini. Mwaka 2009 maskini walikuwa milioni 12,700,000 unawenza ukaona kwamba ni kwa namna gani ambavyo tunapanga tu lakini ukweli ni kwamba kwenye utekelezaji kule kinachotekelizwa sicho. Kwa sababu ya kushindwa kupanga na kusimamia vizuri tunashindwa kufaidi hata rasilimali nyingi ambazo tunazo. Kwa sababu ya kupanga pasipo kusimamia vizuri tunashindwa kufaidi rasilimali kubwa kuliko zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwa nasema kwamba, kama kuna rasilimali kubwa katika Bara la Afrika namba moja ni rasilimali ya amani kwa sababu wana uchumi wote wanazungumza kwamba moja ya tatizo kubwa katika nchi za Afrika kushindwa kuendelea kwa kasi ambayo inatakiwa ni amani kwa maana ya kwamba kuna mivutano kwa sababu hakuna amani, kuna udini, kuna ukabila kwenye Mataifa mengi, matokeo yake wanashindwa kupata maendeleo kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi tuna bahati kwamba sisi tofauti na makabila, ni utani, sisi Mtawala akiwa madarakani anajadili bajeti, leo hakuna mtu yuko msituni. Kuna Mataifa ambayo tunajadili bajeti hapa, kuna *Intarahamwe* iko porini. Kama hali ya sasa ya amani ya kiasi hiki tunashindwa kuitumia kuzalisha, kukuza uchumi, kusababisha utajiri au kusababisha nafuu ya maisha, hivi kweli ikitokea bahati mbaya tunafika huko ambako wenzetu wapo, maana Mwenyezi Mungu ni yule yule, wa Congo ndiyo huyo huyo, wa Sudan ndiyo huyo huyo, wa Tanzania ndiyo huyo huyo. Tukifika mahali tukawa tunapanga bajeti na watu wengine wakawa msituni, hivi tutaendelea kweli kama hali ya sasa tunashindwa kuitumia, haiwezekani! Bahati mbaya sana ni kwamba, katika dhana nzima ya kusimamia hayo matumizi ambayo tunayapanga na kuyapitisha kuna tatizo kubwa sana la mfumo ambaa una udhaifu wa kifisadi. Kuna Waziri, kuna Wabunge wanakula rushwa, nimekamata Mbunge anaomba rushwa kwenye Halmashauri wakati Halmashauri ziko chakavu, wanalia na njaa, mipango haiendi, nilikamata Mbunge anaomba rushwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge muda wako wa kuchangia umekwisha.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Wamo humu ndani, wapo humu kuna akina Zambi, Badwel.

MBUNGE FULANI: Wataje.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Nimewakamata na nimechukua hatua, nchi hii haiwezi ikaendelea kwa *style* hiyo, haiwezekani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kafulila muda wako umekwisha. Nakushukuru kwa mchango mzuri. Naomba sasa niwataje watakaofuata kuchangia alikuwa afuate Mheshimiwa Freeman Mbewe, lakini hayupo atafuata sasa Charles Mwijage, atafuatin Joseph Roman Selasini, halafu atafuatia Hamad Rashid Mohamed. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Charles Mwijage.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia mpango wa miaka mitano wa Taifa langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mipango lina falsafa ya kiuchumi. Wachumi wanapokuwa wanapanga mipango yao kuna mambo ambayo huamua au hudhani kwamba yatabaki kama yalivyo, wao wana msemo wao wanasema *ceteris paribus*, kwa hiyo, ningeshauri tunapojadili mpango huu tuamini kwamba haya mambo yatakuwa hivi na wachumi wenyewe watakuja kuweka angalizo kwamba mambo yakibadilika itakuwa vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoanza kuchangia wale wenye vitabu vile vya Kiingereza twende kwenye ukurasa wa saba nina tafsiri ya kwangu naomba ninukuu, anasema: “Lengo kuu la mpango huu ni kuibua fursa na rasilimali zilizofichika ili kuharakisha upatikanaji wa hali na mahitaji ya msingi katika kujenga uchumi unaowahusisha watu wote”. Aliyesoma kwa kina mpango huu atagundua kwamba, hawa watu walioandaa mpango waliona na waligundua kwamba kuna kuachana ukuaji wa uchumi wa tarakimu na hali ya wananchi, kuna *gape* kuna *mismatch*. Kwa hiyo, mpango huu ukitekelezwa kama ulivyopangwa ni kwamba lile pengo la kuachana litakwisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda ndani katika zile *interventions* zilizozungumzwa, kuna mipango imeainishwa ya kuwawezesha Watanzania kuanzisha vikundi vya vijana. Hapo ndio nasema, naunga mkono mpango huu. Serikali yetu katika mpango huu ina mpango wa kuwawezesha Watanzania kuweza kumudu fursa zilizo nje ya nchi yetu na nashauri kwamba wanapozungumza nje ya nchi usifikiri kwenda Urusi acha kuweza kuzalisha mihogo Kanda ya Ziwa ukapeleka Sudan, ni fursa, kinachotakiwa ni kupata fedha, kuweza kuzalisha mazao ambayo hayana matatizo na yenye hiyo ni fursa. Kwa hiyo, lile *gap* litaweza kufichika, litaweza kuondoka pale utakapoanza kutambua kwamba huu mpango si wa Waziri Mkuu tu, ni kuanzia mtu binafsi kuja kwenye kijiji na kuja kwenye familia. Tutakapokuwa tumekubaliana na mpango huu kila mmoja aumiliki, ujiangalie wewe unafanya nini, unapungukiwa nini ili kusudi mwenzio akusaidie, ndio maana ya mpango huu. Naunga mkono mpango huu kwa kuleta majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine katika mpango huu lipo suala tata la ugumu wa maisha. Mpango huu nimeusoma kwa kina, unalenga kutoa majibu ya ugumu wa maisha, ukiusoma mpango huu, unatufungulia kitendawili cha Makampuni ya Madini kuweka yale mapato yao nje ya nchi, unapendekeza kwamba mapato yawekwe kwenye benki za hapa, iwapo mpango huu utashawishi taratibu na kanuni kubadilishwa, pesa hizo za dhahabu zikawekwa hapa, kuna uwezekano mkubwa shilingi yetu ikaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe mfano, bei ya mafuta, Ijumaa, pipa moja la dizeli kwenye soko la dunia liliuzwa dola 127, mafuta hayo yangekuwa gatini Dar es Salaam ukiweka gharama ya usafirishaji kwa *exchange rate* ya shilingi 1,540/=, lita moja inakuwa shilingi 1,400/= kabla ya tozo lingine. Kama utaratibu huu unaokuja kwamba rasilimali ziwekwe hapa, tungeweza kubahatika shilingi yetu kuimarika ikafikia dola moja shilingi 1000 pipa hilo, lita moja inaweza ikafika shilingi 840/. Kwa hiyo, huu mpango una dhana nzuri, lakini kama ikifikia shilingi 840/= kutoka 1,400/= hili punguzo la shilingi 500/= kabla ya kurekebisha tozo lingine, hayo yatakuwa ni manufaa kwenye maisha ya mwananchi, ndiyo uzuri wa mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mpango huu unazungumzia mchango wa madini ambao kimsingi tulio wengi hatujuona. Lakini katika mpango wameeleza kwamba migodi ya madini pamoja na kuchangia kodi kama Watanzania tungekuwa tunaweza kupeleka ugavi viwandani, tukapeleka vitunguu, nyama na maziwa wananchi wetu wangeweza kupata pato kubwa mno, pamoja na kodi, viwanda au migodi ya madini ina faida kutokana na zile *supplies*. Lakini amekwenda zaidi katika mpango huu ambao nauunga mkono, wakasema Serikali ina lenga kuona wananchi wanashiriki katika dhahabu hizi, madini haya ya almasi katika kuchimba na lakini katika kuongeza thamani ya vito. Utakuja kuona kwamba kwa kufanya hivyo, kile kitendawili cha tunafaidi nini katika migodi hii kitaweza kutanzuliwa. Kwa hiyo, naunga mkono mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye dhana ya kutengeneza ajira. Naunga mkono suala la kuanzisha Vyuo vya Ufundji, VETA. Uko mpango mzuri wa kutengeneza VETA kila Wilaya, lakini kwa niaba ya Mkoa wangu ningeomba Chuo cha VETA kikubwa kama kile cha Changombe kijengwe haraka sana Kagera, sisi hatuna VETA kule, mngeanza na kwetu kwani vijana wangu wanahitaji VETA. Lakini katika kutengeneza ajira, kuna hizi program zinazozungumzwa za kuwaweka vijana vikundi, nimeshakwenda *SELF*, nimeshazunguka Jimboni kwangu, nimeshapeleka makabrasha ya *SELF*, ningeomba mipango hii isambazwe nchi nzima na hizo pesa zije kusudi watu wapewe. Lakini chondechonde mtu hawezi kupewa pesa akiwa amelala kitandani, lazima uwe na kikundi kusudi waweze kukusaidia na lazima uende SACCOS, ni nani huyo anayeweza kugawa pesa? Kwa sababu hiyo, nauunga mkono Mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye suala la elimu na ujuzi. Tulianzisha sekondari za Kata, watu wanaziita majina mengi, mimi naunga mkono mpango huu katika kulenga kuziboresha shule hizi, wazipatie walimu, tukamilishe miundombinu na natoa taarifa kwa Serikali kwamba kwa Jimbo langu, kazi niliyofanya nimewahamasisha,

kila sekondari tumeshakusanya matofali, tunasubiri bajeti inapopita Waziri wa TAMISEMI aje akague, atuletee hizo *industrial materials*, tumalizie majengo katika uimarishaji sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu limezungumzwa suala la kuimarisha elimu ya *primary*, nao tuwasaidie, nina imani kwamba kama *primary* zitasaidiwa kama inavyozungumzwa katika mpango huu, hayo maisha bora, elimu bora tunayozungumza itaweza kufikiwa. Jambo ninaloshauri kwa Serikali, mpango huu na ningependa nitolee mfano wa Jimbo langu katika Chuo cha Elimu cha Katoke, kuna shule za msingi hazina walimu, lakini kuna vijana wenye uwezo na sifa za kusomea ualimu. Jimboni kwangu kuna Chuo cha Katoke, wanafunzi wanawenza kwenda pale naishauri Serikali, hawa watu wa mipango na bajeti mwongeze uwezo wa kuchukua wanafunzi, ili tuweze kuchukua wanafunzi wengi zaidi hata elfu moja kusudi tuweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la miundombinu, yamezungumzwa mengi kuhusu TANESCO, mimi katika mambo ya miundombinu na nishati nazungumzia suala la umiliki na udhibiti, mimi naunga mkono TANESCO iimarishwe, ipewe uwezo ikishakuwa na uwezo ndiyo igawanywe, jambo la muhimu katika hii miundombinu ni kuidhibiti, tusije tukafanya makosa ya kurudi kule kwa TRL, halafu tukaja tukapigwa changa la macho, hatutakuwa na mtu wa kutusamehe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nazungumzia mambo ya bomba la gesi, tunapoanzisha bomba la gesi nashauri kwamba umiliki, Serikali yetu lazima iwe na mkono ndani yake, suala la mchezo huu ni udhibiti, lazima tuweke macho yetu pale, faida iliyomo ni kwamba mbali na faida ya pesa tunatengeneza trainning ground ya vijana wetu. Unaweza kutengeneza *General Manager* wa Kitanzania kwenye bomba la gesi, lakini ikiwa ya mgeni huwezi kupata fursa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la miundombinu. Nimepitia mpango unaokuja, nimeona miundombinu inayotengenezwa, lakini kwa Jimbo langu na nimeusikia utaratibu wa TAMISEMI, nitaomba barabara zangu za Kishulo, Omurunazi mpaka Bija ziwe *up graded* ziwe za TANROAD kusudi tufikie katika eneo la Burigi ambako kuna ukulima mkubwa wa mpunga na mihogo. Katika kuchangia kwangu naomba nitoe shukurani kwa Serikali na hasa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwatambua wajasiriamali waliokuwa wakifuga samaki katika Jimbo la Muleba, akina Bwana Julius Maforonya na Bwana Bushiri na kuwawezesha nasikia mmoja amepelekwa Vietnam kwenda kuangalia samaki wanaofugwa. Mheshimiwa nakushukuru tuko safarini na umetupa *lift*, tunaondoa umaskini kwa kasi, sera za CCM unazitekeleza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala tata la upakuaji wa mafuta katika bandari ya Dar es Salaam, katika upakuaji wa mafuta kwa sasa, Mtanzania anabebeshwa gharama ya dola 30 kwa kila tani anayonunua, lakini jitihada za kujenga bomba la mafuta hazijawekwa wazi, hatujui shughuli itakwisha lini na haileweki, kwa mwaka mzima, tunapoteza dola 60 milioni kutokana na hii hali. Namwomba Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu hawa watu uwaite kusudi watueleweshe, kinachotakiwa ni mfumo mzima wa kupakua mafuta na tungependa hili suala litatuliwe leo, kusudi hizi jitihada za

mpango huu za kuweza kutengeneza hifadhi ya kimkakati, *strategic reserve* na ununuzi wa jumla, ziendane na kuboresha mfumo wa kupakua mafuta, kinyume na hapo kuna kupigana changa la macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa elimu nirudi nyuma tena, huu mpango ni wetu wote, napenda kutoa rai kwa Wabunge wote, kwa watu wote kwamba, tunapotaka vijana wa sayansi ni wajibu wetu kuanza sisi kuwahimiza watoto wetu na watoto wa jirani kwamba wasome sayansi, nimeambiwa mtu anayepembua almasi analipwa milioni ishirini, nani asingependa mwanae akasome sayansi apembue almasi alipwe milioni ishirini. Kwa hiyo, ndugu zangu huu mpango ni wa kwetu Waheshimiwa Wabunge, ni mpango wa watu wote na ninachoshauri Serikali mtutengenezee kalenda, tunapokwenda Majimboni tuweze kutekeleza Mpango huu kwa kuupeleka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofî*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. FELIX F. MKOSAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kujua kwa sababu kabla ya mzungumzaji aliyejita, Mheshimiwa Kafulila wakati amezungumza, ametaja Wabunge ambao wanakula rushwa. Sasa tungependa kujua wewe unachukua hatua gani na pia tungependa tuwajue kwa sababu hapa ni Watanzania wanaliangalia Bunge zima, sasa hatuwezi tukaacha suala la mtu kutaja kwamba fulani anakula rushwa, fulani amekula rushwa, tuwajue hawa watu ni akina nani na Bunge liazimie sio tuache jambo la msingi kama hili kwa Taifa juu juu tu. Tungeomba Mheshimiwa Kafulila awataje hawa watu na Bunge litoe uamuzi kwa sababu ni jambo la msingi sana kwa Taifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kiti kimekusikia na kwa kuwa umeomba Mwongozo, basi Mwongozo tutautoa katika muda ambao tutaona unatufaa, kwa sababu ni jambo ambalo linalohitaji kulifikiri na baadaye kulifanyia maamuzi, kwa sababu umeomba Mwongozo, basi Mwongozi utatolewa katika muda utakaopangwa. Tuendelee. (*Makofî*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika mada iliyo mezani. Katika kuitia mpango huu, ambao kimsingi ninaupongeza, ningependa kutoa mchango wangu katika eneo la rasilimali watu. Kila tunapozungumza kuhusu wataalam wetu katika nchi yetu kwa kweli kwa kiasi kikubwa huwa napata mshangao, sio kwamba Taifa letu halina wataalam, lakini kinachonishangaza ni namna tunavyotumia wataalam wetu

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi za wenzetu za Kusini mwa Afrika wataalam walio wengi katika fani mbalimbali katika miundombinu, afya, elimu na kadhalika ni Watanzania wenzetu. Inavyoelekea ni kwamba utaratibu wa kuwatumia vizuri pengine haupo wanakata tamaa, wanakimbilia kwenye nchi za wenzetu au inawezekana maslahi duni yanawafanya waende wakatafute mahali ambapo kuna namna

nzuri ya kuweza kujipatia riziki zaidi na ndiyo maana wanasoma vizuri hapa nchini au sehemu nyingine, lakini matokeo yake wanatoka na kwenda kufanya kazi katika nchi za wenzetu ambako wanafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba katika mpango huu, tuangalie namna ya kuweka mazingira mazuri ili badala ya kusubiri tu kutayarisha wataalam wapya, lakini tuangalie na namna wa kuweka mazingira mazuri ili wataalam wetu ambao wanafanya kazi katika nchi mbalimbali au sehemu mbalimbali duniani waweze kushiriki katika mpango mzima wa maendeleo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia, ni kuhusu uwajibikaji. Nchi yetu ina mipango mizuri sana na kila ninavyoangalia ni kwamba inawezekana sana wenzetu wa nchi nyingine, nchi jirani wanachukua sehemu ya mipango yetu na kuitekeleza kwa mafanikio makubwa, lakini ninachokiona ni kwamba namna ambavyo wataalam wetu au Watanzania kwa ujumla tunavyofanya kazi katika kuchangia juhudzi za kulikwamua Taifa letu inatia shaka. Licha ya kwamba muda wa kufanya kazi unaweza ukawa pia ni hoja, lakini tulio wengi ukipita maofisini, sehemu mbalimbali za kazi ni kwamba bado Watanzania hatujawajibika ipasavyo katika muda ambao tunapata kwa ajili ya kuchangia maendeleo na juhudzi za kulikomboa Taifa letu. Kwa hiyo, naomba pia uwekwe utaratibu wa namna ya kutathmini kwamba kila mfanyakazi, kila mtu ambaye anawajibika katika jambo fulani ametenda kazi kadiri ambavyo mkataba wake wa kazi unaruhusu maana yake walio wengi wanafika kazini, wanaaga wanakwenda kufanya mambo mengine na mwisho wa siku mambo yanakwenda kama yalivyokuwa tangu awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia misingi ya bajeti yetu ambayo imewasilishwa wiki iliyopita hapa Bungeni na ukiangalia ile misingi utaona kwamba mpango haukutazamwa kama msingi mmojawapo katika kutengeneza bajeti yetu. Katika ile misingi utaona kuna MKUKUTA, Dira ya Taifa 2005, Malengo ya *Millennium*, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, kuna mkakati wa Misaada na Madeni wa Taifa, lakini mpango wenyewe haupo. Sasa kwa haraka haraka unaweza ukaona kana kwamba kuna kugongana kati ya Wizara na Tume ya Mipango, kitu ambacho kwa maoni yangu bajeti yetu ingetazama zaidi huu mpango jinsi ulivyo na kuundwa kwa mpango jinsi ulivyo ili utekelezaji wa mpango wenyewe uweze kuwa mzuri na uweze kuendana na jinsi ambavyo tunataka. Vinginevyo fedha kwa ajili ya kutekeleza mpango huu kama ilivyoelezwa katika mpango wenyewe itakuwa ni shida sana. Nafikiri ni lazima kwa kiasi kikubwa Wizara na Tume ya Mipango viweze kushirikiana kikamilifu katika kuhakisha kwamba mpango huu umetekelizwa na kwa maoni yangu ningefikiri kwamba mpango huu ndiyo ungeongoza, huu mpango ndiyo hasa ungeangaliwa na vyombo vingine vyote ambavyo vinapaswa vipange utaratibu na utekelezaji wa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika mpango ni dhahiri tunakubaliana sote kwamba ili mpango huu uweze kutekelezwa, tunatakiwa katika nchi yetu tudumishe amani na utulivu uliopo na sana sana tuhakikishe kwamba tunasimama kikamilifu katika Utawala Bora. Amani na utulivu sio kitu cha kusema tu mdomoni, lazima tuhakikishe kwamba sote kama Taifa tumehakikisha kwamba tunatengeneza misingi imara na kila

mtu aitekeleze kuhakikisha Taifa letu linakaa katika amani ambayo imedumu sasa katika kipindi hiki cha miaka hamsini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kulifikia hilo, naungana na wenzetu waliosema, kwa kuwa sasa tuko katika mchakato wa uundaji wa Katiba mpya ya nchi yetu, basi nashauri jambo hili liwe la wazi ili kila Mtanzania aweze kushiriki katika kutengeneza Katiba ya nchi yake na misingi ya Utawala Bora iweze kuonekana imetajwa vyema katika Katiba ili Katiba tutakayopata iweze kutuhakikishia amani na utulivu wa nchi yetu. Narejea kusema tena kwamba, bila amani na utulivu na wale ambao wanafikiria kwamba chokochoko katika jambo hili inaweza ikatusaidia watambue kwamba hata tukiwa na mipango mizuri namna gani bila ya nchi yetu kuwa na amani hawa wawekezaji hawataweza kuja na ku-*invest* katika nchi yetu na matokeo yake mipango yote hii itakuwa ni kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Selasini, anayefuata sasa ni Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed lakini baada ya yechee atafuatia David Ernest Silinde na baadaye Nyambali Chacha Nyangwine. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, karibu.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nakushukuru. Kwanza, niwapongeze wote waliota hotuba asubuhi, Waziri, Mwenyekiti na Kambi ya Upinzani. Kilio cha kuwa na Tume ya Mipango ni kilio cha muda mrefu katika Bunge lako Tukufu. Nakumbuka miaka mitatu, minne Kambi ya Upinzani pamoja na Wabunge wengi na hasa Kamati ya Fedha na Uchumi tulikuwa tukiidai sana kuwepo kwa Tume ya Mipango. Nasema tunafarijika sasa kwamba Tume ipo na tunaamini kwamba mipango sasa itaweza kuratibowi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kufanya kosa siyo kosa, kosa ni kurudia kosa. Tulifanya kosa kuivunja Tume, tukafanya kosa kuwa na Tume ambacho ni chombo kilichosimamia mipango yetu ya maendeleo. Leo tunesahihisha kosa, tusifanye tena kosa kwa makosa ambayo tuliya fanya. Tumeunda Tume hivi sasa, Tume ina watumishi wachache sana. Bajeti ya Tume ilitakiwa iwe bilioni 19, lakini wamepewa kama bilioni nane. Sasa hapa tunarudia kosa, kwamba hiki chombo ambacho kilihitaji kisimamie mipango yetu tumeshakinyima uwezo wa kusimamia, hili ndiyo tatizo kubwa na la msingi la kufeli mipango yetu huko tulikotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *review* waliofanya wataalam kasoro moja waliyoiona ya msingi kabisa ni ile *institutional frame work* ya kusimamia mipango yetu. Sasa hii *institutional frame work* sasa imepima uwezo wa kufanya kazi. Hawana uwezo wa kufanya hata ya *research*. Haiwezekani Tume hii ikawa *efficient*, ikasimamia mipango. Kwa hiyo, kasoro ya mwanzo ni hiyo na ningeomba kabisa tujipe muda wa kulisahihisha kosa hilo ili tusirudie tena kosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ukisoma Katiba, inazungumzia kabisa na Waziri kai-*quote* vizuri tu asubuhi hapa, kwamba pamoja na kwamba Bunge hili tulikaa kama Kamati ya Mipango, lakini inatakiwa vile vile ndani yake lipitishe Sheria. Nakubali kabisa mpango huu unatokana na *vision 2020-2025*. Lakini hapo katikati ikapita hatukufanya tathmini ya mipango wala hatukuwa na Tume ya Mipango. Kwa hiyo, sasa tunapoingia katika awamu hii ni vema tukahakikisha kwamba mpango huu unapita pamoja na Sheria ili atakayevunja utaratibu wa kutekeleza mpango, Sheria imbane na aweze kuchukuliwa hatua. Tatizo hapa ni kudhibitiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile tunapopitia bajeti, halafu tunapitisha *Financial Act* kwa maana ya kwamba tunahakikisha bajeti inatekelezwa kwa mujibu wa Sheria na mpango huu lazima ufuatane na Katiba, huu ndiyo msingi wa kwanza katika kusimamia mipango yetu. La tatu, ukienda katika ukurasa wa 73 tunaelezwa tatizo la *resource gap* na limepanuka sana mpaka linatisha. Wamesema wataalam kwamba tunalo tatizo la msingi la *resource gap* yaani kwamba fedha za kutekeleza mipango yetu ni tatizo, nalo ni la msingi. Nimeona mapendekezo mengi mazuri waliyoyatoa, lakini yanahitaji kusimamiwa. Tulikuwa na wataalam wa Benki Kuu, *World Bank Zanzibar*, kwa Wabunge wa CPA wanaotoka katika Visiwa vidogo vidogo, wakasema fedha nyingi zipo za *climate change* na *environment*. Lakini *we have to navigate in order to gate that money*, lazima uhangaike uzitafute.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Tume yenyewe haina watumishi wa kutosha kuzitafuta hizo fedha siyo rahisi. Kwa hiyo, hili ni tatizo la msingi ambalo tunalikabili mbele ya safari. Kwa hiyo, tatizo la *resource gap* ni kubwa sana na linahitaji kufanyiwa kazi. Sasa mapendekezo yaliyotolewa humu naona ni ya muda mrefu na mengine ukiacha lile la *PPP* kama litafanyiwa kazi vizuri. Kwa hiyo, ilitakiwa Tume sasa hivi ikae, iseme ni miradi ipi itakwenda kwenye *PPP*, miradi ipi itakwenda kwenye BOT na miradi ipi tutafanya wenyewe kama Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo *identification* bado haijafanyika. Ndiyo maana kwa maana hiyo ukiangalia bajeti ya mara hii ukiangalia na mipango hii hakuna uwiano ulio sahihi. Kwa hiyo, ningewomba Mheshimiwa Waziri kauli uliyoitao hapa Bungeni ya kusema huu ni mpango wa kipindi hiki cha mpito, tuchukulie kipindi hiki cha mpito ni cha Tume kukaa kitako sasa, *ku-analyze* na kufanya utafiti mzuri zaidi ili mwakani tuingie tukiwa na *programme* ya Tume pamoja na Mipango ambayo sisi tunafikiri inaweza kutekelezeka. Vinginevyo tunazungumzia kipindi cha mpito tutakuja tena rudi nyuma kuchukua mambo ambayo hayakukamilika na tuje tutoe sababu kwamba tulikuwa katika kipindi cha mpito. Nasema kipindi hiki cha mpito tukae kujitayarisha. Tume itafute *resources*, Tume *i-identify* miradi halafu tujue ipi tunaifanya wenyewe, ipi tunawashirikisha wananchi. Nafikiri hilo ni jambo la msingi sana la kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimepitia suala la *human resources*. Hili ni tatizo kubwa la utekelezaji wa mpango huu. Tunahitaji katika kaliba mbalimbali, si chini ya watu laki tisa. Nikajiliza *Wage Bill* itakuwaje. *Wage Bill* humu hajasemwa kwamba hawa watu tunaotaka kuwaajiri *Wage Bill* yao itakuwaje, itakwendaje na bajeti ambayo tunayo. Nafikiri hilo linataka kutafsiriwa sahihi. Lakini pia limeelezea namna gani

tutapata wanafunzi watakaohitimu katika *field* mbalimbali. Ukiliangalia hilo unaliona ni rahisi. Lakini huyu mwanafunzi lazima awe na mtu wa kumwanda. Kwa hiyo, unapopanua Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, cha Mzumbe na kingine chochote, lazima kuwe na *Lecturers* pale ndani, hawaonekani katika huu mpango. Wanaonekana watu watakaopata elimu, lakini watakaowapa elimu, mpango wao hauonekani. Nafikiri hii ni *shortcoming* kubwa kwamba huwezi kuwaandaa watu wakati hawana watu wa kuwaandaa. Kwa hiyo, nafikiri hayo nayo ni mapungufu makubwa katika suala zima la *human resources*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tano, ni suala la rasilimali. Ukisoma hotuba ya Waziri wa Fedha kuna mahali amesema atawasamehe kodi wale waliokuja kuchimba mafuta. Nasema hii Tume ya Mipango inazungumzia kupunguza misamaha ya kodi kwa *one percent*. Huku Waziri wa Fedha anasema aah wale wanaochimba gesi na mafuta tutawapa tena misamaha. Sasa napata tatizo, hawa watu walipokuja kuwekeza kuchimba gesi walikuja na miradi yao imepangwa tayari, wanajua gharama ya mafuta Tanzania ni kiasi gani. Wanajua gharama za kufikisha mafuta kwenye *site* yao ni kiasi gani, inakuwaje leo katikati wanakuja kuomba wasamehewe kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unatoa tena bajeti unazungumzia watu wale wale uwasamehe kodi. Nasema kuna tatizo la msingi. Hebu tuwe *focused, we are not focused*. Tumeamua kupunguza misamaha ya kodi, ibaki *one percent of the GDP*, tubaki hapo na kila anayekuja atuelewe sera yetu ni hiyo. *If you want to come, come in, if you don't come, go out, serious.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa na *double standard* katika hili na katika eneo ambalo tunapoteza mafuta, hata juzi tumekamata Makampuni ya Mafuta yaliyosamehewa kodi, wanaiza mafuta ndani ya nchi. Wamekatwa juzi tu. Lakini tunaendelea kutoa tena mwanya wa kusamehe kodi. Tusifanye haya makosa. Ni makosa makubwa sana na ni tatizo la msingi tulilo nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Makampuni ya Madini hapa yalianza na bei ya dhahabu ya dola milioni 200. Leo wako 1,500, hawatozwi kodi. Tungekaa kitako tukajiuliza hizi fedha zote hizi acha hivi viposho posho tunavyopata, hii pesa kubwa hii, tunafanyaje kuipata nchini. Nafurahi mpango unasema sasa wataanza kuwekeza pesa ndani ya nchi na kadhalika, watakubali? Maana haikuwemo ndani ya mikataba yenu ya awali. Sasa haya ni mambo lazima ikae Tume iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawili ya mwisho, *resources* ambazo tunaweza kuvuna haraka. Nazisemea tena *resources* za uvuvi, hizi hazihitaji miezi sita, kuna meli 190 zinavua samaki zinaondoka. Wenzetu wa Maldives wamepitisha Sheria pale. Meli yoyote ya kigeni inayokuja kuvua, hakuna kesi, ni kukamatwa na kafilisiwa, wame-preserve marine products zao. Leo wanaingiza watalii milioni moja pale kwa sababu ya marine products zilizopo, *nothing else*. Sisi tunaziacha meli zinavua, zinaharibu mazalia ya samaki halafu tunakuja hapa tunashindwa kuwa-tax watu wale. Hii ni *revenue* ya haraka. Halafu tunawatoza kodi wavuvi wetu wadogo wadogo kwa vifaa vidogo wanavyovitumia. *What are we doing?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni la amani na utulivu. *Success* ya jambo lolote ni amani. Hata katika nyumba mkikaa amani ni jambo la msingi. Tulikuwa Maldives tuliwakuta wenzetu wanaandamana, hii kwetu ni *quite interesting story*. Wao kwa miaka 68 waliondoka katika *GDP per capita* ya *200 dollars*, leo wanazungumzia *three thousand four hundred dollars*. Lakini wao wakiandamana, wanaandamana saa tatu za usiku mpaka saa sita za usiku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikawauliza, mbona nyinyi mnaandamana usiku usiku, wakasema hii *achievement* tulioipata ni kwa sababu kila mmoja alifanya kazi. Kwa hiyo, suala la *management of time* hapa ni *paramount*, hakuna mchezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, hii *programme* yetu ya maendeleo ni ya Taifa, ni yetu sote. Tumeshiriki sote katika kuijenga mpaka tukafika tulipofika. Ndiyo maana leo Mheshimiwa Hamad unakuja hapa unakuta hoteli yetu kitanda chake ni dola 3,500. Wana *capacity* ya kuchukua watalii 24,000 kwa usiku mmoja. *We don't have that in Tanzania*. Lakini kwa sababu sisi tunasema hiki tulichokichuma tukitunze, wao ni Waislam wale, wakimaliza kuswali *Isha* ndiyo wanaanza maandamano yao na Wabunge wao unawakuta pale, wanapiga kelele na askari wamepangana huko, wakimaliza saa nne na nusu wanakwenda kulala, asubuhi wako kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajifunza kitu cha ajabu sana, nikawauliza na nilipokwenda usiku wenzangu walikuwa wamelala, lakini kidogo nikapenya nikaenda kuwaliza. Hivi siri yenu ni nini juu ya hili? Akasema hapa suala la *management of time* bwana siyo mchezo. Tunataka kuhakikisha uchumi wetu haubadiliki kwa sababu *resources* zetu ni chache. Tuna samaki, tuna Visiwa na sisi wenyewe, *nothing else*. Nenda kaangalie na nguo zao zote *a hundred percent* pamoja na *Tsunami*. Nenda kaangalie *capacity* na *service* zinazotolewa katika mahotelii yao, *first class*. Lakini wana *management of time*. Lakini upande wa pili na wa Serikali unasikia. Pale wanapoandamana askari wako hapo, wanatikisana hapo weee! Wakimaliza hawapigwi. Askari anajua *demand* na Serikali inasikia *demand*, *this is very important*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasikia malalamiko kwamba hawa waliondamana, wanaandamana ni kwa sababu tuna kasoro moja, mbili, tatu, wanarudi kwenda kusahihisha. *This is two ways traffic*, ili hao wananchi waridhike na Serikali lazima isikie na itekeleze kilio chao. Kama Wajapan wanapoandamana, Wajapan wakigoma wanafunga kitambaa cheusi. *Management* inajua kama hawa watu wamegoma. Kwa hiyo, hakuna haja ya kupigana wala kuvutana, wanajua kitambaa cheusi kile maana yake watu wamegomea kitu gani. Tunataka na Serikali isikie ili na wananchi waelewe. Lakini nasema *it is two ways traffic*. Nchi hii ni lazima ibaki katika amani ili tupige hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tena, Mheshimiwa Waziri, kwa heshima zote, mpango mzuri sana, unataka kusimamiwa. Lakini unahitaji Tume ijiandae. Naomba sana tukubali mwakani mpango huu uingie katika utaratibu wa mipango yetu. Ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwa mchango mzuri. Maandano usiku siyo mchana, *management of time*.

MBUNGE FULANI: Maandamano daima.

MWENYEKITI: Sasa anayefuatia ni Mheshimiwa David Ernest Silinde.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kuhusu mpango mzima wa mkakati wa 2011/2012 mpaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la Tanzania siyo namna ya kuandika mipango. Tatizo la nchi yetu ni namna ya utekelezaji wa mipango ambayo imekuwa ikiandikwa kila mwaka. Kinachosikika na kinachozungumzwa hata ndani ya mpango huu kimeelezeka. Kumekuwa na mipango ya muda mrefu kuanzia mwaka 1961 wakati tulipopata uhuru. Lakini mpaka sasa ambapo tunafikia miaka 50 tangu tupate uhuru bado ile mipango haijatekelezeka kwa kiwango cha kumsaidia Mtanzania aweze kufaidika na rasilimali za Taifa lake. Wananchi wetu huko waliko hawapendi kusikiliza ni namna gani tuna uwezo wa kuandika mipango. Wanataka kusikiliza viongozi wao wanazungumza ni kwa namna gani mipango hiyo inaweza kuwanufaisha. Maana ya kuwanufaisha iwe zaidi kiutekelezaji na kimatendo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa mara nyingi ni waandikaji tu. Kiuhalisia, ukiupitia huu mpango hauna tofauti na kuurithi ufalme wa Mungu, unaweza ukauona ni mzuri kweli kweli kwamba Watanzania sasa baada ya miaka mitano basi wategemee neema. Lakini tutakuja mwaka 2016, 2017 tutatengeneza mpango mwingine baada ya huu mwingine kushindwa. Hivyo ni lazima tueleze hofu yetu, kwa sababu ni mambo ambayo tumekuwa tukiyaona kadri mwaka unavyokwenda. Mpango umeelezea mambo mengi. Lakini hofu yetu juu ya huu mpango, moja, unategemea zaidi fedha za wahisani ambazo hatujui ni muda gani zitafika hapa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango unagharimu zaidi ya trilioni 42 ambaa karibu trilioni 8.6 kila mwaka. Lakini asilimia kubwa ya fedha hizo ni kutoka kwa nchi wahisani. Ikiwemo mikopo pamoja na misaada mbalimbali. Sasa hapa tunategemea Mpango utakuwa hautekelezeki. Kwa nini? Unapokuwa na mpango unamaanisha kwamba mpango huu una nia thabiti ya kwenda kuutekeleza. Maana yake ni lazima uwe na fedha mkononi ambayo fedha hiyo ni lazima iwe ya uhakika. Lakini fedha ya matarajio, fedha ambayo hauna mfukoni kwako, mpango hauwezi kutekelezeka. Hii ni lazima tueleze ukweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mpango umeelezea hofu yake ni kuwa, Mpango wa mwaka 1981 mpaka 2000 ambaa umeshindwa kutekelezeka. Sababu iliyoandikwa pale ni mtikisiko wa uchumi wa dunia. Kwa hiyo, mtikisiko ukitokea tena 2012, 2013 maana yake mpango tena umekwisha kufa. Sasa haya ndiyo mambo ambayo tunahitaji kwenda kuyazungumza. Sasa je, ikitokea mtikisiko wa uchumi mwaka

2012/2013, je, nini hatima ya mpango wetu? Sasa haya ni mambo ambayo Watanzania tunasema wanahitaji kuyafahamu. Kwa hiyo, hili ni lazima mjue. Pia suala la mpango kutegemea wahisani, ni lazima Waziri husika atueleze ni kwa uhakika gani kwa asilimia 100 kabisa unajua kabisa kwamba hawa Wahisani wataleta hizo fedha na mpango utafanya kazi kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, hofu yetu kwa nini tunakuwa na hofu kidogo na Mpango huu? Marekebisho ya mipango iliyopita, miaka nenda rudi, maana yake Watanzania hawajaelezwa. Huu ni mwaka wa 50 tunatakiwa tuelezwe sasa. Kuanzia 1961 mpango gani ulifanikiwa na ni mpango gani ulishindwa na kwa nini ulishindwa. Tupewe sababu, kwa nini haukuaidisha Watanzania ambao wanaishi katika nchi yao, tunahitaji haya maelezo. Kwa sababu unajua aibu ambayo Taifa hili tunaweza kuipata, tunakwenda kusherehekea miaka 50, lakini hatujaitangaza ile miaka 50 kwa Watanzania wakajua ni nini tunakwenda kumaanisha ndani ya miaka 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunaona aibu ndani ya nchi yetu wenyewe, wakati ukienda nchi ya Ghana wametoka kuadhimisha miaka 50, mwaka mzima watu wanafanya sherehe kuadhimisha miaka 50. Wanaelezea mafanikio, wanaelezea mipango ya mafanikio na mipango waliyoshindwa. Kwa hiyo, ndiyo mambo yanavyokuwa yanakwenda. Lakini sisi hayo tumeshindwa kuyatekeleza. Kukosoana siyo uadui ni suala la kutaka kufikia lengo ambalo linahitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili la marekebisho ndilo ambalo Watanzania tunasema sasa kwamba tumechoka kusikia, kulikuwa kuna MKURABITA, ukaja sijui MKUKUTA wa kwanza. Utakuja wa pili, utakwenda wa tatu. Sijui kulikuwa na MKUMBITA. Ni masuala ya mabadilisho tu ya taarifa. Haya ni mambo ambayo sitaki kuyasikia. Sasa nasema ni sawa sawa na huu mpango wa sasa ni kwamba unamtamanisha mtu kula pilau wakati hata ugali wenyewe hajawahi kuula. Ndiyo kitu ambacho tunakifanya kwamba Watanzania miaka 50 bado hawajafikia yale malengo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alikuwa anahitaji. Sasa mnawaambia bwana, yale ya Mwalimu Nyerere ambayo yalishindwa sasa tunakwenda na haya na hayo yote mara nydingi yanatokana na nguvu za Wahisani, ambao wanatulazimisha sisi twende kinyume na vile ambavyo sisi Watanzania tunahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni lazima lifanyiwe kazi na ni lazima Watanzania waelezwe. Mpango umeweka vipaumbele vitano ambavyo ni vipaumbele vya msingi kabisa kwamba kuna masuala ya miundombinu, viwanda, kilimo, rasilimaliwatu pamoja na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianzie kwenye sekta ya maji kwamba tangu kuanzishwa kwa ulimwengu huu asilimia kubwa ya Watanzania hawajui faida ya maji safi na salama na ndiyo maana vijijini kwetu afya za watu wetu siyo nzuri, wana magonjwa hususan ya tumbo kama taifodi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo mpango unasema utakavyomalizika maana yake kufikia 2015/2016 suala la maji safi mijini itakuwa asilimia 95 na vijijini itakuwa

asilimia 65. Je, tuna uhakika gani kwamba haya malengo yanaweza kufanikiwa. Je, tumetumia vigezo gani kuhakikisha kwamba haya maji yanaweza kufanikiwa ikiwa miaka 50 tumeshindwa. Je, hii miaka mingapi minne iliyobakia tutaweza kufanikiwa? Kwa hiyo, ni lazima tutofautishe, miaka 50 tumeshindwa, miaka minne tutawezaje? Ni miujiza! Ni mambo ambayo tunaona kabisa hayawezekani. Ni changa la macho. Kwa hiyo, sasa ni lazima tuwe wakali ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kwenye kuhusika na suala zima la kilimo. Kilimo kwa kweli ni zaidi ya 80% ya Watanzania kama wa Mbozi kwetu kule Kamsamba na maeneo mengi wanategemea kilimo. Lakini tunaangalia mwaka mmoja tu uliopita kwenye sekta hii katika ugawaji wa pembejeo za kilimo, Serikali imeshindwa kusimamia na watu wamechakachua mbolea zakutosha. Swali langu siku tunafungua Bunge hapa, Waziri alijibu kabisa tumewachukulia hatua; baada ya kuwachukulia hatua ni nini kitakachofanyika? Maana Watanzania wameshakosa pembejeo, wameshakosa mbolea, wamekosa mbegu na vitu vingine. Maana yake mwaka unaokuja tunakwenda kukabiliiana na janga la njaa. Sasa ni mipango ambayo imekuwa ni ya kimaandishi zaidi na wala si kiutekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jamani muwe makini, Watanzania wamechoka, tena wamechoka kusikiliza maneno mazuri, wamechoka! Mjue hili jamani, muwe mnasoma nyakati! Kama mnaweza kusoma nyakati, muwe mnaona sisi tumetoka *University*, moja kwa moja, unashinda Ubunge bila kutarajia! Ni mambo ambayo yalikuwa hayawezekani Tanzania, ina maana hamjui kabisa kwamba wamechoka au ni mpaka Watanzania waingie katika vurugu? Maana wakati mwingine tunasema jamani, amani ipo na tutaendelea kuihubiri amani kwa sababu ndio dira waliyotuachia babu zetu, wazee wetu akina Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ni kitu ambacho tutaendelea kukilinda. Lakini tutakuja kujiuliza je, mafanikio ya amani yako wapi kama watu tumeendelea kulala njaa mpaka leo? Kwa hiyo, tutakwenda tutahoji na Watanzania watachukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kwa uchungu kabisa na wakati mwingine wengine tunajaribu, watu wanalia kwenye...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MWIGULU L.N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti. Natumia Kanuni ya 64 (a), inayoelezea, Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli ambazo zinakusudia kupotosha umma kwa maslahi ambayo hayajulikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa anayeendelea kuongea amefananisha kwamba miaka 50 hatujaweza, kwenye miaka minne tutawezaje *as if* kwenye hivi vitu ambavyo viko kwenye huu mpango, tunaanzia kwenye *zero ground*. Ni kama vile, hakuna kitu kabisa kabisa, kwa hiyo tunafananisha miaka 50 ya *zero*, halafu turuke mpaka kwenye hizi asilimia zilizooneshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa taarifa yake tu, nadhani angerejea pale kwenye ustawi wa jamii na huduma za jamii, ajue vile vitu ambavyo vimeshafanikiwa. Tukienda kwenye upande wa kiustawi, tayari tumeshatoka shule ya msingi tume-*double*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae nimekuelewa. Mheshimiwa Mbunge Mwigulu, alichokisema Mheshimiwa Silinde, amejaribu tu *ku-relate time* na kimsingi anajaribu kujenga vizuri tu hoja yake. Lakini pia wewe ulichokuwa unasema, nadhani ulikuwa unampa taarifa. Kwa hiyo, bwana Silinde kama ni taarifa naona ameipata, tuendelee. (*Makofi*)

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake siihitaji kwa sababu hakusikiliza vizuri. Nimezungumzia suala la maji, nimeweka mfano miaka 50 tumefikia hapa; je, kwa miaka minne kufikia kiwango cha 95% inawezekanaje? Mbona ni masuala ya msingi kabisa ya kusaidia Taifa! Sio masuala ya kutafuta umaarufu wa mtu mmoja mmoja. Mheshimiwa, nafikiri hili uwe makini unisikilize vizuri ninachozungumza ni kwa maslahi ya Taifa hili. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, ieleze Meza.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, na wewe pia. Suala la miundombinu. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la miundombinu, maana kwenye mpango mkakati umezungumzia miundombinu kwa maana ya umeme zaidi, maana hapa tunataka upatikanaji wa nishati ya umeme toshelevu na wa uhakika katika maeneo mengi ya Tanzania. Sasa haya mahitaji, tunasema ni ndani ya miaka mitano. Miaka 50 katika Jimbo la Mbozi Magharibi ni Kata moja tu ndio ina umeme, Kata ya Tunduma, lakini Kata nyine 14 hazijawahi kujua umeme, wao wanachojuwa ni giza, maana hata huwezi kwenda kwenye jukwaa ukamweleza mtu wa Kamsamba kwamba ukinichagua mimi kuwa Mbunge, nitahakikisha kwamba umeme unaweza kufika hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo unamwambia ndani ya miaka minne, maana yake haya mnayoyaeleza, sisi tukirudi kule Jimboni, tutawaambia jamani, Serikali ya Chama cha Mapinduzi kimesema hivi, kuanzia 2011/2012 – 2015/2016 umeme Mbozi utapatikana, maji Mbozi yatapatikana, kilimo kitakwenda kama vile mnavyotaka. Haya wameyasema Chama cha Mapinduzi; maana yake na Mheshimiwa Waziri ambaye ametuletea Mpango huu awaambie kabisa Watanzania kwamba, tukishindwa kuutekeleza huu mkakati Watanzania wawachukulie hatua gani 2015. Hilo ndio suala ambalo nilitaka kulieleza, kwa sababu mipango inapotoka bila kuipa *time limit* na bila kuji-*commit* maana yake ni kwamba, Tanzania haitakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ingekuwa Mawaziri wanasema kabisa kwamba, Mpango ukishindwa tunajiuzulu nyadhifa zetu za Uwaziri, mipango mingi ingefanikiwa au mpango ukishindwa, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi itakubali kuijuzulu yote na kukabidhi Serikali ya Chama kingine ili iweze kuongoza kuhakikisha mpango ule unafanikiwa, nakwambia hii mipango ingekwenda. Naomba kwa mpango unaotarajiw

kufanywa, tuhakikishe kwamba hili linawezekana, mkakati unakwenda, isiwe mtu anaendelea kukaa, anasubiri, kama ujio wa *Jesus Christ*, kama sisi Wakristu tunavyoamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili ni lazima lichukuliwe. Kwa hiyo, changamoto zote tulizozieleza, tunaomba mzifanyie kazi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

MHE. DAVID E. SILINDE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na wote walioshiriki kuandaa mpango huu, bila kumsahau Waziri wa Uratibu na Mahusiano na Viongozi wengine wote katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mimi binafsi ningependa, tunapojadili mpango huu tuangalie zaidi *logic* kuliko ushabiki, hii itatusaidia zaidi. Niseme kuhusu wananchi wa Tarime, pamoja na yote ambayo watu wameyaeneza kule Nyamongo, tunaamini kabisa kwamba kauli yangu kwamba Tarime tutatatua matatizo yetu sisi wenyewe wana Tarime na ninatoa onyo kwa wanasiasa wanaokimbilia Tarime kufanya fujo, iwe mwiko na marufuku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, naamini kabisa kwamba tukiamua tunaweza. Hata Tarime tulipoamua tuliveza na tutaweza tena. Katika kuchangia hoja hii, napendekeza zaidi kwamba tuweke uzalendo mbele, tuweke moyo wa kujituma mbele, tuijali nchi yetu; kwa sababu, tumezaliwa katika nchi hii, hakuna haja ya kukimbilia madaraka au vitu vingine pasipokuwepo na *logic* ya kuwafanya wananchi wa Tanzania maendeleo? Katika kufanikisha jambo hili, najua kabisa kwamba Watanzania tuna nia nzuri ya kuitetea nchi yetu na naamini kabisa kwamba, ndio maana bado Watanzania wanatuamini. Katika miaka 50, tumefanya makubwa na yanaonekana dhahiri. Mtu anayesema hatujafanya chochote kile kwa kweli hata Mungu mwenyewe naamini atamlaani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuunga mkono hoja ya mpango ambayo imewasilishwa na Chama cha Mapinduzi, naamini kabisa tukiamua, tunaweza katika vipengele vifuatavyo:-

MWONGOZO WA SPIKA

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu umewasilishwa kama ni Mpango wa Taifa na sio wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, hausikiki vizuri.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema, Mpango huu umewasilishwa kama ni Mpango wa Taifa na sio mpango wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, Mbunge, anayeendelea kuzungumza alijue hilo. (*Makofi*)

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali ni Mpango wa Taifa lakini mjue kabisa kwamba ni Mpango ulioanzishwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Naomba msijibizane! Mheshimiwa Nyangwine, naomba usubiri. Umeombwa Mwongozo na Mwongozo ni lazima utolewe ndio undelee na aliyeomba Mwongozo na yeye ni kama alikuwa anatoa taarifa tu. Kwa hiyo, kama unaipokea unawenza ukaipokea, kama ndivyo au sivyo, unawenza ukasema na ukaendelea na mjadala, ndio utamu wake.

Mheshimiwa Nyangwine, endelea.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yake hiyo siipokei kwa sababu, mpango huu umewasilishwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi/Kicheko*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji wa hoja anayeendelea inabidi aseme, hapa ni Bungeni, ni Bunge la Watanzania na Watanzania wote wanaskia. Anasema kwamba mpango huu ni wa Chama cha Mapinduzi; tunawaambia nini Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, afute usemi, Mpango umewasilishwa na Serikali ambapo Serikali ina vyama vyote na ni ya wananchi wote. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, kama nimemsikia vizuri, maana pia ninasikiliza. Amesema Mpango huu umewasilishwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, kwa kuwa hili ninalolisema mimi ndilo jibu sahihi, basi Mheshimiwa Nyangwine, endelea. (*Makofi*)

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, vyovoyote itakavyokuwa, narudia kusisitiza kwamba ni mpango ulioandaliwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa idhini yako tunaomba, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tunawawakilisha Watanzania wote na tunazungumza kwenye *serious issue* ya mipango ya nchi. Ningemba tuelekeze huu Mpango kuwa ni Mpango wa Taifa, ni wa Watanzania wote. Tujielekeze huko, tusitoke, tusiyumbe, tukianza kuyumba hapa, huu mpango

hautapokelewa na ni moja katika kasoro tulizozigundua huko nyuma tulikotoka; tusirudie hayo makosa. Ahsante.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nadhani tunapoteza muda wa Bunge bure. Kimsingi tukubaliane tu kwamba na kama nilivyo sema, Mpango huu ni Mpango wa Serikali lakini Serikali yenyewe hii ni ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, pale ni suala la wewe tu kuweka vizuri. Kwa hiyo, tuseme tu kwamba...

TAARIFA

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sio Serikali ya Chama cha Mapinduzi, bali inayoongozwa na Chama kilichoshinda, Chama cha Mapinduzi. Lakini Serikali, nasema... (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hamad, nimesimama naomba, Waheshimiwa Wabunge make. Nadhani tunazungumza kitu kile kile. Mheshimiwa Nyangwine, endelea.

MHE. NYAMBARI C.M. NYANGWINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza kabisa naomba kuchangia katika sekta ya kilimo. Bila shaka naamini kabisa kwamba Watanzania wote karibu 90% ya Watanzania wanategemea kilimo na ina maana kabisa kwamba huu mpango umetambua hilo. Ninachosisitiza ni kwamba tuangalie namna tutakavyoweza kuwarahisishia wakulima wetu waweze kuuza mazao yao na vilevile watakavyoweza kuzalisha mazao ya chakula cha kutosha na tukila na tukashiba, naamini tutapata kufikiri zaidi kuliko kusinzia. Haya yatatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile tuangalie namna tutakavyosimamia kilimo. Tusiangalie kwamba tulime mahindi tu au mchele, mazao mengine yanayostahimili ukame kama vile mtama na mihogo; tuangalie namna tutakavyowasaidia wakulima wetu waweze kulima. Hilo naamini kabisa kwamba tukilifanya hivyo tutaweza kuwasaidia wakulima wetu waweze kusaidia kuchangia pato la Taifa. Lakini vile vile tuangalie namna tutakavyoweza kuhusisha sekta ya kifedha hasa benki, tuweze kuwakopesha wakulima wetu ambao ni 80%, wakikopeshka, naamini uchumi wa Tanzania utakua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie sekta ya madini katika kuendeleza pato la Taifa na hususan katika huu mpango, jinsi madini yalivyo chambuliwa. Naamini kabisa kwamba asilimia ndogo sana ya pato la Taifa linalotokana na madini ni kwa sababu hatujaweka mkazo wa kusimamia zaidi. Maana wawekezaji naamini kabisa kwamba kwa kiasi kikubwa kwa *ku-refer* Mgodi wa Dhahabu wa *North Mara* wa Nyamongo, wamekuwa sio wazalendo, wanadanganya. Hali hii inasababisha mikataba mingi inakuwa ni mibovu ambayo hailinufaishi Taifa. Naamini kabisa kwamba, kwa sababu katika mpango huu tumejadili suala hili, sasa kuna mambo ambayo tunaweza tukayafanya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, ni tuhakikishe kwamba, kabla hatujaingia mkataba wowote ule na mwekezaji, tuangalie huo mkataba utanufaisha vipi wale watu ambao wanauzunguka mgodi. Hususan katika mgodi wa Nyamongo, wananchi wote wanaouzunguka ule mgodi ni maskini sana, lakini tunaona dhahabu kila siku inachukuliwa na baadhi ya watu ambao sio wazalendo, walioingia ubia na ule mgodi, wanatoka kule Nyamongo wanakwenda kujenga Mwanza. Sasa nasisitiza kabisa kwamba, tuhakikishe tunaendeleza uzalendo na zaidi mikataba hii iwanufaishe wananchi wa Tarime na wale wananchi wengine ambao wana migodi nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kabla hatujafanya kitu chochote kile katika sekta ya migodi, tuhakikishe kabisa kwamba wananchi wanalipwa fidia halali. Kuna maeneo ambayo kwa kweli, wananchi wanayalamikia sana kwamba migodi haiwanufaishi kwa sababu mtu analipwa hela kidogo, lakini akishahama anarudi kule kuwa omboomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile eneo la madini liwaendeleze wachimbaji wadogowadogo. Hii itawezekana endapo tutaweka uzalendo mbele zaidi kuliko maslahi ya wawekezaji. Aidha, Serikali ihakikishe kabisa kwamba hawa wachimbaji wadogo wanapoendelezwa tusiwape fedha, tukishawatengea eneo tuwaandae, tuwandalie vifaa na nyenzo za kuchimbia, hii ikiwezekana tutatoa ajira kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda nichangie kuhusu elimu kwa sababu hiyo ni sekta yangu, ambayo naweza kusema kwamba, ninaimudu, lakini naomba nisisitize zaidi katika elimu ya ufundi. Elimu ya nadharia imetusaidia sana kusoma na kuhitimu. Lakini tukielekeza nguvu katika elimu ya ufundi, nina uhakika kabisa kwamba tutaweza kutayarisha watu watakaozalisha zaidi kuliko wale ambao wanahitimu Vyuo Vikuu lakini wanaotegemea ajira na ukienda kuomba ajira unaambiwa uzoefu miaka mitano. Kwa hiyo, tuhakikishe kabisa kwamba, tunajenga vyuo vya VETA katika kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, tuhakikishe kabisa kwamba vile vile tunawasomesha watu elimu ya biashara kutoka ngazi zote za elimu. Pili, kama tunataka kufungua fursa ya biashara katika nchi yetu ya Tanzania, bila watu kuwa na elimu ya biashara naamini kabisa kwamba tutakwama. Lakini cha msingi na cha maana ni kwamba watu wasome biashara na wajifunze namna ya kumiliki fedha halali, hii itawasidia sana kufanikisha suala hili la mpango huu wa miaka mitano. Hivyo tutaweza kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nirudi katika sekta ya miundombinu kama mpango ambavyo unajieleza, lakini zaidi niegemee katika Jimbo la Tarime, ambalo kwa hakika Jimbo hili halina miundombinu ya barabara nzuri hasa barabara za lami. Kuna barabara moja tu, lakini Jimbo kubwa sana linalozalisha mazao ya biashara na chakula. Naiomba Serikali pamoja na mpango huu, tuhakikishe kabisa kwamba tunafanikisha kujenga miundombinu ya uhakika hasa barabara ya lami kutoka Serengeti mpaka Tarime na ile inayotoka Sirari, inapita mpaka katika Kata ya Susuni inakwenda mpaka Mwema, inatoka hapo inaunganisha mpaka Borega, inakwenda mpaka Nyantira

pamoja na Kegonga. Hii barabara ni barabara ya *security* ikiwekewa lami itaweza ku-*compete* zaidi kwa sababu pale ni mpakani, tutaweza kufanikisha. Kwa sababu, ukiangalia nchi ya jirani imeendelea zaidi na barabara yake ina lami, ina umeme na Watanzania bado tunatamani hilo, tukifanikisha hilo tutaleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ihakikishe kwamba, kuna barabara mbili ambazo ni za kutoka Mangucha mpaka Murito kupitia Gibaso, hiyo barabara Halmashauri haiwezi kuitengeneza kwa muda mrefu. Naomba Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Magufuli, aichukue iwe chini ya *TANROAD*. Barabara hii ikichukuliwa ikawa chini ya *TANROAD*, itaweza kuinua uchumi wa Mwana-Tarime. Naamini kabisa kwamba, mahali popote ambapo pana nia, tutaweza. Watanzania tuna mambo mengi sana, tuna matatizo mengi sana yanayotuandama na jambo la msingi na la busara ambalo tutalielekeza ni kwamba tuweke maslahi ya Taifa mbele kuliko maslahi ya mtu binafsi, maslahi ya Chama yatakuwepo lakini maslahi ya Taifa yaye mbele zaidi kuliko maslahi ya mtu binafsi. Tukiyafanikisha hayo tutahakikisha kabisa kwamba *plan* yetu tunayoiendeleza inatimia.

Tanzania hii inapita katika vipindi mbalimbali vya mpito katika historia. Tutumie rasilimali hasa rasilimali watu, watu wengine wanakimbilia nje ya nchi kwa sababu wanalamika kwamba ni maslahi duni, lakini naamini kabisa kwamba ni ukosefu wa uzalendo na moyo wa kujitolea wa kuitumikia nchi yetu. Tujaribu kuwajenga Watanzania ambao watakuwa na moyo wa uzalendo, vilevile watakaokuwa na ari ya kuleta umoja na mshikamano ambao watakuwa tayari kufanya kazi kufa na kupona wakipigania nchi ya Tanzania. Lakini mambo mengine porojo za kisiasa za kupenda vitu vingine ambavyo haviwezekaniki haviwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi narudia kusositiza wana Tarime tuko imara kwa wale watakuja kutushawishi kwamba tusidumishe umoja na mshikamano wetu kwa kuonyesha ushuja, mimi naamini kabisa kwamba tutawashughulikia na hatutawaogopa. Hilo natoa onyo kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja na kuunga mkono mpango wa miaka mitano ya maendeleo ya Tanzania. (*Makof*)

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uzinduzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wote waliowasilisha leo mpango huu pamoja na Bwana Mpango wa mipango. Mimi naunga mkono mpango huu, mpango huu una vipaumbele vya uhakika ambavyo vimepangwa na mtiririko wake unakwenda ukijiafiki wenye kwa wenye. Mpango huu umelenga katika vipaumbele ambavyo kwa kweli kama vitafanyiwa kazi sawa sawa vitamsaidia Mtanzania katika kufikia maisha bora kwa kila Mtanzania. Mpango huu umezungumzia kuhusu habari za kilimo ambayo karibu asilimia 75 ya Watanzania wanakitegemea. Mimi nilikuwa naomba tu kwamba basi katika mpango huu wa utekelezaji, wakulima wadogo wadogo ni lazima

wapewe kipaumbele, umwagiliaji na uboreshaji wa kilimo ni muhimu sana kwa uchangiaji wa maendeleo.

Katika vijiji ambavyo vimeendelezwa na kuweza kuwa na maendeleo wameweza kuchangia maendeleo yao wenye tofauti na vile vijiji ambavyo kusema kweli bado kilimo chake hakijaboreshw. Hata ukiomba mchango ukasema kwamba jamani tuchangie maendeleo basi kijiji kizima kinaweza kikachangia shilingi 10,000. Kwa hiyo, ni muhimu sana kwamba mpango huu uweze kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ambao ndiyo kwa idadi kubwa sana wako vijijini. Lakini mimi naomba pia mpango huu ujikite pia katika kilimo cha ufugaji wa samaki, sasa hivi wanazungumzia uvuvi lakini mimi nafikiri tuzungumzie ufugaji wa samaki, samaki ni kiumbe kinachozaa watoto wengi kuliko kiumbe kingine chochote duniani. (*Makofî*)

Kwa hiyo, kama tutaweza kuwafundisha wananchi ufugaji wa samaki hasa sehemu zile za Pwani ambazo wanaweza kufuga samaki wa aina zote inaweza ikasaidia sana katika maendeleo. Nimesikia katika mpango huu kuna ufugaji wa kuku, lakini nimeona tu chakula kinazungumziwa, kinashushwa na pengine tutaiongea kwenye Bajeti. Lakini nilikuwa naomba pia tuwasaidie akinamama ambao ndiyo wazalishaji wakubwa sana wa kuku wasaidiwe kufuga kuku kwa kisasa ili kusudi kweli iweze kuleta tija na kusaidiwa pia vifaa ambavyo vinaweza kuleta tija ya kuweza kufuga kwa kupata mazao mengi kuliko ilivyokuwa sasa hivi wakati mtu anasubiri mama kuku ndiyo aatamie. Nafikiri kilimo hicho cha kuku sasa hivi kimepitwa na wakati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo siyo tu kitatuongezea tija, lakini pia kinatakiwa kitulete afya bora kwa hiyo, ni muhimu sana tukaangalia namna gani kilimo hiki kitaweza kumpatia tija ya kutosha mkulima aweze kupata afya bora kwake yeye na familia yake na afya bora inaendana na kuweza kutoa mtoto au mfanyakazi mwenye afya, mtoto mwenye afya anaweza akapata elimu bora. Elimu ni muhimu sana ambayo imezungumzwa vizuri sana na mimi naunga mkono kweli kwamba afya na elimu mafanikio yaliyopatikana yaweze kuendelezwa ili kusudi yasije yakarudi nyuma. Elimu na afya ni muhimu sana, nimesema kwa makuzi ya mtoto. Wenzetu nchi za nje huko nchi zilizoendelea akiagiza chakula anaagiza anataka *fish and chips, chicken and chips*, sisi hapa tunasema hebu nipatie ugali na samaki kwamba ugali ndiyo muhimu sana kuliko samaki, nipe ugali au wali na kuku kwa hiyo, mimi nafikiri kwamba kilimo bora kinaweza kikatubadilisha na sisi tukaanza kuzungumza kwamba nipatie kuku na wali, na samaki na ugali. Lakini ukizungumzia kilimo ni lazima uiunganishe na miundombinu kwa sababu ili mtu aweze kupeleka mazao yake ni lazima uweze kuboresha miundombinu, sasa Serikali naipongeza kwa jinsi ilivyoweza kusaidia katika ujenzi wa barabara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi naomba niongelee ubora wa barabara, kwa sababu isiwe tu bora barabara na siyo barabara bora. Barabara zetu nyingine zinajengwa chini ya kiwango, nikichukua mfano wa barabara yetu ya Kilwa - Dar es Salaam imeharibika kabla hata haijaanza kutumika, mifereji iliyopelekwa pembeni, barabara yenye ukiambiwa kwamba imetengenezwa hata katika miaka mitano iliyopita huwezi

kukubali. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema hilo lizingatiwe kwamba tusije tukatumia hela nydingi kutengeneza miundombinu ambayo itaharibika katika kipindi kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya reli nafikiri ni muhimu sana kwa sababu reli ni njia ambayo inaweza ikabeba mizigo mingi kwa wakati mdogo. Kwa hiyo, ni muhimu sana reli yetu imechoka, imechakaa na ya siku nydingi, kwa hiyo, iko haja kabisa ya kuangalia ni jinsi gani tunaweza tukaboresha hizi reli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitaka kuzungumzia maendeleo hasa yakaleta tija...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge unaweza ukahama hiyo *mic* naona ina matatizo.

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Hapa vipi?

WABUNGE FULANI: Hapo sawa. (*Kicheko*)

MHE. ZARINA S. MADABIDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kilimo ni lazima kiendane na usindikaji, sasa kupeleka mazao yetu nje ambapo sisi wenyewe tunaweza kusindika, nafikiri imepitwa na wakati. Kwa hiyo, ni lazima mpango huu uangalie ni jinsi gani itaweza kusaidia kuboresha usindikaji na tunapozungumzia usindikaji ni pamoja na usindikaji mdogo mdogo maana yake tukizungumzia usindikaji mkubwa tu tunakuwa tunawasahau wakulima wadogo wadogo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba sana viwanda vinasaidia kuongeza thamani ya mazao basi ni muhimu na siku ile nilimsikia Mheshimiwa Rais akisema basi tupeleke nyazi au nguo, lakini siyo hiyo tu tuna matunda mengi sana ambayo yanaharibika tu hayafanyiwi kitu chochote tuna mboga mboga wakati wa msimu wa nyanya utasema vile watu wanaweza kufanya mdako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naunga mkono hii hoja lakini suala hili ni muhimu sana usindikaji wa mazao yetu badala ya kuyapeleka mazao haya yakiwa ghafi. Tunapozungumzia viwanda ni lazima uzungumzie umeme, umeme kusema kweli umeturudisha nyuma sana, kwa wale ambao kidogo tuna biashara za viwanda vidogo vidogo hivi wengi sana tulikuwa tumeweka majembe pembeni kwa sababu ya umeme. Gharama ya uendeshaji ni kubwa sana na upatikanaji wa umeme umekuwa mbaya sana, sasa tunapozungumzia maendeleo ya nchi hatuwezi bila kuzungumzia umeme. (*Makofi*)

Mimi naomba nimponeze Mheshimiwa Rais na Serikali yake yote leo timesoma kwenye magazeti kwamba Mheshimiwa Hillary Clinton amesema atatusaidia umeme na tayari ameshazindua mradi wake ule wa *Symbion Power*, basi kama ikiwa utatekelezeka huo na kwamba kama alivyosema kwamba mpaka mwaka 2015 tutakuwa na *Megawatt 3000* kutoka *Symbion* sijui kama na kwingine, mimi nasema hili ni neno la kulikaribisha sana na kulipalilia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nasema kweli nampongeza Mheshimiwa Rais kwamba amekuwa ni baba wa kuhemea, maana yake wengine walikuwa wanasema sema anatoka, anatoka lakini sasa matokeo yake tunayaona ya kutoka. Kwa hiyo, mimi naomba nimpongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumezungumza hapa masuala ya *solar*, umeme wa jua, jua sehemu kubwa sana ya Tanzania tunalo, ni kitu ambacho ni lazima mpango huu ukiangalie kwa undani wake, unaweza kabisa ukajibu maswali mengi sana na matatizo mengi sana ya umeme hakuna sababu ya majumbani kutumia umeme mwingine zaidi ya *solar* (umeme wa jua) kwa sababu ni rahisi lakini upatikanaji wake na uunganishaji wake ni ghali sana. Kwa hiyo, hilo linapaswa kuangaliwa ili kusudi kuangalia sisi hapa kushindwa kutumia *solar* wakati wenzetu Ulaya wanatumia *solar*, haieleweki wakati jua tunalo sisi, wao jua wanalipata kwa msimu. Kwa hiyo, suala la umeme ni suala muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mimi naomba tu nitoe angalizo utekelezaji wa suala zima hili la mpango huu kusema kweli kunahitaji usimamizi mzuri wa kuelewaka na wa kusimamia mipango hii. Maana yake isije kuwa tumepanga vizuri, tunazungumza, lakini mwisho wa yote mipango ile haitekelezeki, tuna tabia ya umangi meza Tanzania, Mkurugenzi yuko mezani, Meneja yuko mezani, Afisa Mradi yuko mezani hivyo hivyo mpaka mtu wa mwisho wako mezani kila mtu anaangalia *figures* zake yupo mezani.

Mimi naomba hilo tuliache, tuinuke na mimi kusema kweli nasema pamoja na kwamba watu wanasema posho, posho hizi lakini hizi posho kwa watendaji wengine lazima ziendelee, wataendaje? Tunawaambia hapa watoke waende wakasimamie na wote hapa tunaafiki kwamba usimamizi ni lazima uwe wa karibu hasa kwenye sehemu zetu za kilimo, mifugo, kwa hiyo, huwezi kumtarajia atembee kwa miguu, lazima aende, kule lazima aende akale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi naomba utendaji hapa unahitajika usimamiwe vizuri sana, mpango huu ukisimamiwa vizuri kwa kweli hiyo mwaka 2025 maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo mimi naunga mkono mpango huu, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi naomba nichukue fursa hii kuchangia kidogo kwenye eneo la mpango kwa sababu tumewasikia Wabunge walio wengi wamechangia mambo mbalimbali ambayo ni ya muhimu sana. Kwa hiyo, sitapenda kurudia sana lakini nina mambo machache ambayo nitapenda nichangie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema kwamba Tanzania tuna bahati ya kuwa na wataalam makini sana hilo halipingiki, tuna wataalam wazuri wenye uwezo mkubwa wa kuandaa mipango mizuri, tatizo liko kwenye utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Kigoma katika Wilaya ya Kasulu. Wilaya ya Kasulu imeanzishwa tangu mwaka 1920, unapotaja Wilaya kongwe ndani ya Tanzania ni pamoja na Wilaya ya Kasulu, lakini mpaka leo ninazungumza hapa Wilaya Kasulu bado ni giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatafuta usawa wa Watanzania, tumeongea mambo mengi kwamba kuna tabaka la maskini, kuna tabaka la matajiri, ni namna gani tutaleta usawa kule, ni lazima Serikali iwe na mpango mkakati kwa nia njema na hasa katika hili ndugu zangu naomba niwaombe sana wale ndugu zangu Wabunge, viongozi mbalimbali wakuu wa Wizara mbalimbali, wakuu wa idara mbalimbali ambao Mwenyezi Mungu amewajalia kupata nafasi hiyo tutende haki kwa wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hii ni mama yetu, Watanzania wote ni watoto wa Tanzania kwa hiyo, leo kama tunajadili umeme wakati mimi tangu babu yangu amekaa gizani kwenye koroboi, baba yangu amesoma kwa koroboi, mimi nimesoma kwa koroboi, mtoto wangu amesoma kwa koroboi mpaka mjukuu jamani. Kwa hiyo, ni wazi kabisa kwamba tuna kila sababu ya kuangalia na kutoa vipaumbele kwa mikoa ile ambayo tunajua kwamba kuna fursa ambazo bado hatujaziwekeza vizuri ili kuleta usawa huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naongea hayo kwa sababu ukiangalia mkoa wa Kigoma, ukiangalia mkoa wa Rukwa, ukiangalia mkoa wa Kagera ni maeneo ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na maporomoko ya kutosha, kuwa na mito mikubwa ya kutosha, ni kwa nini hatuna umeme? Jibu unalipata kwamba hapa tatizo ni viongozi ambao hawana utashi na kupeleka umeme maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nitachangia kidogo kwenye mpango huu na hasa ukizingatia kwamba kinara mkuu aliyeandaa mpango huu na naomba nichukue fursa hii kumpongeza Dokta Mpango ni zao la Kasulu, Dokta Mpango kwa hiyo, ni mpiga kura wangu kwa namna moja au nyingine kwa hiyo, naomba nimpongeze sana na niombe Serikali kwa kazi nzuri aliyoifanya mumuunge mkono kwa kuleta maendeleo Kasulu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kwa maana moja niliyotaja mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera, kwamba tuna maporomoko ya kutosha tumeahidiwa kwa miaka mingi kuunganishwa na umeme wa Gridi ya Taifa kitu ambacho ni ndoto. Ni kwa nini kwenye mpango huu Serikali isiandae mpango wa makusudi wa kutafuta chanzo cha kuzalisha umeme kwenye maporomoko ya maji tuliyonayo, mito tuliyonayo ya Rukwa, Kigoma na Kagera ili tuweke *zone* au kituo cha *TANESCO* katika mikoa hiyo ambayo tunapata umeme wa uhakika wa kuhudumia mkoa wa Rukwa, Kigoma na Kagera na tuna uhakika Serikali ikiamua kutafuta chanzo cha kuzalisha umeme katika mikoa niliyotaja tutapata umeme wa kutosha na chenji tutawagawia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia hayo ninaamini Serikali ni sikivu, kulingana na kilio changu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, naamini Serikali itarekebisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba nichangie kwenye sekta ya kilimo. Historia inajirudia, hakuna ambaye haelewi kwamba Kigoma ni wazalishaji wazuri wa chakula, tuna ardhi nzuri na maeneo ya kutosha lakini kubwa zaidi Serikali kwa kulijua hilo imetuletea miradi mikubwa ya kilimo, tunawashukuru sana. (*Makofi*)

Lakini kubwa ni kwamba naomba Serikali iangalie mikoa hiyo kwa macho mawili hususan Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kasulu ambapo tuna mradi wa Kilimo Kwanza. Mnajua katika ile mikoa sita iliyoteuliwa kuwa ya mfano ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Lakini katika Mkoa wa Kigoma shamba la mfano wa Kilimo Kwanza liko kwenye Jimbo langu Wilaya ya Kasulu. Lakini kitu kinachonisikitisha na naomba Serikali inisaidie katika hilo hasa Waziri wa Kilimo, Kasulu tangu Serikali ya Awamu ya Kwanza ilituletea Chuo cha Kilimo Mbondo, lakini leo Chuo kile kwa sababu ambazo kwa kweli mimi sizifahamu, chuo kile kimebadilishwa imekuwa shule ya sekondari. Sasa mahali ambapo tunazalisha kwa wingi na mnajua kabisa Kasulu tuna historia ya kuzalisha chakula kwa wingi na ndiyo maana miradi ya kilimo iliyo mikubwa inaletwa Wilaya ya Kasulu, ni kwa nini mbadilishe Chuo cha Kilimo muweke Sekondari? Lakini ukija Dodoma Sekondari inabadilishwa inakuwa Chuo Kikuu.

Ndugu zangu, mimi sisemi mengi naweza nikalia, naomba Serikali itusikilize kwa sababu haya mambo ndiyo manung'uniko na hoja za msingi wananchi, tunapiga kelele huko lakini Serikali haisikii mwisho watu wanakata tamaa. Naamini Waha ni wavumilivu na wananchi wa Kigoma pia ni wavumilivu, lakini tunaomba sasa wakati umefika ili mtusaidie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo naomba nizungumzie habari ya barabara lakini sitagusia barabara kwa sababu najua nina nafasi ya kuongea siku mbili au tatu zijazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vitu ambavyo ni vingi katika Wilaya ya Kasulu ambavyo vinatukera, kila kitu ni *zero*, kila kitu ni *zero*, tutaendeleaje? Hata hivyo Mungu anatupenda ndugu zangu, kwa sababu haiwezekani unawaona akina Dokta Mpango wote wanapatikana ni katika mazingira magumu yaani ni mpango wa Mungu. Lakini kama Serikali ingeamua kuwekeza mahali palipo na fursa kama Kasulu na Kigoma, sasa hivi tungekuwa na maisha bora kwa Watanzania lakini maisha bora imekuwa ni ndoto. Wakati umefika na hii ni nusu karne yaani miaka 50, tunapotoka hapa tunataka twende wapi? Na ndiyo maana nina imani kuwa Serikali itanisikia kwamba akina mama tumeumbwa na moyo wa huruma na Mheshimiwa Rais ametoa nafasi na fursa kwa akina mama wengi kuingia Bungeni, inawezekana! Ni wakati muafaka wa kuleta kero za wananchi ili Serikali isikie, inawezekana akina baba wakawa wanaunguruma tu humu lakini hakieleweki. Naomba mnisikilize ndugu zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha, ahsanteni. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Buyogera na anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Alphaxard Kangi Lugola.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuja na mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano kwa muda muafaka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu umesheheni maeneo mengi ya kisekta na majibu mengi katika kutatua kero za wananchi wa Tanzania na kama utasimamiwa na kutekelezwa kama ulivyopangwa Tanzania patakuwa mahali pa kuishi na hapatakuwa mahali pa kukimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 17 kwenye mpango huu, mpango ambao umeandikwa kwa lugha ya kiingereza, ni eneo ambalo limenifurahisha sana kwamba Serikali imejipanga vizuri katika kudhibiti pamoja na kuwajibika kwenye eneo la matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo moja ambalo nimejaribu kulitafsiri kwa Kiswahili naomba ninukuu; “Serikali itaboresha udhibiti na uwajibikaji katika mapato pamoja na mambo mengine imepanga kutazama uhalali na kuondoa posho za vikao na safari ambazo zinatumika kwa sasa.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni wa Serikali lakini kumekuwa na wananci tena wengine ni Wabunge wanapotosha Watanzania juu ya masuala haya ya posho. Wamechukua *agenda* na mpango wa Serikali kujitafutia umaarufu wa kisiasa na ndiyo sababu hata leo naomba uniruhusu ninukuu kutoka katika magazeti haya machache, moja ni Tanzania Daima linasema Zitto achafua hewa, halafu amuandikia Mheshimiwa Spika Makinda kupinga mambo ya posho.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu! Mheshimiwa Lugola hapa tunachangia mpango wa maendeleo wa miaka mitano, hiyo habari ya magazeti na habari nyingine naomba uzitafutie mahali pengine. Nadhani uendelee na mpango wa maendeleo Mheshimiwa Mbunge. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Akasome tena!

MBUNGE FULANI: Hajasoma!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo sababu nilinukuu kuhusu mpango, haya maneno sijayatoa sehemu nyingine bali ni katika ukurasa wa 17. Kwa hiyo, ninapoambiwa kwamba hapa tunajadili mpango na mimi ndiyo ninajadili mpango ... (*Kicheko*)

MBUNGE FULANI: Kama hujasoma kaa chini!

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde kwani najadili mpango katika ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nirekebishe hili ili kuweka kumbukumbu na ili Watanzania wasipotoshwe wakadhani kwamba Serikali haina mpango kama huu ila ni Wapinzani ndiyo wana mpango kama huu. Naomba sasa niende moja kwa moja katika kuupima mpango mzima huu na malengo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwa na mpango ni jambo moja na kuwa na mpango mzuri ni jambo lingine. Kuna mwanazuoni mmoja miaka ya 1980 aliiwa George Dora, katika menejimenti ya kupanga mipango na malengo alitupatia kigezo ambacho sasa hivi tunakitungia Kimataifa kinaitwa *SMARTER* kwamba malengo yaliyopo kwenye mpango ni lazima yakidhi kigezo cha *SMARTER* ndipo itaonekena kwamba malengo haya yanatekelezeka. *SMARTER* maana yake ni *Specific Measurable, Attainable Realistic Time Bound Evaluatable* na *Rewarded*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niupime mpango huu katika vigezi viwili vya *specific* pamoja na *realistic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 116 hadi 119 kwenye mpango huu, tunazungumzia masuala ya maji kwamba tutaboresha ili Watanzania wawe na maji safi na salama. Kusema tu kwamba vijijini ni 65%, miji midogo 57%, Dar es Salaam 75%, mijini 95% huwezi kukidhi kigezo hiki. Watanzania tunatumia maji kwa galoni, kwa siku Watanzania wanahitaji galoni ngapi ambazo ndizo tunahitaji kuzifikia na katika kipindi cha miaka mitano ni galoni ngapi ambazo kwa mfano ukienda Mwibara ukachimba kisima lazima uhakikishe kisima hicho kitatoa galoni ngapi kwa siku kulingana na mahitaji ya wananchi wa kijiji hicho.

Kwa hiyo, kuna tatizo la *performance indicator* kwamba hatujapanga ni galoni ngapi za maji Watanzania wanazihitaji katika kipindi cha miaka mitano na kila mwaka tutakuwa tunatenga fedha kwa kuhakikisha tunazalisha galoni ngapi za maji zinahitajika kwa Watanzania.

Eneo la elimu ni *specific* katika ukurasa wa 145 na kuendelea, tunajenga madarasa lakini hatukuonyesha ni madarasa mangapi yanahitajika, tunajenga nyumba za walimu lakini hatukuonyesha ni nyumba ngapi za walimu tutajenga, tutanunua vitabu na tutatengeneza madawati na kadhalika. Katika mazingira ambayo mpango hauonyeshi kiasi gani cha mahitaji inakuwa ni vigumu sana katika kutekeleza kwa sababu huwezi kupima kwa maana nyingine ile *measurable* kwenye *SMARTER* mpango huu haukidhi. Kwa hiyo, naishauri Serikali iupitie upya mpango huu na uainishe ni galoni ngapi za maji na majengo mangapi katika utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni katika rasilimali fedha kwa maana ya *realistic* kwamba mpango huu ni wa kweli katika kutekeleza. *Realistic* ni pale ambapo tunaangalia upatikanaji wa fedha. Kwa kweli fedha tulizonazo na tutakazoendelea kukusanya ukiangalia na maeneo ambayo yanaainishwa kutakuwa na tatizo la fedha katika kutekeleza mpango huu. Kwa maana nyingine mpango huu unaonekana siyo *realistic*, kwa hiyo, naishauri Serikali ihakikishe kwamba tunakuwa na mpango ambao kwa uwezo wa fedha na hata zile ambazo tunaweza tukakopa ni zile tu ambazo zinaweza zikatekeleza mpango huu, vinginevyo tutakuwa na ukubwa wa mipango lakini hatuwezi kuitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo lingine la kushauri Serikali. Tuna vikwazo vingi katika nchi hii ambavyo baada ya kuanza kutekeleza mpango huu vitakuwa vinapringa mpango huu usitekelezek. Eneo la kwanza ni la utawala bora. Utawala bora una mchango na nafasi kubwa sana katika utekelezaji wa mipango hii. Kwa nini nasema utawala bora na utawala wa Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunazungumzia kilimo katika mpango huu, lakini wananchi vijijini kumekuwa na tatizo la ardhi yao kuvamiwa lakini Serikali inakaa kimya. Watalima wapi katika kuteleleza mpango huu? Mfano mdogo ni Mwibara, kuliwahi kutokea kikundi cha Wanajeshi Mwanza kikavamia eneo la Bunere zaidi ya ekari 200, wanancni watalima wapi? Kama wananchi na vyombo vyenyewe haviheshimu utawala wa sheria na utawala bora, Bulama kuna mwananchi amekuja akachukua ekari zaidi ya 100 je, wananchi watalima wapi katika kutekeleza mpango huu? Lakini Serikali imekaa kimya. Usawa mbele ya sheria, Katiba hii Ibara ya 13 inasema Watanzania wote tuko sawa mbele ya sheria lakini kwa sababu hatuko sawa mbele ya sheria kiutekelezaji ninaamini mpango huu itakuwa vigumu sana kuutekeleza. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatutakuwa na dhamira ya dhati kuhakikisha kwamba yejote anayefanya kosa katika nchi hii anachukuliwa hatua, mpango huu hautatekelezeka. Wapo watu wengi hata sasa wanatusikiliza tunapitisha mabilioni na matrilioni ya fedha, lakini wao wanajipanga kuiba fedha za miradi na fedha za Serikali. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema mtoto akichezea moto unamchoma palepale, akishika wembe unamkata palepale. Kama ambavyo wavuvi katika Ziwa Victoria kule Mwibara, wakikutwa na zana haramu kama kokoro wanakamatwa palepale kwa maana wameshika moto basi sheria inawachoma palepale. Tunataka kuona Sheria ya Manunuzi, maafisa wanapoiba fedha wakagundulika katika *auditing* basi wamechezea moto waungue palepale. Sheria ya Manunuzi iko wazi kwamba atakayevunja sheria katika Ibara ya 87 lazima achukuliwe hatua, lakini wanapovunja sheria wanaitwa wanaambiwa ni udhaifu lakini wamevunja sheria. Kama wanavyofanya doria kwenye Ziwa Victoria kudhibiti uvuvi haramu, tunataka ma-*auditor* wafanye doria za kudhibiti wezi na wawachukulie hatua palepale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wa Mara hautajwi kuwa na mabonde ambayo tunaweza tukamwagilia. Lakini tuna mabonde mengi sana hasa Mwibara ambapo ni Ziwa

Victoria, tuwe na mpango mwingine kama mliouweka Kusini na Kaskazini. Mwibara kuanzia Bunda na Nyatwali, Ngolamba, Kabainja, Namuhula na Nansimo pia kuna mabonde makubwa ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho tuna matatizo kwenye sera ya mapato.....

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge hiyo ni kengele ya pili.

MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana lakini yote hayo yakizingatiwa na kurekebishwa naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Anayefuata sasa ni Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Madelu.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niuzungumzie mpango huu wa maendeleo wa miaka mitano. Lakini kwanza nataka kuwaambia Watanzania kwamba kuna kazi iliyo mbele yetu, kuna *Millennium Development Goals* ambayo yako mbele yetu ambayo tunatakiwa Watanzania na Taifa kwa ujumla tufanyie tathmini mwaka 2015, 2020 na 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika malengo la kwanza kuna lengo la kufuta umaskini ambalo ndiyo tunalizungumzia hapa. Lengo la pili ambalo tumejiwekea ni elimu ya shule za msingi na sekondari yaani elimu ambayo itatoa watu wenye ujuzi na la tatu ni suala la haki za akina mama na kuwawezesha kupata haki zao, ya nne ni vifo vya watoto wachanga na walio chini ya miaka mitano, ya tano ni kuhusu uzazi salama kwa akina mama halafu na suala la mazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo haya ya *millennium* ambayo yapo mbele yetu ni lazima yatekelezwe. Sasa tutapata wapi pesa ya kufanya kazi hiyo? Mimi nashukuru mpango huu kwa kuweka vipaumbele vichache, haiwezekani tukaendeleza vitu vyote na nchi yote tukavipa umuhimu na hela za kutosha. Tuangalie nchi moja kwa mfano Uhlanzi, nimekuwa naangalia wenzetu walivyoendelea, mwaka 1946 walikuwa wanafanana na sisi. Nchi ndogo ina maili za mraba 36,000 ukilinganisha na maili za mraba za Tanzania 900,000 yaani Uhlanzi inaweza kuingia hapa Tanzania mara 25, lakini walitafuta vipaumbele vitatu. (*Makofi*)

Kwanza walijenga bandari Rotterdam, wakajaribu kuondoa maji, wakajaribu ku-reclaim ardhi kutoka baharini wakajenga bandari nzuri sana ambayo meli kubwa kutoka Brazil zenyetani 460,000 zinaweza zikafika pale. Walivyofanikiwa hilo wakajenga uwanja wa ndege Amsterdam na wakaimarisha ndege zao ambazo zinaruka duniani kote sasa hivi. Kipaumbele cha tatu kikawa ile gesi yao kule Kaskazini ambayo wanaipeleka Ujeruman, wanaipeleka Uingereza na Ubelgiji. Kwa hiyo, ni vitu vitatu tu ambavyo walivipa vipaumbele kuanzia mwaka 1946 sasa ni kama miaka 64, leo Uhlanzi ina uwezo wa kutusaidia sisi Watanzania na nchi nyingine za dunia ya tatu. (*Makofi*)

Kwa hiyo, na mimi nilikuwa nafikiri kwamba huu mpango umekuja wakati muafaka, ni kweli tumechelewa lakini lazima tuanze. Mimi nimeshukuru kipaumbele cha kwanza umesema ni kuhusu miundombinu na tukazungumzia Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam ina uwezo wa kutengeneza fedha za kuweza kuendeleza nchi hii kwa mambo mengi kwa sababu kuna nchi kama nane zinazotuzunguka zinahitaji kutumia Bandari ya Dar es Salaam na reli ya kati, tukiimarisha reli ile mizigo yote inayokwenda katika hizi nchi ambazo hazina bandari, hazina reli tunaweza tukapata fedha nyingi katika kipindi cha miaka mitano tukaondoa umaskini tuliouelezea kwenye *Millennium Development Goals*, tukasomesha watoto wetu, masuala ya vifo nya akina mama, vifo nya watoto chini ya miaka mitano na wamama wetu wakajengewa mazingira mazuri wakati wanajifungua, tunaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo la kwanza, kwa hiyo, naliunga mkono masuala ya kuwekeza kwenye miundombinu hasa ya Kitaifa, lakini hata mimi nimefurahi sana kuona jimbo langu litakavyonufaika na huu utaratibu wa kujenga barabara. Tumejenga barabara ya Mwika kwenda Kiracha pale Himo nzuri ya lami, barabara vijijini Mwika kuja Marangu Mtoni barabara ya lami, na katika kipindi cha miaka mitano kuna barabara inayoanzia Kawawa kwenda Kirua Vunjo Magharibi, kwenda Kilema Kaskazini mpaka Marangu Mtoni, ni barabara za lami za vijijini ambazo zitaleta maendeleo makubwa sana kule Vunjo, kule Mkoa wa Kilimanjaro. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia barabara za changarawe siwezi kuacha kukumbusha barabara ya Kilema Pofa kwenda Kilema Hospitali au Uchira kwenda Kirua Vunjo Mashariki. Hiyo ni miundombinu kwa hiyo, lazima niunge mkono mpango huu kwa sababu una manufaa kwangu na kwa wananchi wa Vunjo, na kwa wananchi wa Kilimanjaro hasa ukija tena kwenye kilimo, leo nilikuwa naongea na Waziri wa Kilimo hapa naomba mnapoimarisha kilimo muangalie kule ninakotokea, mkishafanikiwa pale ndiyo mmefanikisha Tanzania nzima. (*Kicheko*)

Kwa mfano, Waziri alikuwa ananiambia mwezi wa tano wadau wa zao la Kahawa wamekaa wakazungumzia namna ya kuimarisha zao lile, na nilitaka niwaambie wananchi wa Kilimanjaro, kahawa AA ile *grade* ya kwanza kabisa kilo moja ni shilingi 8,000 hajawahi kutokea katika historia ya nchi hii, kwa hiyo, mkulima anaweza kupata bei ya ile Kahawa kavu bei yake ikawa kati ya shilingi 3,000 mpaka 3,300.

Kwa hiyo, ninachotaka kuiambia Serikali kama Kahawa ya Brazil imeungua moto na tunaambiwa bei ile itakuwa angani kwa muda wa miaka 25 itakuwa kwenye bei ya shilingi 8,000 kwa kilo na kuendelea mbele haturudi nyuma, kwa hiyo, ni lazima Serikali kama mlivyo sema mnatoa kipaumbele kwa kilimo, mtusaidie watu wa Kilimanjaro tuweze kupata miche mizuri ya Kahawa, tuweze kupanda miche ambayo katika miaka miwili, miaka mitatu inaweza ikaza tukapata fedha tukazihamishia katika maeneo mengine ambako hakuna zao la kudumu kama lile la Kahawa. Hilo limenifanya nifurahie huu mpango, niuone ni wa maana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili mmezungumzia mazao ya chakula na mkataja Mahindi na kule kwangu Ukanda wa Juu kuna Mahindi, kwa hiyo, lile zao la Mahindi tukiweza tukapata pembejeo na mambo mengine ina maana watu wangu watajitosheleza kwa chakula na Mahindi mengi tutauza nje na yana soko zuri sana, wenzetu wa jirani wanapeleka Somalia na Sudan ya Kusini, kwa hiyo, tusaidieni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya tatu mmezungumza habari ya Mpunga, na mimi kule kwangu kuna eneo zuri sana la Mpunga. Kahe ya Tambarare, Kahe Mashariki, Kahe Magharibi na kumbe Wajapani walikwishakuja pale Chekereni wakatusaidia sana umwagiliaji lakini haujatosheleza, lakini kama zile kata tatu; Kahe Mashariki, Kahe Magharibi pamoja na Makuyuni Serikali itawekeza kama ninavyoona kwenye mpango ina maana wale watu wangu watapata chakula cha kutosha na tutapata ziada ya kuza nje. Katika mpango huo yapo mambo mengi ambayo wenzangu wameyataja mengi tu lakini jambo ambalo nilitaka nimalizie kwamba pamoja na vipaumbele mlivyovitoa ninachoomba kama mnataka mpango ule ufanikiwe, tuangalie suala la amani na usalama wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila amani na usalama tutatibua kila kitu *it takes two to tangle*, kwanza naomba nianze na Serikali ambayo ndiyo mna dola, mimi ninachoomba ni kwamba m jitahidi sana kujenga mazingira mazuri. Kama watu wanataka Katiba mpya wape, msiwacheleweshe, kama watu wanataka Tume Huru ya Uchaguzi angalia uwezekano wa kupata ile Tume ili kujenga mazingira mazuri, nchi yetu isiwe na fujo na wananchi na sisi vyama vya siasa nataka pia tuonyane, tuambizane ukweli kwa sababu ukiangalia katika nchi nyingi za Kiafrika uchaguzi unakuwa na mgogoro mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1995 nilivyogombea mimi nilikuwa na nguvu sana, nilipata kura 1,800,000 au 28% ya kura zote, mwenzangu Mwanawasa wa Zambia alipata kura kama hizo akawa Rais, mimi sikupata Urais na hakuna mtu aliye kuwa anapendwa kama mimi, nilikuwa nabebwa, gari linasukumwa, akina mama wanabitandikia khanga lakini sikutumia umaarufu wangu kumhujumu Rais aliye kwenye madaraka, wala sikutumia umaarufu wangu kutaka watu wanisindikize kwenda Ikulu, sikufanya, nataka tujifunze hata watu wanavyolinganisha Tanzania na Libya. Kule Libya Muammar Gaddafi amekaa kwenye madaraka miaka 42, nani Rais hapa ukimuondoa Mwalimu Nyerere amekaa miaka 23? Mwinyi miaka 10, Mkapa miaka 10 na Rais Kikwete miaka mitano hii ikiisha biashara inaisha anaenda zake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tukubaliane na demokrasia, naomba Chama Tawala na Serikali muimarishe demokrasia lakini tusitumie demokrasia kama kisingizio cha kumpiga ngwara Rais aliye kwenye madaraka. Tumpe muda amalize muda wake, hata kama siitaki CCM lakini sikubaliani na mpango wa kuipiga ngwara CCM, tingojee tuwatafute mwaka 2015 ndiyo tuwaondoe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nilisisitize hilo kwa sababu naona tunakotoka na tunakoelekea ni kubaya. Halafu na wananchi tuwafundishe, ukiangalia wananchi wa

mwaka jana mimi waliniudhi sana, kwa kweli walijiandikisha wapiga kura milioni 20 lakini walioenda kupiga kura ni milioni 8, hao milioni 12 walienda wapi?

MBUNGE FULANI: Tume!

MBUNGE FULANI: Ndiyo uchakachuaji huo.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Sijui kama ndiyo uchakachuaji, lakini tunao ushahidi watu milioni 12 hawakwenda kupiga kura, lakini watu hao ukiwaambia tufanye maandalamanu wako tayari kukimbia barabarani, ukiwaambia wakapige kura kwa nini tusianzishe maandalamanu ya kwenda vituoni kupiga kura watu hao? Kama wanataka *TLP* ishinde kwa kuipigia kura, CHADEMA washinde kwa kuwapigia kura, Dokta Slaa ashinde kwa kumpigia kura, watu lazima tuwafundishe hivyo, tusipowafundisha tunakuwa na mpango kama huu unakuta muda mwangi watu wanatembea barabarani, watu wanafanya maandalamanu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali maandalamanu ni haki ya Kikatiba, mikutano ya hadhara ni haki ya Kikatiba lakini huwezi kuwa na maandalamanu ya kila siku jamani, kila kukicha. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Maandalamanu ni haki ya Kikatiba pia.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Watu watalima saa ngapi? (*Makofi*)

MWONGOZO WA SPIKA

MWENYEKITI: Mwongozo wa Spika!

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tulipoanza kujadili ulimzuia Mbunge mmoja kwamba hapa tunazungumza mipango ya maendeleo ya nchi yetu, hatuzungumzii maandalamanu.

MBUNGE FULANI: Hatuzungumzi maandalabu hapa, Katiba inaruhusu kila chama kufanya maandalamanu kwa mujibu wa sheria, sasa Mheshimiwa Mrema anazungumza maandalamanu ambayo CHADEMA tunafanya kwa mujibu wa Sheria.

MBUNGE FULANI: Ulinzi na usalama.

MBUNGE FULANI: Kama hana uwezo wa kukusanya watu hilo ni kosa lake yeye.

MBUNGE FULANI: Ulinzi na usalama!

MBUNGE FULANI: Hamna hicho.

MBUNGE FULANI: *Point.*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge...

MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA: Kazi watafanya saa ngapi?

MWENYEKITI: Jamani hii miongozo maana sasa inaombwa kiholela mno, mwongozo ukiombwa ni lazima useme ni Kanuni gani imekiukwa. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: *Message sent!*

MWENYEKITI: Lakini kwa kuwa tulianza hivyo na kwa sababu Kanuni inayotoa fursa kwa Mbunge kuomba Mwongozo inajulikana, sasa imekuwa ni kama utaratibu wa kawaida, lakini siyo utaratibu mzuri.

Mimi nilivyomuelewa Mheshimiwa Mrema ni kwamba yeze anajaribu kusema kwamba hatuwezi kuwa tuna harakati kila siku wakati tuna mpango, kwa hiyo, bado anausemea, hajatoka nje ya mada. Lakini bahati nzuri sana kama nimempsikia vizuri hakutaja chama wala mtu yejote, kwa hivyo naomba sana Waheshimiwa Wabunge tuendelee, Mheshimiwa Mrema endelea. (*Makofi*)

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mimi ni tahadhari tu ninayoitoa ili nchi yetu isije ikageuka ni nchi ya fujo, ni nchi ya vita kila siku, mimi nasema tukiishakubaliana na huu mpango mimi sikatai maandamano mtu yejote anayetaka lakini na maandamano katiba inaruhusu, hata mikutano ya hadhara katiba inaruhusu lakini ninachosema haiwezekani yakawa maandamano ya kila siku, kila kukicha. (*Makofi*)

MJUMBE FULANI: Mkakati wetu wa chama.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, taarifa.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Kanuni ya 64 (a) Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sijawahi kuona wala kusikia kwamba katika Tanzania kuna maandamano kila siku, sijawahi kusikia hiyo. Sasa huyu Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba kuna maandamano kila siku, atuambie jana na juzi maandamano yalikuwa wapi? (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: *UDOM.*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu, ulichokiomba kupitia Kanuni hii umetoa taarifa, kwa hiyo Mheshimiwa Mrema ana haki ya kuipokea au kuikataa, Mheshimiwa Mrema endelea. (*Makofi*)

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Nimeikataa.

MBUNGE FULANI: Alikuwa anaandamana na yeye.

MBUNGE FULANI: Lakini ujumbe umefika.

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kutahadharisha ni kwamba hii nchi ni yetu wote na huu mpango kama tunataka ufanikiwe ni lazima tuunge mkono kwa sababu huu mpango ni wa Kitaifa, ni wa watu wote, hauna chama cha siasa wala hauna kabilia, wala hauna dini ni mpango wa Taifa.

Sasa kama tunataka tufanikiwe ninachotaka tuseme kama una matatizo katika nchi kuna namna ya kuondoa matatizo yetu wala mimi sijakataza kwamba kusiwe na demokrasia, na ninasisitiza demokrasia lazima iwepo lakini ninachotaka kusema ndugu zangu haiwezekani, hata leo Chuo Kikuu cha Dodoma hapa kulikuwa na maandamano watu wameumizwa, sasa kama kuna *agenda*...

MBUNGE FULANI: Walipwe hela zao.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

MWENYEKITI: Mwongozo Mheshimiwa Makamba.

MHE. JANUARY Y. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba chonde hii tabia ya Mheshimiwa Mbunge anazungumza, mwingine anazungumza chini chini, inalishushia hadhi Bunge letu, naomba Mwongozo wako kwamba kwa kweli tuikemee wote tabia hii, tuiache, ahsante sana. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kunakuwa kuna minong'ono ya chini chini hasa inayohusu maelezo au hotuba ya mtu anayehutubia Bunge, sasa mimi nilikuwa nadhani imekuwa kama unataka kuwa utaratibu, tuchukue tu mawazo hayo mazuri na kwamba sisi kama Wabunge ambao tunaheshimika sana na wananchi wanatazamia kwamba tutatumia fursa hii ku-addresss matatizo yao basi tutoe fursa ya watu kutoa mawazo yao bila kukerwa kerwa. (*Makofi*)

Lakini unapokuwa na Bunge la Vyama vingi lazima utarajie mambo fulani ambayo yatahusiana kati ya pande mbili, kwa hivyo, tuwe wavumilivu, tuyumiliane lakini tuendelee kuzungumza masuala ya wananchi, Mheshimiwa Mrema endelea. (*Makofi*)

MHE. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, muda umeisha na mimi nitakaa chini na naunga mkono hii hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Mrema, anayefuata sasa ni Mheshimiwa Mwigulu Madelu, atafuatiwa na Mheshimiwa Pauline Gekul na baadae Mendrad Kigola.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yake kwa kutuletea mpango huu Watanzania, kwa kweli ni mpango ambao unatoa majibu mengi sana ya matatizo yaliyokuwa yanalikabili Taifa letu kwa wakati huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana halisi ya mpango huu inasema kufungulia fursa za ukuaji wa kiuchumi wa Taifa. Kwa kweli kwa yeote mwenye mapenzi mema na Tanzania hawezi akachukulia kinyume chake dhana ya mpango huu kwa kila mtu wa Tanzania hii. Nimekuja kujifunza kwamba upotoshaji nao ni kipaji. (*Makofi/Kicheko*)

Kwa mtu wa kawaida hawezi akafikia ngazi ya upotoshaji ambayo nimeanza kuona katika kipindi hiki na kutokujali *agenda* na kuhamia kwenye *agenda* ambazo si za msingi. Mfano mmoja niliouona hata leo kwenye *paper* moja iliyotolewa hapa mtu anasema kwa nini rasimu hii imesainiwa? Jamani hii *paper* imetoka kwenye Tume, Mwenyekiti wa Tume hii ni Rais na Dokta Mpango ni Katibu wa Tume hii, kwa hiyo, rasimu hii imetoka kwenye hii Tume, Mwenyekiti wake na Katibu wake wamesaini, mtu anahoji hivi kweli taasisi kama Bunge inaweza ikajadili *document* haijasainiwa, inaelealea tu kweli? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ngazi hii mimi hata kadi ya mchango wa harusi napewa imesainiwa, ndiyo najua kuna harusi.

TAARIFA

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Tundu Lissu.

MHE. TUNDU A. M. LISSU: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa chini ya Kanuni ya 64(1)(a), Mbunge hatatoa taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Jakaya Kikwete ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, siyo Mwenyekiti wa Tume ya Mipango, amesaini huu mpango wa maendeleo wa miaka mitano kwa nafasi yake kama Rais wa Jamhuri ya Muungano siyo kwa nafasi ambayo Mbunge huyu asiyejua anataka kusema Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Tundu Lissu kwa kuwa umetoa taarifa nadhani uliyekuwa unamtaarifu ni mzungumzaji aliyekuwa anazungumza, lakini kwa faida ya Watanzania ni vizuri tukaweka vizuri jambo hili.

Rais wa nchi yetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa nchi hii yaani ana vyeo vingine vingi vinavyotokana na nafasi yake hiyo na ndiyo maana pia katika Tume hii yeye pia ni Mwenyekiti wa Tume hii. (*Makofii*)

Sasa kwa kuwa ni Mwenyekiti na Bwana Mpango yeye ni Katibu, kusaini mipango hii au hii rasimu ni haki yake kabisa, ni sawasawa kabisa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge taarifa yako imechukuliwa na ana uwezo wa kuikubali au kuikataa, lakini kwa faida ya wananchi Mheshimiwa Rais pia ni Mwenyekiti wa Tume hii ya Mipango. (*Makofii*)

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. MOSES J. MACHALI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge samahani naomba ukae. Jamani kama kweli tuna nia ya kutaka kuleta michango itakayosaidia, nadhani hii miongozo inaweza isitusaidie kuliko mambo tunayoyajadili. Tusiwe na Bunge la Miongozo, tuwe na Bunge ambalo tutapeleka michango itakayosaidia Serikali iweze kuchukua michango ya Wabunge. Naomba nikuruhusu uombe huo Mwongozo, lakini jamani naomba tusifanye miongozo kuwa ndio shughuli ya leo.

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kurejea na kuangalia taarifa hii chini ya mpango huu na jambo ambalo lilikuwa linazungumzwa na Mheshimiwa Mbunge Tundu Lissu alikuwa anajaribu kupotosha. Yeye anasema kwamba kuna baadhi ya watu, Waheshimiwa Wabunge kwamba wanapotosha japo hajawataja. Lakini naomba niseme kwamba yeye anapotosha kwa sababu lugha iliyotumika hapa inaonekana kabisa kwamba Bunge limeshirikishwa katika kuja kufanya *finalisation of this plan.*

Sasa kwa kuwa yeye anajaribu ku-*challenge* taarifa iliyowasilishwa na Kambi ya Upinzani. Anasema Mheshimiwa Mbunge kwamba anashangaa kuona watu wanapotosha, lakini yeye ndio ambaye anajaribu kuweza kuwapotosha Watanzania ambao wanatuangalia hivi sasa kwa sababu naomba ninukuu sasa hapa panaeleza namna gani, "*I recommend all stakeholders for invaluable contributions, leading the finalisation for this plan. Specifically I applaud the law played by the Cabinet, Parliament, Ministries, Departments and Agencies.*" Naomba niishie hapo.

Sasa Mheshimiwa Mbunge anachojaribu kuweza kutuambia anataka kutudanganya sisi na sisi lugha tunajua na Watanzania wanaotuangalia pia wanatambua lugha hii. Naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Spika juu ya upotoshaji ambao

unafanywa na Mheshimiwa Mbunge ambaye alikuwa *challenged* Mheshimiwa Tundu Lissu na atutake radhi Waheshimiwa Wabunge. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge huo Mwongozo unaoutaka bwana, nadhani unataka kitu ambacho unajua kikoje kwa sababu kimsingi ulichokisoma hapo ndicho kilichotokea. Kwa sababu Kamati za Bunge zimeshirikishwa sana katika uuandaji wa mpango huu na Bunge linafanya kazi zake kwa kutumia Kamati zake. Kamati ikifanya kazi ni Bunge limefanya kazi. Tunacholetewa hapa sisi leo ni tuendelee kujadili ili kuboresha kama tunavyofanya katika sheria na katika Miswada ya kupitia masuala ya fedha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge Mwongozo wangu ndio huo, Mheshimiwa Mbunge endelea.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, nazikataa taarifa zote na nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge kwamba hili ndilo tatizo la kukosa *continuity*. Wakati Mheshimiwa Rais anahutubia Bunge hili alipokuwa anazindua Novemba 18, 2011 aliyelezea hapa hapa Bungeni wao walikuwa wametoka na hawakufuatilia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo aka-*institute* kwa utaratibu unaohusika kwamba Kamati zitoe michango yao na tumefanya vile ndio maana Mwenyekiti wa Kamati ametoa mchango wake, ameelezea tuliyokuwa tunayafanya. Kwa hiyo, hiki kilichofanyika nilichosema, *I maintain* kwamba watu waepuke kupotosha, wanatakiwa wazingatie kwamba huu ndio utaratibu ambao unatakiwa utumike, unatoa *document for reference*, lazima iwe signed. (*Makofî*)

Baada ya kuwa nimesema hayo niendelee kwa kupongeza kwamba vipaumbele vilivyotolewa kwenye huu mpango kwa sehemu kubwa vimefuata michango ya Wabunge wakati tunajadili hotuba ya Mheshimiwa Rais ya Ufunguzi wa Bunge hili. Tuliletewa vipaumbele vilikuwa vingi tukaainisha sisi humu tuliokuwa tunatoa michango kwenye ile hotuba ya Mheshimiwa Rais, lakini pia vimetolewa kutoka kwenye *documents* ambazo tayari zimeainishwa pale ambazo sitapendelea kuzisemea. Kwa hiyo, kwa kweli mpango huu ni mpango ambao ni wa muhimu sana kwa Taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yameelezewsya lakini tukienda kiutalaamu, kiuchumi tunaona kwamba majibu mengi ambayo yamekuwa yakilikabili Taifa. Moja ya matatizo ambayo yamekuwa yakilikabili Taifa letu kwa upande wa uchumi ni ule uchumi mkubwa kutokwenda kuwa *translated* kwenye maisha ya kawaida ya wananchi wa kawaida wa Taifa hili.

Sasa kwa jinsi mpango ulivyoainisha inaonesha dhahiri kwamba kwenye kile kipato ambacho tumekuwa tukiongelea kuondoa umaskini kunahuisha vipato vya aina mbili, kuna kipato cha mfukoni kwa mtu mmoja mmoja, lakini pia kuna kipato cha kiustawi yaani kuondoa umaskini kufuatana na kuboresha ustawi katika huduma zinazotolewa. (*Makofî*)

Sasa ukienda kwenye kilimo ni dhahiri kwamba tunapokuwa tumeboresha Kilimo Kwanza kinaajiri watu wengi sana na kinapokuwa kinaajiri watu wengi na kwa namna ambavyo imeoneshwa kitakavyokuwa kimeboreshwa kwenye huu mpango inaonesha ni dhahiri kwamba wananchi wengi watapata kipato na kupunguza umaskini. Lakini pia tumeona kwenye maji, maji ni tatizo kubwa sana linalorudisha nyuma maendeleo ya wananchi kwa namna ya kiustawi pamoja na kipato. Sasa kwenye huu mpango inaonyesha ni dhahiri kiasi gani ambapo wananchi wetu wataweza kufaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna upande wa umeme na nishati, mpango umeonesha dhahiri na hili ongezeko tutakapokuwa tumepata hizo megawati inaonesha wazi kwamba kwanza bei za bidhaa zitakuwa zinashuka, kupanda kwa gharama za maisha kutakuwa kumedhibitiwa, lakini uzalishaji utaongezeka kwa sababu kama msemaji aliyetangulia kwamba kuna viwanda vidogo vingi sana vinavyotegemea nishati na punde nishati inapokosekana huwa vinapunguza uzalishaji na vingine kufunga kabisa uzalishaji. Kwa hiyo, kwa kudhibiti tatizo la umeme, uzalishaji utaongezeka lakini pia tutakuwa tumepanua kwenye hilo tatizo la upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia mpango huu unaelezea kuhusu *human capital development*. Hii ni sehemu nyingine ambayo ni nyeti sana na katika huu mpango umeonesha mahusiano ya sekta katika kuongeza uzalishaji kwenye viwanda vidogo vidogo, kuongeza thamani ya uzalishaji, lakini pia umeelezea viwanda vya usindikaji.

Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba unapoongeza udahili kwenye vyuo uzalishaji wa *human capital development*, hawa watu hawawezi wakarudi katika shughuli ya kilimo unategemea wataenda kwenye viwanda. Kwa hiyo, tunapoongeza huko unaona muingilio wa kisekta ambao umeoneshwa na huu mpango. Lakini pia uzalishaji wa kijiji ni utakuwa umetengenezewa soko tutakapokuwa tumeboresha usindikaji. Kwa hiyo, niwaambie Watanzania kwamba hii ni ahadi nzuri sana kwani maisha yao yataboreshwa na wataweza kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la elimu na afya limeelezewa hii ni sehemu ya kupunguza umaskini kiustawi kwamba hata kama una kipato kikubwa kama hauwezi ukazipata huduma, huwezi ukaongelea kuboresha maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimalizie vipengele viwili ambavyo ni vya muhimu nikianza na kile cha vijana. Mpango huu umeelezea kwa vijana, mimi niishauri Serikali kwenye hili Mheshimiwa Waziri asikilize kwamba kwenye hili la vijana tunatakiwa tubuni utaratibu mpya.

Kwanza vijana wanatakiwa watengewe fungu lao maalum. Ulitokea mfuko uliokuwa unajulikana maarufu kama *JK billions*, lakini utekelezaji wake haukuwafikia vizuri walengwa. Kwenye huu mpango iwekwe sheria ambayo kutakuwepo na mfuko maalum kwa ajili ya vijana na kila Halmashauri iweze kulea vile vikundi kwa upande wa vijana walioko kwenye Halmashauri na iwatengenezee soko na iwatengenezee namna ambavyo wanaweza wakakopa.

Kwa mfano, vijana wana vipaji tofauti tofauti wale ambao wana vipaji vyatya useremala mathalani watafutiwe namna ya kukopa vifaa vyatya kufanyia kazi. Kwenye lile soko waunganishwe na Halmashauri, wapewe kazi ya kutengeneza madawati watakapoizua Halmashauri madawati kiasi cha pesa kiende kwao na kiasi cha pesa kiende kulipia zile mashine. Lakini tuna vijana wa Chuo Kikuu watakaomiliza wengi sana katika muda sio mrefu kuanzia muda huu, wale vijana nashauri kwenye huu mpango itengenezwe sheria ambayo itaruhusu cheti chao cha taaluma pamoja na kitambulisho cha uraia kuwa ndio dhamana yao ya kuweza kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zingine zinafanya hivyo kwa hiyo hii itaweza kuwaruhusu vijana wanapomaliza Chuo Kikuu kutokuelekeza malengo yao kwenye kuajiriwa peke yao lakini watakuwa wameweza kupata mitaji na kuweza kubuni miradi wakiwa *fresh* kutoka vyuoni na kuweza kutekeleza miradi ya maendeleo na hii itatusaidia kuwafanya wasomi wetu wanapomaliza waweze kutengeneza ajira. Hili ni jambo jema sana kwa sisi viongozi tuwafanye wale watu wafikirie. Maana yake kuna watu wengine *they make them stop thinking so that they can be followers. The best leader creates leaders rather than followers.* Kwa hiyo, kwenye hili tuwatengeneza vijana kwenye namna ambayo watafikiria waweze kuwaajiri vijana wengine ambao hawakupata fursa ya kufika katika elimu hiyo.

Lakini jambo la mwisho niliongelee kwenye matumizi ya ardhi. Serikali tujikite sana kwenye kurekebisha matumizi ya ardhi. Kumekuwepo na mwingiliano mkubwa sana ambao unatishia.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge muda wako umekwisha.

MHE. MWIGULU L. N. MADELU: Naunga mkono hoja hii, naunga mkono mpango huu, ni ahadi nzuri kwa maisha ya Watanzania na Watanzania wote tuupokee kwa mikono miwili. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mwongozo.

MWENYEKITI: Ndiyo Mwongozo.

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia kifungu cha 68 (7). Mwongozo ninaomba chini ya Kanuni 64 ambayo kwa ruhusa yako Mwenyekiti naomba niisome; “Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge (a) hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Sehemu ya (f) inasema hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwingine yoyote.”

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelazimika kusimama kuomba Mwongozo wako chini ya Kanuni hiyo kwa sababu Mheshimiwa David Kafulila alipokuwa anachangia

mpango ambao tunaendelea kuujadili hapa Bungeni alinitaja kwa jina kwamba wapo Wabunge wanaomba rushwa na akataja jina langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *character assassination*, ameharibu jina langu kwa umma kwa sababu Watanzania wanafuutilia Bunge hili, lakini pia amekidhalilisha chama ambacho kimenipitisha mimi kuwa Mbunge, lakini pia jitihada zangu za kuwatetea Watanzania, kuwasemea Watanzania ndani ya Bunge na nje ya Bunge zinajulikana. Kwa sababu Mheshimiwa Davidi Kafulila alisema Mheshimiwa Zambi nilimkamata akipokea rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umtake athibitishe kwa kukuandikia wewe barua akiweka vielelezo vyote ili niweze kupata nafasi ya kwenda kwenye vyombo vinavyohusika na kuujua ukweli. Zipo tabia za Wabunge ambao zimezuka sasa na baadhi ya watu ambao pengine maadili na mimi namwelewa Mheshimiwa David Kafulila maana najua alitoka CHADEMA na huko tu alifukuzwa kwa sababu ya kutokuwa na tabia nzuri ya kuwasema sema wenzake vibaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kuendeleza hili ndani ya Bunge, ninaomba athibitishe pasipo na mashaka kwamba...

MHE. MOSES J. MACHALI: Mwongozo wa Spika.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge huwezi kuomba Mwongozo juu ya Mwongozo. Mheshimiwa Zambi malizia muda wako. (*Makofi*)

MHE. MOSES J. MACHALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, umeniruhusu Mwongozo huo, lakini Mwongozo wangu hujaujibu? Kwa hiyo, hata Mwongozo ambao unaendelea si halali, kwa sababu Mwongozo wangu bado hujaujibu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, samahani Mwenyekiti akisimama wewe unakaa ndio utaratibu. Mwenyekiti akisimama wewe unafanya nini, unakaa.

MBUNGE FULANI: Mwambie Zambi akae naye.

MWENYEKITI: Mwongozo wako ulikuwa na jibu lake na huu ulioomba nao utakuwa na jibu lake, Mheshimiwa Zambi endelea. (*Makofi*)

MHE. GODFREY W. ZAMBI: Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ndiyo matatizo ya Wabunge wanaojiita vijana wanataka waendelee kulipuka na Watanzania wawaone ili waone kwamba wanajua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hatua zichukuliwe ili ukweli ujulikane juu ya jambo hili. Ahsante sana. (*Makofi*)

MBUNGE FULANI: Mwongozo

MWENYEKITI: Mheshimiwa hivi Kanuni mnazisoma? Huwezi ukaomba Mwongozo wakati Mwongozo mwingine haujatolewa Mwongozo wake.

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitoe Mwongozo ufuatao, natumia Kanuni ya 68(7). Mheshimiwa Mbunge umeomba Mwongozo, lakini kifungu hiki kinaniruhusu mimi Mwenyekiti kutoa Mwongozo wa jambo hili katika muda wowote nitakaoona unafaa. (*Makofi*)

Labda nikisome kwa faida ya wengine; “Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu wa Spika yatatolewa papo hapo au baadae kadri atakavyoona inafaa.”

Kupitia kifungu hiki na kuhusiana na jambo hili hili ilikuwa nimeombwa Mwongozo na nilisema Mwongozo huo utatolewa kwa muda amba o itaonekana inafaa. Sasa nichukue nafasi hii pia kutoa Mwongozo kwako kwamba hata huo Mwongozo unaouomba wewe basi utatolewa wakati huo amba muda huo utakuwa umeonekana unafaa kufanya hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge yule aliyekuwa anachangia tunaomba aendeleee. Anayefuatia sasa ni Mheshimiwa Pauline Gekul.

Basi kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge muda wetu uliosalia hautoshi Mbunge mwingine kuendelea kuchangia zimebakia kama dakika 10 niombe basi Bunge lirezee.

(*Bunge lilirudia*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwapongeze kwa michango mizuri na kwamba hoja hii itaendelea tena kesho. Ninayo matangazo machache.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Katibu wa Wabunge wa *CUF* anaomba kuwatangazia Wabunge wote wa *CUF* kuwa wanatakiwa kuhudhuria kikao kitachofanyika leo saa 2.00 usiku baada ya kuahirisha Shughuli za Bunge ukumbi namba 227 ghorofa ya pili.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo kesho itaendelea na wachangiaji waliobakia bado ni wengi lakini amba wanapaswa kuijandaa na wataanza kesho ni kuanzia Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Mendrad Kigola, Mheshimiwa Mariam Kisangi na wengine wataendelea. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hapa mezani sina matangazo yoyote, naomba sasa kulahirisha Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

(*Saa 1.37 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne,
Tarehe 14 Juni, 2011 saa tatu asubuhi*)

